

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**



**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA
WA FEDHA 2010/2011**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Sanduku la Posta 9080,
Simu: 255 (022) 2115157/8
Nukushi: 255 (022) 2117527
Barua pepe: ocag@nao.go.tz
Tovuti: www.nao.go.tz
DAR ES SALAAM,
Tanzania.

Machi, 2012



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080,
Dar es Salaam. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi: 255(022)2117527,
Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. CA.27/442/01

Tarehe 28 Machi, 2012

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Sanduku la Posta 9120,
Ikulu,
DAR ES SALAAM.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa
Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma
kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebisha 2005) kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya 3 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, nawasilisha kwako ripoti yangu ya tano ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo 125 kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2010, 31 Disemba, 2010 na tarehe 30 Juni, 2011.

Nawasilisha kwako kwa ajili ya kuwasilisha Bungeni kulingana na matakwa ya sheria.

Ludovick S.L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

**Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

***(Imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)***

Kazi na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainishwa katika Ibara 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebisha 2005) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008.

Dira ya Ofisi

Kuwa kituo bora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.

Lengo la Ofisi

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya misingi ifuatayo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalam inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Kujali Watu	Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na tija.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya Taasisi.
Matumizi bora ya rasilimali za umma	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

YALIYOMO

Ukurasa

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.....	ii
Dira ya Ofisi na Lengo la Ofisi	ii
SHUKRANI.....	vii
DIBAJI	ix
MUHTASARI	xi
SURA YA KWANZA.....	1
Utangulizi na Taarifa za Jumla.....	1
SURA YA PILI	10
Aina za Hati za Ukaguzi Zilizotolewa	10
SURA YA TATU	16
Muhtasari wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita	16
SURA YA NNE	30
Ukaguzi wa Mishahara katika Vyuo Vikuu.....	30
SURA YA TANO	45
Ukaguzi wa Menejimenti	45
SURA YA SITA.....	53
Uzingatiaji wa Sheria za Manunuzi na Mikataba	53
SURA YA SABA.....	67
Usimamizi wa Rasilimali	67
SURA YA NANE	81
Usimamizi wa Rasilimali Watu.....	81
SURA YA TISA.....	92
Utawala Bora	92
SURA YA KUMI.....	104

Vitega Uchumi vya Serikali, Maendeleo ya Ubinafsishaji na Ufuatiliaji wa Tathmini ya Mashirika Yaliyobinafsishwa	104
SURA YA KUMI NA MOJA	112
Matokeo ya Kaguzi Maalum	112
SURA YA KUMI NA MBILI.....	125
Hitimisho na Mapendekezo	125
VIAMBATANISHO	140

MAJEDWALI

Ukurasa

Jedwali Na.1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi za Mashirika ya Umma.....	7
Jedwali Na.2: Mchanganuo wa Hati Zilizotelewa	14
Jedwali Na.3: Nakisi Iliyokuwa Inapatikana Kutokana na Serikali kutoa Fedha kidogo za Mishahara.....	37
Jedwali Na.4: Watumishi Wenye Cheki Namba zaidi ya Moja.....	42
Jedwali Na.5: Barua kutoka MUCCoBS	43
Jedwali Na.6: Wadaiwa wa Muda Mrefu	68
Jedwali Na.7: Mashirika yenye Udhaifu katika Usimamizi wa Vifaa Ghalani	71
Jedwali Na.8: Mifuko ya Pensheni Iliyotoa Mikopo Chuo Kikuu Dodoma.....	73
Jedwali Na.9: Upungufu wa Wafanyakazi katika Nafasi Muhimu Kiutendaji kwenye Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji wa Dodoma	83
Jedwali Na.10: Mwenendo wa Mapato ya Serikali kutokana na Gawio, Ulipaji Mikopo na Mapato Mengine.....	107

VIELELEZO

Ukurasa

Kielelezo Na.1: Kinachoonyesha Mgawanyo wa Kazi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine.....	8
Kielelezo Na.2: Kuwasilisha Hesabu.....	13
Kielelezo Na.3: Mchanganuo wa Hati Zilizotolewa	15
Kielelezo Na.4: Mwenendo wa Mapato ya Serikali Kutokana na Gawio, Ulipaji Mikopo na Mapato.....	108

SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za mara kwa mara za kutilia msisitizo kwenye ripoti zangu za jumla za mwaka za ukaguzi.

Shukrani zangu za dhati pia ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyekiti na waheshimiwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma na kwa kujitolea kwao kujadili mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti yangu.

Napenda, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na wafanyakazi wote wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo za Umma zilizokaguliwa kwa ushirikiano walioutoa kwa wakaguzi wakati wa zoezi zima la ukaguzi.

Vilevile, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha uchapaji wa ripoti hii na hivyo kuifanya itoke na kuweza kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge kwa muda uliowekwa kisheria.

Zaidi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabia wa maendeleo ambao wamekuwa wakitoa msaada kwa Ofisi yangu na hususani Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Sweden (SIDA), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO) na Mpango wa Maboresho wa Menejimenti ya Fedha za Umma (PFMRP) chini ya uratibu wa Benki ya Dunia, na wadau wote wanaoitakia mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa.

Zaidi ya hayo, napenda kuzishukuru Kampuni Binafsi za Ukaguzi ambazo zimekuwa zikifanya kazi za ukaguzi na Ofisi yangu katika ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo za Umma.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kujitolea kwao na uvumilivu waliouonyesha

katika kukamilisha ripoti hii, umekuwa wa manufaa na faraja sana kwangu.

Kwa ujumla wigo wa ukaguzi umepanuka baada ya Shirikisho la Asasi Kuu ya Kikaguzi (SAI) la Tanzania kuungana na Uingereza pamoja na China kuunda Bodi ya Ukaguzi wa Umoja wa Mataifa ambapo Ofisi yangu itahusika na ukaguzi wa hesabu za Umoja wa Mataifa kwa miaka sita ijayo kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Nawasihi wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi waendeleo kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na umoja kwa siku zijazo ili kuendelea kudumisha heshima ya Ofisi yetu katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora, kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo na matumizi ya rasilimali za Umma.

DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya tano ya mwaka kuhusu taarifa ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2011. Ripoti hii ni majumuisho ya ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma zilizofanyika kwa kipindi husika. Ripoti hii inaonyesha masuala kadhaa yanayozorotesha ufanisi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma katika kutekeleza malengo waliyojiwekea.

Ripoti hii pia, inalenga kuwapa wadau wetu kama vile Serikali, Bunge, Mahakama, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kijamii na Umma wa Watanzania kwa ujumla, muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2011, pamoja na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa Mashirika na Taasisi hizo. Ripoti hii imechambua mambo mbalimbali ambayo yameonekana kwa njia moja au nyingine kuathiri ufanisi na uwajibikaji wa Mashirika hayo katika kufikia malengo yake. Kwa kipindi hiki ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la uwajibikaji kwa umma, limekuwa ni jambo muhimu kwa watendaji kutoa taarifa zao za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha na usimamiaji wa mali za umma ndani ya Mashirika na Taasisi za Umma. Napenda kueleza kuwa ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008.

Ili kuhakikisha kuwa kazi yangu inachangia katika maendeleo ya Taifa, Ofisi yangu imekuwa ikiboresha mbinu za ukaguzi mara kwa mara ili kuona kuwa matokeo ya kaguzi yanakidhi haja za wadau wetu. Kujenga uwezo wa wakaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni jambo linalopewa kipaumbele ili kuhakikisha kuwa wanapata uelewa wa sheria, miongozo, kanuni na matoleo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayofanywa na Taasisi za taaluma ya uhasibu na ukaguzi za kimataifa kama vile “IFAC”, “INTOSAI” na nyinginezo ambazo ofisi yangu ni mwanachama.

Mafunzo ya wakaguzi yalisisitizwa na Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya uzinduzi wa Jengo la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tawi la Morogoro uliofanyika tarehe 16 Januari, 2012. Alisema kwamba ‘mafunzo ya wakaguzi ni muhimu sana ukizingatia hasa kwa wakati huu ambapo

mbinu mpya za wizi wa rasilimali za umma umejitokeza. Bila mafunzo ya mbinu za kisasa, wakaguzi watakuwa wamepitwa na wakati. Wakaguzi wanatakiwa kuwa na ujuzi wa ziada ukilinganisha na wahasibu hata kama wanasoma masomo sawa ya kitaaluma. Wanatakiwa waimarishwe na mbinu mpya za ukaguzi na hii itawezekana kwa njia pekee ya mafunzo”. Msisitizo huu ulifanywa kufuatia hotuba ya ukaribisho iliyofanywa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina mpango wa kujenga Kituo cha Mafunzo ya Ukaguzi katika eneo la Gezaulole Kigamboni-Dar es Salaam.

Ni vyema ikafahamika kwamba, wakati vyombo vyenye dhamana ya uangalizi (Oversight Organs) vina jukumu la kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zinafuatwa ndani ya Taasisi za umma, Bodi za Wakurugenzi na Maafisa Watendaji Wakuu wa Taasisi hizo kwa upande wao, wana jukumu la kuweka mifumo imara ya udhibiti wa ndani na miongozo ili kuhakikisha kwamba sheria na taratibu hizo zinazingatiwa.

Juu ya yote, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa ujumla, Kamati za Bunge za usimamizi wa utendaji, Bunge, Wadau wa Maendeleo na Benki ya Dunia na wananchi kwa jumla kwa michango yao katika kufanikisha uwajibikaji katika nchi yetu.

Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

MUHTASARI

i. Utangulizi

Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi hoja mahususi zilizojadiliwa kwa kina katika sura husika za ripoti hii na zinazohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti husika ili kuhakikisha utendaji wa Mashirika ya Umma wenye ufanisi.

Mambo yanayozungumzwa yanajumuisha: mwelekeo wa maoni ya ukaguzi kulingana na kifungu cha 33(2) cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka, 2008. Utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Usimamizi wa Mishahara, Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba, Usimamizi wa Rasilimali, Usimamizi wa Rasilimali Watu, Utawala Bora, Maendeleo ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika yaliyobinafsishwa, ukaguzi wa Menejimenti na Ukaguzi Maalum kama ifuatavyo:

ii. Hali ya Ukaguzi na Ripoti zilizokamilika

Kufikia tarehe 5 Machi, 2012 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 125 (71%) kati ya kaguzi 176 zinazotakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kaguzi zilizokamilika kuna mashirika 107 ambayo ripoti zake zimetolewa maoni ya ukaguzi na kusainiwa, wakati mashirika 18 yanasubiri hesabu kuthibitishwa na kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi. Sababu kuu ya kuchelewa kusainiwa kwa ripoti hizi ni kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi katika baadhi ya mashirika na kuchelewa kuitisha vikao vya Bodi kwa wakati kama sheria inavyoelekeza. Hali kadhalika, pamekuwepo na ucheleweshwaji wa majibu juu ya hoja za ukaguzi uliophelekea kuchelewesha zoezi la ukaguzi kumalizika kwa wakati. Ninashauri mamlaka husika, kuhakikisha kwamba Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati pindi muda wake unapokwisha.

iii. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita

Katika ripoti za miaka iliyopita, kuna jumla ya mapendekezo 31 ambayo bado hayajatekelezwa na yameandikwa kwa muhtasari katika sura ya tatu ya ripoti hii kwa nia ya kuitaka Serikali na

Wadau wengine ambao mapendezo hayo yanawahusu moja kwa moja na wanawajibika kuyatekeleza.

Ikumbukwe kwamba malengo ya kutoa mapendekezo katika ripoti za mwaka ni kuona kuwa yanatekelezwa ili kuboresha uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma yenye kuleta tija na thamani ya fedha katika Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

iv. Usimamizi wa Malipo ya Mishahara

Wakati wa mapitio ya taarifa na kumbukumbu zinazohusu utaratibu wa malipo ya mishahara kwa Vyu vikiu vya Umma, nilibaini kutowiana kwa kumbukumbu kati ya Hazina, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Vyu Vikuu. Kimsingi, tofauti hizi zilisababishwa na kuwepo kwa mawasiliano hafifu kati ya taasisi hizi, kutokuwepo na uoanishi wa taarifa zinazotunzwa na idara husika, upungufu wa fedha na kucheleweshwa kutolewa kwa fedha kutoka Hazina, na wakati mwingine kuwepo kwa wafanyakazi wa mikataba ya muda mfupi katika Vyu Vikuu.

Haya yote kwa ujumla yalisababisha Hazina kupeleka fedha vyuoni tofauti na kiasi kilichohitajika kuwalipa wafanyakazi na wakati mwingine fedha za mishahara zilipelekwa zaidi ya kiasi kilichotakiwa na hakuna marejesho yaliyowasilishwa Hazina.

Pia ukaguzi ulibaini kuwa Hazina ilituma fedha katika vyuu kwa watumishi ambao walishaondoka katika ajira za Vyu Vikuu husika. Katika mwaka wa ukaguzi Hazina ilituma jumla ya Shilingi milioni 612.1 kwenda Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), Shilingi milioni 134.74 kwenda Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Shilingi milioni 194.4 kwenda Chuo Kikuu Mzumbe (MU), Shilingi milioni 181 kwenda Chuo cha Ustawi wa Jamii na Shilingi milioni 778.7 kwenda Chuo Kikuu Kishiriki cha Ualimu Dar es Salaam (DUCE). Fedha hizi zilitumwa vyuoni kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi ambao walishaacha kazi kwa sababu mbalimbali.

Pia nilibaini kwamba, Hazina imekuwa ikipeleka fedha pungufu kwenye Vyu Vikuu vya Umma kiasi ambacho hakitoshelezi malipo ya mishahara kwa watumishi. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha

Mzumbe kwa miaka mitatu mfululizo kutoka 2008/09 hadi 2010/11 fedha za mishahara zilizopelekwa zilikuwa pungufu kwa jumla ya Shilingi bilioni 1.1.

v. Ukaguzi wa Menejimenti

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilifanya ukaguzi wa menejimenti kwa mashirika manne ambayo ni; Shirika la Ndege Tanzania, Mamlaka ya Udhambi wa Mawasiliano Tanzania, Shirika la Madini la Taifa na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Moja ya mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi wa Shirika la Madini la Taifa ni kukosekana kwa Mamlaka ya usimamizi wa sekta ya madini nchini. Hivyo basi, Serikali inapasawsa iangalie uwezekano wa kuunda Mamlaka itakayosimamia na kuratibu shughuli za sekta ya madini nchini ili kuhakikisha fursa sawa kwa wadau wote walioko katika sekta hiyo.

Pia, Shirika la ndege limekuwa likijiendesha bila Bodi ya Wakurugenzi kwa muda mrefu na hii imepelekea kudorora kwa shughuli za shirika hilo. Baada ya bodi ya mwanzo kuisha muda wake mwezi Machi, 2010, shirika lilibaki bila bodi hadi mwezi Agosti, 2010 Serikali ilipoiongezea bodi iliyokuwa muda wake umeisha mpaka tarehe 31 Machi, 2011. Hivyo, tangu mwezi Aprili 2011 hadi wakati wa kuandika taarifa hii, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) halikuwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Mkataba kati ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na Shirika la ndege la Afrika Kusini ulivunjika kutokana na sababu mbalimbali za kiutendaji. Baada ya kuvunjika kwa Mkataba huo Septemba 2006, Shirika la Ndege Tanzania lilisaini mkataba mwingine wa makubaliano na kampuni ya China Sonangol International Holdings Limited. Kampuni hii ilileta ndege mbili chakavu ambazo zilikuwa zikitumiwa na shirika jingine kinyume na makubaliano. Ndege zilizoletwa ni aina ya Bombardier Dash 8-Q400s ambazo zilikuwa zimekwishatumiwa na mashirika mengine ya ndege na nyingine aina ya Airbus A320 ambayo ilikuwa na umri wa miaka 10 hadi kufikia mwaka, 2007. Januari 2009 ndege aina ya Airbus A320 ilipaswa ipelekwe kwenye matengenezo makubwa yafanyikayo kila baada ya miaka 4 - 5. Matengenezo haya yanajulikana kama “Check D au “the

Heaviest Check for the Airplane au Heavy Maintenance Visit (HMV)". Mnamo mwezi Julai, 2009 ndege hii ilirudishwa kwa mwenyewe.

Kutokana na matatizo hayo, Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuliunda upya Shirika la Ndege, kulipatia fedha za kutosha kwa ajili ya kuliwezesha kufanya kazi zake vizuri. Hata hivyo, Shirika la Ndege la Tanzania lina wafanyakazi wengi ambao hawatumiki kutokana na kupungua kwa shughuli za shirika na hivyo kuwa ni gharama kwa Serikali. Ni maoni yangu kwamba, kama shirika litaweza kuundwa upya na likapewa mtaji wa kutosha na likawa na uongozi bora na madhubuti, na kusiwepo na muingiliano wa kiutendaji, shirika litafanya kazi vizuri na kurudisha imani ya watazania.

vi. Usimamizi wa Sheria za Manunuzi na Mikataba

Manunuzi yasiyoendana na sheria yametolewa taarifa katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ambapo Mamlaka hii ilifanya manunuzi ya mfumo wa mawasiliano katika bandari zake kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 1.0 nje ya mpango wa manunuzi wa Mamlaka. Pia mamlaka hii katika hali nyingine isiyo ya kawaida ilishindwa kumlipisha mkandarasi tozo ya kiasi cha dola za Kimarekani elfu 95.3 lililotokana na kosa la mkandarasi kushindwa kutekeleza vipengele muhimu katika mkataba wa kufunga mfumo wa mtandao wa mawasiliano bandarini (Internet). Kasoro nyingine iliyotolewa taarifa katika Mamlaka ya Bandari ni ile ya kutumia kiasi cha Shilingi milioni 92.5 kumlipa Mkandarasi fidia kutokana na mamlaka kuvunja mkataba wa ujenzi wa uzio katika bandari ya Mtwara. Tozo hili lililotokana na kosa la mamlaka kuvunja mkataba kwa sababu ya kutokuwepo kwa fedha za kutosha za kumlipa mkandarasi.

vii Usimamizi wa Rasilimali

Katika ukaguzi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) nilibaini kwamba mfuko ulitumia Shilingi bilioni 234.1 kujenga Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), chini ya makubaliano ya buni, jenga, miliki na hamisha miliki baada ya miaka kumi (10). Mifuko mingine iliyochangia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu Dodoma kwa makubaliano hayo hayo ni Mfuko wa Pensheni kwa wafanyakazi wa Serikali Kuu (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mtaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa

Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) ambayo yalichangia jumla ya Shilingi bilioni 181.3.

Majengo haya hayako kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hii inatokana na uelewa tofauti uliopo kati ya pande mbili zinazohusika. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inafahamu kwamba kiasi cha fedha kilichotumika kujenga majengo hayo kilikuwa ni mikopo kwa Serikali wakati Serikali inafahamu kwamba kilikuwa ni uwekezaji wa mifuko hiyo.

Mikopo mingine isiyolipika yenye udhamini wa Serikali ni ya jumla ya Shilingi bilioni 91.7 na dola za Kimarekani milioni 9.65 ikiwa ni mikopo ya ujenzi wa ukumbi wa Bunge Dodoma, Nyumba za Polisi, Jengo la Machinga, Kiwanda cha Matairi cha Arusha ambapo makampuni binafsi ambayo mikopo yale hailipiki kwa mujibu wa makubaliano ni Mgodhi wa Makaa ya Mawe Kiwira, Kiwanda cha Saruji Dar es Salaam, Continental Venture Ltd, Kiwanda cha Sukari Kagera na Medtch Industrial Co.Ltd yote yakiwa na udhamini wa Serikali.

Kutolipika kwa mikopo hii iliyodhaminiwa na Serikali kunaiweka mifuko hii ya hifadhi katika hatari ya kupoteza fedha za wanachama na kuhatarisha uwezo wa mifuko kufanya uwekezaji zaidi.

Zaidi ya hayo, nimebaini kwamba kutokurejeshwa kwa mikopo hii kwenye Mifuko ya Hifadhi na Serikali kutolipa dhamana iliyoweka kwenye mikopo hii ni kinyume na Sheria ya Udhhamini ya mwaka 1974.

Matatizo mengine makubwa yalionekana katika usimamizi wa mali ghalani. Ilionekana kuwepo kwa mlundikano wa madawa yaliyokwisha muda wake yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 8.4 katika Bohari Kuu ya Madawa ya Serikali (MSD). Madawa haya yaliyokwisha muda wake yamekuwa yakilimbikizwa tangu mwaka 2002. Pia ilibainika kutokuwepo kwa ulinganifu sahihi wa madawa yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.08 yaliyohesabiwa na yasiyolingizwa katika vitabu. Moja ya sababu zilizochangia tofauti hii ni pamoja na upotevu au ugawaji wa madawa usio sahihi. Tatizo jingine linatokana na kutokuwepo na usimamizi madhubuti wa fedha katika Taasisi mbalimbali za Umma.

viii Usimamizi wa Rasilimali Watu

Mapungufu kadhaa yamebainika kuhusiana na usimamizi wa rasilimali watu kama ilivyoielezwa katika sura ya nane (8). Moja ya upungufu mkubwa ulikuwa ni kuondolewa kwa wafanyakazi 115 wa Kituo cha Elimu Kibaha kutoka kwenye orodha ya mishahara ya Hazina na hivyo kusababisha kituo kutumia fedha za maendeleo kulipia mishahara ya wafanyakazi na hivyo kupata nakisi ya shilingi milioni 86.1 kwenye bajeti ya maendeleo. Ukaguzi ulibaini pia kwamba baadhi ya mashirika ya umma huajiri wahasibu na wakaguzi wasiokuwa na sifa za kuwa wakuu katika vitengo vya uhasibu na ukaguzi kwa mujibu wa matakwa ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi. Utaratibu huu unaweza kuleta wasiwasi juu ya usahihi wa taarifa za kiuhasibu zinazoandaliwa. Mapungufu mengine yalikuwa ni kucheleweshwa kuwasilishwa kwa makato ya kisheria.

ix Utawala Bora

Kasi ya utekelezaji wa hoja mbalimbali zinazohusu utawala bora ambazo zimetolewa tangu mwaka 2006/2007 siyo ya kuridhisha kwa sababu mapendekezo mengi hayajafanyiwa kazi kama ilivyoielezwa katika sura ya tatu (3) na tisa (9) ya ripoti hii. Mapendekezo hayo ni kama yalivyoielezwa hapo chini;

- a. Bunge ni chombo kikuu chenye majukumu ya kutathmini utendaji kazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo za Umma, hivyo basi si sahihi kwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma.
- b. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, linapaswa kufikiria kupanua majukumu ya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma (POAC) katika kuhakikisha kuwa Kamati inakuwa na nguvu ya kikanuni za bunge katika kusimamia hesabu za Mashirika na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa, hata kama Serikali inamiliki asilimia chini ya 50.
- c. Mwenendo mzuri ungelikuwa kwa Watendaji Wakuu kuteuliwa na Bodi za Wakurugenzi badala ya kuteuliwa na mamlaka moja. Rais angeachiwa jukumu la kuteuwa Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma.

- d. Serikali inapaswa kuingia mikataba ya kiutendaji na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma. Bodi hizo zinapaswa kuwajibika kwa Serikali kwa matokeo ya utendaji kazi, vilevile, Bodi za Wakurugenzi zinapaswa kusaini mikataba na Watendaji Wakuu ambao nao wataingia mikataba na wafanyakazi waliopo chini yao katika Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali. Kwa Kufanya hivyo ni dhahiri kuwa itaboresha uwajibakaji na utendaji kazi katika Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma.
- e. Ili kuleta ufanisi katika utendaji wa bodi za wakurugenzi, ninapendekeza Msajili wa Hazina alitazame kiundani suala la malengo ya uanzishwaji wa mashirika na kuchukua hatua madhubuti inapobidi za kutoa maelekezo ya utendaji ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Mashirika ya Umma.
- f. Katika utendaji wa kamati za ukaguzi na wakaguzi wa ndani, ninapendekeza kwamba miundo ya ukaguzi wa ndani na ya kamati za ukaguzi iundwe ipasavyo kwa ajili ya tathmini ya udhitibi wa ndani madhubuti.
- g. Serikali inapaswa kutoa maelekezo mahususi ya jinsi ya kupanga posho za wakurugenzi wanaosimamia Mashirika ya Umma ili kuondoa mazoea ya wakurugenzi kujipangia posho zao bila idhini ya Msajili wa Hazina au Waziri mwenye dhamana katika shirika husika.
- h. Mashirika yote ya Umma yanatakiwa kuhakikisha yanafuata maagizo yanayotolewa na Serikali na pia kutoa michango yao kwa Hazina kama waraka Na.8 wa Msajili wa Hazina ulivyoelekeza. Pale ambapo Mamlaka haziwezi kutimiza maagizo hayo, basi zitoe taarifa kwa chombo husika ili kupata ufafanuzi wa kufanya vinginevyo.
- i. Serikali inapaswa kuhakikisha Ofisi ya Msajili wa Hazina inafanya kazi kwa mujibu wa matakwa ya sura ya 418 ya Sheria ya Msajili wa Hazina. Vinginevyo Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha Mamlaka itakayokuwa na majukumu ya kudhibiti utendaji na kusimamia shughuli za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo

kama ilivyokuwa Tume ya Kudumu ya ya mashirika ya Umma (SCOPO).

- j. Bodi za Wakurugenzi zimekuwa zikiingilia kazi za Menejimenti jambo ambalo ni kinyume na taratibu za utawala bora. Masuala ya kiutendaji ya shirika yanatakiwa kutekelezwa na menejimenti, Bodi za Wakurugenzi zinapaswa kutathmini utendaji wa menejimenti katika kufikia mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati wa shirika. Hali hii inaleta mgongano wa kimaslahi kati ya menejimenti na bodi za wakurugenzi.

Mbali na mapendekezo hayo ya miaka iliyopita, Serikali pia inapaswa kutekeleza mapendekezo mengine kama yafuatayo;

- k. Kumalizika kwa muda wa bodi za wakurugenzi kumeathiri kwa kiasi fulani lengo langu la kukamilisha ukaguzi wa baadhi ya ripoti kwa kuwa, haikuwezekana kwa hesabu zilizokaguliwa za mashirika hayo kupitishwa na bodi. Kwa kuzingatia kwamba muda wa bodi za wakurugenzi huisha kwa nyakati tofauti, inakuwa vigumu kwa mamlaka ya uteuzi kuzifuatilia kiurahisi. Kutokana na hilo, nashauri Msajili wa Hazina aanzishe uwekaji wa kumbukumbu “database” ya wakurugenzi wa bodi za mashirika ya umma ili kuweza kufuatilia muda wa bodi unapokwisha ili kuziwezesha mamlaka za uteuzi kupata taarifa kwa ajili ya kuteua bodi mpya kwa wakati.
- l. Serikali itambue kwamba watu binafsi wenye kupenda utawala bora na wenye nia ya dhati juu ya taaluma za ukurugenzi unaofuata utawala bora, hivi karibuni wameunda taasisi ya wakurugenzi nchini. Taasisi inatarajia kutoa mwelekeo, mafunzo, huduma za kiushauri kwa wanachama wake na kuongoza na kufadhili utafiti juu ya ukurugenzi wa mashirika na juu ya masuala ya kiutawala.

Hata hivyo, taasisi hii iko katika hali ya uchanga na hivyo mambo muhimu yahasuyo uendeshaji wake kama kujenga uwezo, uandaaji wa miongozo ya uendeshaji na uandaaji wa kanuni za maadili za wajumbe wa bodi hayajakamilika. Kwa kutambua umuhimu wa taasisi hii katika kukuza utawala bora nchini, Serikali iangalie uwezekano wa kuunga mkono mpango wa taasisi itakayowezesha kukuza utawala bora Tanzania. Mamlaka ya uteuzi akiwemo

Msajili wa Hazina kwa siku zijazo atumie taasisi hii katika uteuzi wa bodi za wakurugenzi wa mashirika yetu ya umma.

x Taarifa ya Ubinafsishaji wa Mashirika Yaliyosalia kwa Ajili ya Ubinafsishaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mashirika Yaliyokwisha Binafsishwa

Mpaka muda wa kuandaa ripoti hii, mashirika 34 ambayo yalishatengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji yalikuwa bado yapo kwenye hatua mbali mbali za ubinafsishaji. Kimsingi mashirika haya yako kwenye hatua zile zile yalipokuwa wakati wa kuandika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ya mwaka jana 2009/2010. Hii inaashiria aidha ufanyaji kazi usioridhisha wa Shirika Hodhi la Mali za Umma au matatizo kwenye sehemu nyingine zinazo husika kwenye mchakato wa ubinafsishaji. Serikali ni inapaswa iamue ama kuharakisha zoezi la kukamilisha zoezi la ubinafsishaji kwa mashirika yaliyosalia ili kuepusha kuharibika kwa rasilimali zilizopo au ibadilishe maamuzi yake na kuyapa mashirika hayo mtaji yaweze kufanya kazi kwa ufanisi.

xi Matokeo ya Ukaguzi Maalum

Matokeo ya kaguzi maalum yalibaini mambo yafuatayo:-

Ilionekana kuwa, kulikuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina na Wizara ya Fedha zilihusika moja kwa moja katika uuzwaji wa Kiwanja Na.10 kilichopo kando ya barabara ya Nyerere kilichouzwa kwa kampuni ya Mohamedi Enterprises Tanzania Ltd bila kuishirikisha Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC).

Nilibaini kuwepo kwa sintofahamu katika Hati ya madai ya Shilingi bilioni 2.4 kutoka katika kampuni ya DRTC kama gharama za ulinzi na tozo la matumizi ya barabara ya kuingia kwenye kiwanja Na.192 kando ya barabara ya Nyerere.

Mapungufu yalionekana pia kwenye uuzwaji wa jengo la kampuni ya Tanzania Motors (TMC) lililopo kiwanja Na.24 kilichopo kando ya barabara ya Ali Hassani Mwinyi.

Pia, Menejimenti ya CHC haikuwa makini kwenye uuzaji wa kiwanja Na. 33 kilichopo katika eneo la viwanda la Chang'ombe kwa

kampuni ya Maungu Seed. Menejimenti ya CHC ilifuta madeni yaliyorithiwa kutoka Kampuni ya SIMU 2000 na iliyokuwa PSRC bila kuwa na uthibitisho wa kushindikana kulipwa kwa madeni hayo ya muda mrefu. Kwa ujumla ukaguzi maalum wa CHC ulionyesha Serikali ilihusika kufanya maamuzi katika Shirika la CHC ambayo hayakuwa na tija wala manufaa na wala hayakuzingatia thamani ya fedha.

Ukaguzi Maalum wa Chuo cha Ubaharia cha Dar es Salaam (DMI) ulibaini, kuwepo kwa malipo yanayotia shaka na malipo ya posho mbali mbali ya kiasi cha Shilingi milioni 83.9 kilicholipwa bila kufuata sheria za fedha na bila kupitishwa na Baraza la Ushauri la Chuo. Ukaguzi ulibaini pia kuwepo watumishi wa Chuo wanaolipwa mishahara kwenye ngazi ambazo hawastahili na bila kupitishwa na Baraza la Ushauri la Chuo na kinyume na Sheria za Utumishi za Chuo. Komputa 25 zilizotolewa kama msaada kwa maabara ya Chuo kutoka Chuo Kikuu cha Leeds Metropolitan cha London bado hazijapokelewa chuoni hapo licha ya kulipiwa gharama za ushuru tangu tarehe 7/12/2007. Kulionekana pia kuibiwa vifaa vya Komputa katika maabara ya Chuo na mtumishi aliye ajiriwa kwa muda mfupi (temporary employee) chuoni hapo.

Ukaguzi maalum wa Bohari ya madawa (MSD) ulibaini kuwa, Bajeti ya Serikali ya kununua madawa na vifaa vya matibabu imekuwa ikipungua kila mwaka hivyo kusababisha upungufu na ukosefu wa dawa na vifaa vya matibabu kwa MSD. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haipeleki MSD fedha zote inazopelekea kutoka Hazina kwa ajili ya manunuzi ya dawa na vifaa vya matitabu ambapo kuna kiasi cha Shilingi milioni 658.9 ambacho hakikupelekwa MSD. Serikali haijalipa deni la Shilingi bilioni 40 inazodaiwa na MSD. Kwa upande mwingine ilionekana kuwepo kwa upungufu au kukosekana kabisa kwa dawa muhimu katika mahospitali na kuwepo kwa dawa na vifaa vya matibabu vinavyotolewa na MSD bila kukidhi viwango. MSD ilionekana kuwa na mapungufu katika kuzingatia sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 kwa kufanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi bilioni 7.0, manunuzi ya Dola za kimarekani milioni 23.46 na mengine ya Euro milioni 4.7 bila kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

1.0 Uanzishwaji wa Kazi ya Ukaguzi Kisheria

Ofisi ya Taifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ofisi ya kikatiba iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 iliyorekebisha mara kwa mara. Ukaguzi wa umma Tanzania umeelezewa zaidi kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na kifungu cha 44 (2) cha Sheria Na.21 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004.

Mamlaka ya kukagua Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine yameandikwa katika Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyorekebisha mara kwa mara, na ilivyoelezwa zaidi kwenye kifungu cha 32 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008. Katika uhusiano huo, kifungu cha 33(1) cha Sheria hiyo, inamwezesha Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumruhusu mtu au kampuni kukagua, au kuchunguza kwa niaba yake vitabu vya hesabu vya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine kama ilivyofafanuliwa zaidi katika Sera na Mwongozo wa Ugawaji Kazi za Kikaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine ya Januari, 2009 (*Policy and Guidelines for Contracting out Public Authorities and Other Bodies of January, 2009*)

Katika kuelewa mwongozo wa kisheria unaoongoza kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine, ni vizuri kuelewa pia kwamba Mashirika mengi yanafuata viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu na miongozo mbali mbali inayotolewa na Serikali kuhusiana na utayarishaji wa taarifa ya hesabu. Vile vile, Mashirika ya Umma na Taasisi

Nyinginezo zinazingatia sheria ya makampuni Na. 12 ya mwaka 2002 au sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge inayohusu shirika husika katika kuandaa mahesabu na kuyawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

1.1 Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

1.1.1 Mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ya Kuandaa Taarifa

Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa yake ya mwaka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo tarehe 31 Machi ya kila Mwaka. Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaelekeza watu wanaohusika kuwasilisha taarifa hizo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge ndani ya siku saba tangu kikao hicho cha Bunge kilipoanza. Kama Rais hatachukua hatua zozote za kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha nakala ya taarifa yake kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano (au Naibu wa Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo, au ikiwa kwa sababu yoyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha taarifa hizo Bungeni. Kimsingi, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo hujadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

1.1.2 Mamlaka ya Ukaguzi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kulingana na kifungu cha 30 na 32 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo kinampa mamlaka

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni kwa nia ya:-

- Kuzuia na kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyokuwa na tija,
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya Umma,
- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu udanganyifu au rushwa kuhusiana na fedha na raslimali za Umma.

1.2 Wigo na Viwango Katika Ukaguzi

1.2.1 Wigo wa Ukaguzi

Tunapozungumzia wigo wa ukaguzi huwa tunamaanisha maeneo ambayo yatakaguliwa. Kwa kawaida wigo wa ukaguzi unajumuisha, nia ya ukaguzi, aina ya ukaguzi na mbinu za kukagua zilizotumika na muda uliotumika kwenye ukaguzi. Nia na madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kwenye mahesabu ya Mashirika ya Umma yanayoishia tarehe 30 Septemba, 2010, 31 Disemba, 2010 na tarehe 30 Juni, 2011. Pia inajumuisha mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa za kaguzi za miaka iliyopita ambayo hayajatekelezwa kazi na mamlaka husika.

Zaidi, ripoti yangu ya mwaka inajumuisha matokeo ya kaguzi maalum na ukaguzi wa menejimenti zilizokamilika katika kipindi husika. Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya aina yeyote ya ukaguzi atakayoona inafaa. Matokeo ya kaguzi maalum yameelezwa zaidi katika sura ya 4, 5 na 11 ya ripoti hii.

Ukaguzi unaangalia ubora wa mifumo ya kiuhasibu, ubora wa mifumo ya udhibiti wa ndani, ubora wa hesabu, taarifa za utendaji kazi na mbinu nyingine za kiukaguzi zinazoonekana ni muhimu katika kutoa maoni ya ukaguzi.

Kwa hiyo atakachokitolea taarifa mkaguzi kwenye ukaguzi wake kitategemea upatikanaji wa kumbukumbu, nyaraka na taarifa zilizoombwa na mkaguzi.

1.2.2 Utumiaji wa Viwango vya Ukaguzi

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Asasi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI), Shirikisho la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika kwa Nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAL-E) na Jumuiya nyingine za Kimataifa katika taaluma ya ukaguzi. Hivyo, tunatumia Viwango vya Kimataifa (ISSAIs) vilivyotolewa na Shirikisho la Asasi Kuu za Ukaguzi Duniani (INTOSAI) na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Hivyo, wakati wa kufanya kaguzi zetu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ina jukumu la kipekee la kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu katika matumizi, uwajibikaji na uwazi. Pia, ofisi ina jukumu la kutoa ripoti iliyo bora na kwa wakati unaofaa inayoelezea namna raslimali za Taifa zilivyotumika.

1.3 Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu

Jukumu la kutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu kwa madhumuni ya ukaguzi ni la Bodi ya Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine. Kiwango cha kwanza cha Kimataifa cha utayarishaji wa Taarifa za Hesabu na kiwango cha kwanza cha Kimataifa cha Uhasibu vinaelezea aina za taarifa za hesabu zinazotakiwa kutayarishwa. Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine hapa nchini zinapaswa kutayarisha hesabu zao kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) au viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS), kulingana na hali halisi na majukumu ya Mashirika ya Umma na Taasisi husika. Hii ni kutokana na uamuzi uliofanywa na Bodi ya Taifa

ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na kuungwa mkono na Serikali. Kuanzia Julai 2004 Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo Tanzania zilitakiwa kutengeneza hesabu zake kwa kufuata viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) na ukaguzi utafuata viwango vya ukaguzi vya kimataifa (ISA) na sheria nyingine zinazotolewa mara kwa mara na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo ni jukumu la kisheria lililoainishwa kwenye Sheria zilizoanzisha Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002. Pia, kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. II ya mwaka 2008.

Ripoti za mwaka za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zinawawezesha wananchi kupima ufanisi wa utendaji kazi wa Mashirika hayo na kuona yanawajibika ipasavyo katika kutumia raslimali za Umma. Hesabu zinazowasilishwa kwa wakati zinawezesha ukaguzi na uandaaji wa ripoti hii ukamilike kwa wakati.

1.4 Mifumo ya Udhhibiti wa Ndani

Mifumo ya udhibiti wa ndani ni namna ambavyo Mashirika ya Umma yanapangilia mifumo katika kuhakikisha kuwa rasilimali za Umma zinatumiwa ipasavyo. Udhhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma.

Kwenye taasisi yeyote, lengo la udhibiti wa ndani ni kuhakikisha uaminifu katika kutoa ripoti ya mahesabu, kupata majibu kwa wakati kuhusu mafanikio ya malengo iliyojiwekea na kuhakikisha sheria na kanuni zinatekelezwa.

Tukiongelea malipo na manunuzi mbalimbali katika Mashirika ya Umma, udhibiti wa ndani una maana ya hatua zilizochukuliwa ili kufikia malengo mbalimbali yaliowekwa kwa mfano, namna ya kuhakikisha kuwa malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma na mali za shirika ni sahihi na halali. Kuangalia kama udhibiti wa ndani unafuatwa ni kazi ya mkaguzi wa ndani wa shirika husika.

1.5 Majukumu ya Msajili wa Hazina

Kulingana na Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 418 na kifungu Na. 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.16 ya mwaka 1992, inaeleza kwamba Msajili wa Hazina ana kazi na majukumu ya kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika.

1.6 Mpangilio wa Ripoti Hii

Ripoti hii inaelekeza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi uliofanywa katika Mashirika kwa kipindi husika. Ili kutimiza malengo na kazi zangu kikatiba, niliamua kushirikiana na makampuni binafsi ya ukaguzi katika kufanya kazi. Katika kutekeleza wajibu huu, tulifanya kazi hizo kwa kushirikiana, au kwa kuziachia kampuni binafsi zenyewe kufanya ukaguzi chini ya usimamizi wa ofisi yangu.

Kazi za ukaguzi zilizofanywa na makampuni binafsi kwa niaba yangu ziliwasilishwa kwenye ofisi yangu ili kuhakiki ubora wake kabla ya kumaliza kazi za ukaguzi na baadaye kutoa ripoti husika.

Katika mwaka husika, Ofisi yangu ilifanya kazi kwa pamoja na kampuni binafsi za ukaguzi 52 ambazo ziliomba kufanya kazi na ofisi yangu na ambazo zimesajiliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa

Hesabu (NBAA). Kama inavyoonyeshwa kwenye kiambatanisho Na. I cha ripoti hii.

1.7 Kuwasilisha Hesabu kwa Ajili ya Ukaguzi

Kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008, kinawataka Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kutayarisha hesabu katika kipindi cha miezi mitatu baada ya tarehe ya mwisho wa kila mwaka wa fedha na kuziwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

1.8 Uteuzi wa Makampuni Binafsi ya Ukaguzi

Kifungu Na. 33(5) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya 2008, kinampa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kumruhusu mtu au kampuni yoyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na.33 ya mwaka 1972 (iliyorekebishwa mwaka 1995) kufanya ukaguzi kwa niaba yake na kuwezesha kupeleka ripoti kwa wakati Bungeni. Wakaguzi watakaoteuliwa watafuata Sheria kama inavyotakiwa na hawatakuwa na mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza wajibu wao. Wajibu wa kutoa maoni ya ukaguzi ni wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe. Katika mwaka husika, ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo 176 ulifanyika kama ifuatavyo:


Jedwali Na.1: Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi za Mashirika ya Umma

Na	Maelezo	Mashirika	Asilimia
1.	Mashirika yaliyokaguliwa na Ofisi yangu	25	14.2
2.	Mashirika yaliyokaguliwa kwa kushirikiana na Makampuni Binafsi ya Ukaguzi	13	7.4

3.	Mashirika yaliyokaguliwa na kampuni binafsi kwa niaba yangu chini ya usimamizi wa Ofisi yangu	138	78.4
Jumla		176	100

Taarifa hiyo hapo juu inaweza kuonyeshwa kwenye kielelezo kama ifuatavyo:-

Kielelezo Na.1: Kinachoonyesha Mgawanyo wa Kazi za Ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo



Idadi ndogo ya Mashirika ya Umma, yaani asilimia 14.2 ndiyo yaliyokaguliwa na maafisa wa ofisi yangu. Hii ni ishara ya upungufu mkubwa wa wafanyakazi na inahitaji wafanyakazi wa ku tosha na wenye ujuzi ili kuweze kukabiliana na changamoto mbalimbali ninazokumbana nazo.

Majina ya makampuni binafsi ya ukaguzi yaliyotumiwa na ofisi yangu yameorodheshwa kwenye kiambatanisho Na. I cha ripoti hii.

1.9 Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo

Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo unafanywa na kusimamiwa na Idara ya Ukaguzi wa mashirika ya Umma. Kwa sasa Idara hii haina watumishi wa kutosha kuhimili wingi wa kazi za ukaguzi katika kumwezesha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika Ibara 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ilivyofafanuliwa zaidi na kifungu cha 32 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008. Matokeo yake kaguzi chache ambazo ni asilimia 14.2 zinafanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na zaidi ya asilimia 78.4 ya kaguzi zinafanywa na makampuni binafsi ya ukaguzi kwa niaba yangu.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina Idara ya Mashirika ya Umma inayohusika na kuandaa, kuratibu na kusimamia kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine zinazofanywa na ofisi yenyewe, ukaguzi wa pamoja na ukaguzi wa kampuni binafsi. Kaguzi zikikamilika, wajibu wa kutoa maoni ya ukaguzi ni wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 33 (3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Idara ina upungufu wa wafanyakazi. Kwa hiyo, ili kukidhi matarajio ya umma katika uwajibikaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyingine, inabidi Idara hii iimarishwe zaidi.

SURA YA PILI

AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi kuhusu hesabu zilizokaguliwa ili kumwezesha mtumiaji kujua kama Hesabu hizo zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu, vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na vile vinavyotolewa na Bodi za Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa.

Kulingana na kanuni za ukaguzi, nia ya kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa maoni ya ukaguzi yanayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya shirika na zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyotakiwa.

Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji juu ya Hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika, na kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika ya kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa makubwa yanayotokana na wizi ama makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

Ukaguzi wa taarifa za hesabu za sekta ya Umma hapa nchini ni kwa mujibu wa matakwa ya sheria ambayo yameelezwa na Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofafanuliwa na kifungu cha 43 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambayo inaeleza kuwa “baada ya kupokea taarifa za hesabu kwa mujibu wa sheria, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakagua hesabu hizo ndani ya miezi tisa (9) baada ya tarehe ya mwisho ya mwaka wa

hesabu husika na kutoa maoni ya ukaguzi wa kila hesabu na matokeo ya ukaguzi”.

2.1 Aina za Hati za Kaguzi

2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa, na vile vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika kimataifa.

2.1.2 Hati Inayoridhisha na yenye Suala la Msisitizo

Suala la msisitizo halibadilishi hati ya ukaguzi kutoka hati inayoridhisha, bali kuleta uelewa zaidi wa hali ilivyo ndani ya Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati inayoridhisha.

2.1.3 Hati Yenye Shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu. Maelezo ya hati yenye shaka yanafanana sana na hati inayoridhisha lakini aya ya ufafanuzi inaongezwa ili kuelezea sababu zinazoleta shaka. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zinaonyesha vizuri hali ya kifedha isipokuwa kwa kasoro zitokanazo na masuala yaliyohojiwa.

2.1.4 Hati Yenye Shaka na Suala la Msisitizo

Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapokutana na mazingira ya kutokukubaliana na menejimenti au mazingira yenye shaka ambayo yana athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa hesabu.

Aya ya suala la msisitizo inaambatanishwa wakati kunahitajika uzingatiaji wa haraka kutoka kwa Watendaji Wakuu na watumiaji wa taarifa za fedha kuwatahadharisha kuhusu masuala hayo yanayohitaji kushughulikiwa haraka. Hata hivyo, lengo kuu la suala la msisitizo ni kuleta karibu uelewa wa hali ilivyo ndani ya Shirika au Taasisi iliyokaguliwa ingawa imepewa hati yenye shaka.

2.1.5 Hati Isiyoridhisha

Aina hii ya hati ni moja wapo ya sababu zinazoweza kubadilisha hati ya ukaguzi. Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu hesabu zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri hesabu kiasi cha kushindwa kutoa maoni kuhusiana na hesabu hizo. Katika hali ambayo hati hii inatolewa ni pamoja na kukosa uhuru wa kufanya kazi ya ukaguzi ipasavyo kunapokuwa na wigo finyu wa kupata taarifa kwa ajili ya ukaguzi ama kwa kukusudia au kutokukusudia ambako kunazuia kazi ya mkaguzi kupata vielelezo vya kutosha.

2.1.6 Hati Isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapona kuwa taarifa za fedha za Shirika la Umma au Taasisi nyinginezo kwa kiasi kikubwa zina makosa na zikiangaliwa kwa ujumla wake hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu vinavyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu na zile zinazotolewa na Taasisi Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa. Hati hii inaonekana kuwa ni kinyume cha hati inayoridhisha. Kimsingi hati hii hueleza kwamba taarifa zilizomo katika hesabu za Shirika au Taasisi kwa kiasi kikubwa si sahihi wala za kuaminika kwa ajili ya kutathmini hali ya kifedha na matokeo ya kiutendaji ya Shirika au Taasisi husika.

2.2 Hali Halisi ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma

Ripoti hii ya ujumla ya Mashirika ya Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2011 itajadili ripoti 176 za Mashirika ya Umma ukilinganisha na ripoti 170 zilizoripotiwa kwenye ripoti ya ujumla ya mwaka 2009/2010. Hali hii inatokana na kujumuishwa kwa Bodi ya Mazao, Bodi ya usajili wa Maghala, Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Kijamii, SNOTASHIP, Mamlaka ya Maji Kahama Shinyanga na Baraza la Wafugaji Ngorongoro kwenye orodha ya Mashirika yanayokaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2011, Maafisa Watendaji Wakuu wa mashirika 175 waliwasilisha hesabu zao kwenye ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa. Shirika moja (1) ambalo ni Usafiri Dar es Salaam halikuwasilisha hesabu zake kwa mantiki kuwa kwa sasa sio shirika la umma. Kaguzi 125 zilihitimishwa, kaguzi 18 zilikuwa zinasubiri kupitishwa na bodi za wakurugenzi, kaguzi 16 zipo katika uboreshaji, kaguzi 34 zinaendelea.

Kwa kifupi, taarifa hii inaonyeshwa kwenye jedwali kama ifuatavyo:

Kielelezo Na.2: Kuwasilisha Hesabu

Na	Kundi la shirika	Idadi ya Mashirika Niliyo Paswa Kukagua	Ripoti Zilizokamilika	Ripoti za Ukaguzi Zinazosubiri Kupitishwa Na Bodi za Wakurugenzi	Kuhakiki Ubora Wa Ukaguzi	Kaguzi Zinazoendelea	Hesabu ambazo Hazijawasili Shwa
1.	Taasisi za fedha, Mifuko ya pensheni na kampuni za Bima.	16	12	-	2	1	-
2.	Taasisi za uzalishaji.	18	9	6	1	3	-
3	Bodi za udhibiti, Mabaraza, Kamisheni	61	37	6	8	8	-

	Na Mamlaka						
4	Vyuo vya elimu ya juu, Tafiti, Mafunzo.	36	19	5	4	10	
5	Mashirika ya kutoa huduma.	45	30	1	1	12	1
Jumla		176	107	18	16	34	1

Hali halisi ya uwasilishaji wa hesabu na ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma kufikia tarehe 5 Machi 2012 ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Kiambatanisho Na. III cha taarifa hii.

2.3 Hati Zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma

Kufikia tarehe 5 Machi, 2012 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 125 (71%) kati ya kaguzi 176 zinazotakiwa kukakaguliwa na ofisi yangu. Katika kaguzi zilizokamilika, mashirika 107 ripoti zake zimeshasainiwa wakati mashirika 18 yanasubiri hesabu kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi za mashirika husika. Kati ya kaguzi zilizosainiwa, kaguzi 84 (78.5%) za Mashirika ya Umma zilipata hati inayoridhisha, kaguzi 12 (11.3%) zilipata hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo. Kaguzi 7 (6.5%) zilipata hati zenye shaka, kaguzi 4 (3.7%) zilipata hati zenye shaka zenye masuala ya msisitizo na hakuna shirika lililopata hati isiyoridhisha.


Aina ya Hati zilizotolewa na Mashirika husika ni kama ilivyoonyeshwa kwenye kiambatanisho Na.II cha ripoti hii.

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Hati zilizotolewa

Mashirika	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha yenye msisitizo	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka na msisitizo	Hati kushindwa kutolewa
125	84	12	7	4	0
100%	78.5%	11.3%	6.5%	3.7%	0.0%

Mchanganuo hapo juu unaweza kuonyeshwa kwenye pai chati kama ifuatavyo:

Kielelezo 3: Mchanganuo wa Hati zilizotolewa



SURA YA TATU
MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA
UKAGUZI YA MIAKA ILIYOPITA

3.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha kwa muhtasari mapendekezo ya Ukaguzi ya ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za miaka iliyopita, ambayo bado hayajatekelezwa. Mapendekezo hayo yapo aidha kwenye hatua za utekelezaji au hayakutekelezwa kabisa hadi ilipofikia wakati wa kuandaa ripoti hii. Ili Serikali iweze kufikia malengo ya utawala bora wenye kuleta uwajibikaji na kufanikisha malengo ya kila Shirika la Umma na Taasisi Nyinginezo, kunahitajika jitihada madhubuti za Serikali za kusimamia na kuhakikisha mapendekezo yanayotolewa kila mwaka yanatekelezwa. Hata hivyo, maagizo hayo ambayo hayajatekelezwa yanahitaji kupewa kipaumbele siyo tu na Serikali bali pia kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC), Wakurugenzi wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zinazohusika.

3.1. Majibu ya Ripoti ya Mwaka Uliopita (2010)

Nakiri kupokea majibu ya ripoti ya mwaka uliopita kupitia barua ya Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu Na. EB/AG/485/01/VOL.III/31 ya tarehe 28 Juni, 2011. Hata hivyo, katika majibu hayo ya mapendekezo yaliyotolewa kutokana na kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo kwa mwaka uliopita hayakuwa na msimamo ulioonyeshwa na upande wa Serikali kama kuna jitihada madhubuti zinazochukuliwa kushughulikia mapendekezo ya mapungufu yaliyojitokeza kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo katika ripoti iliyopita.

Katika ripoti zilizopita zinazohusu kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo kwa miaka iliyoishia tarehe 30 Juni, 2008, 30 Juni, 2009 na 30 Juni, 2010, nilitekeleza wajibu wa ofisi yangu kwa kutoa mapendekezo kwa nia ya kuzuia na kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuiepushia Serikali hasara zinazotokana na uzembe, kutowajibika, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu na vitendo vya rushwa. Mapendekezo hayo pia yanalenga kuhakikisha kuwa Mashirika ya Umma yanaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora ambayo italeti ufanisi na kuyawezesha Mashirika hayo kufikia malengo yaliyokusudiwa. Uendeshaji mzuri wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo utaboresha utoaji wa huduma zilizo bora na uzalishaji mali unaokidhi matakwa ya Wadau wa Taasisi na Mashirika husika na kuleta maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Kwa kuzingatia misingi hiyo nimeona ni vyema kuyarudia tena mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zilizopita ambayo yanahitaji kutekelezwa na Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma, ikiwa ni kukumbushia kuwa bado kuna mapendekezo ambayo ama hayajatekelezwa kabisa au utekelezaji wake bado unaendelea na kunahitajika uwajibikaji wa pamoja katika kuyatekeleza.

Ufuatao ni muhtasari wa mapendekezo ambayo hayajatekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008:-

3.1.1 Mtaji Mdogo wa Mashirika ya Umma

Msajili wa Hazina anapaswa kuhakikisha kuwa Mashirika ambayo hayana mtaji wa kutosha, yanapatiwa fedha kwa ajili ya kuyaendesha kwa kuanzisha vyanzo mbalimbali vya mapato ili yaweze kufanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa umma.

3.1.2. Mamlaka Itakayosimamia Mashirika ya Umma

Serikali inapaswa kuanzisha Mamlaka itakayokuwa na majukumu ya kudhibiti utendaji na kusimamia shughuli za Mashirika ya Umma kama ilivyokuwa SCOPO.

3.1.3. Haja ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina Kuendana na Tamko la Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 418

Endapo Ofisi ya Msajili wa Hazina haitafanya kazi kwa mujibu wa Sura 418 ya Sheria ya Msajili wa Hazina, Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi itakayokuwa na jukumu la kudhibiti, na kusimamia uendeshaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali 176 zenye hisa/mtaji yenye jumla ya shilingi trilioni 10.3 katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika kutoa huduma nzuri kwa Umma. Vinginevyo, Serikali iwasilishe muswada Bungeni wa kuifuta Sheria ya Msajili wa Hazina - Sura ya 418.

3.1.4. Utawala Bora

Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anapaswa kuangalia uwezekano wa kupanua majukumu ya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma (POAC) katika kuhakikisha kuwa Kamati ina utaratibu uliopata nguvu ya kikanuni za Bunge wa kusimamia na kuhoji maswala ya taarifa za fedha za Taasisi na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa, hata kama ni chini ya asilimia 50.

3.1.5. Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika

Utawala bora ni kuwa Watendaji Wakuu kuteuliwa na Bodi za Wakurugenzi badala ya kuteulia na mamlaka moja. Rais angeachiwa jukumu la kuteuwa Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wakati uteuzi wa Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi

Nyinginezo lingekuwa ni jukumu la Bodi za Wakurugenzi ili Bodi za Wakurugenzi ziweze kuwajibisha menejimenti za Mashirika kwa kutowajibika.

3.1.6. Uwekezaji DAWASCO

Menejimenti ya Shirika la Maji Dar es Salaam (DAWASCO) inapaswa kuwekeza kwenye uchimbaji wa maji ardhini ili yatumike kwa eneo kubwa la Jiji la Dar es Salaam ambalo halina maji ya kutosha. Pia, Shirika lipitie upya viwango vya ankara za maji ili kuiwezesha DAWASCO kulipa gharama zake za uendeshaji.

3.1.7. Kuanguka kwa Uchumi wa Dunia

Serikali inapaswa kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali, kuziba mianya ya ukwepaji kulipa kodi hususani kwenye mafuta ya magari na mitambo, kupunguza misamaha ya kodi na kupanua wigo wa kodi ili kuweza kuhimili mtikisiko wa uchumi duniani.

3.1.8 Udhibiti wa Matumizi ya Serikali

Serikali inapaswa kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima kama vile ilivyoamua kupunguza manunuzi ya magari ya kifahari na kupunguza gharama za semina. Pia, matumizi ya kawaida yanaweza kusimamiwa vizuri zaidi ili mapato yanayokusanywa yatumike kwenye shughuli za maendeleo.

3.2 Ufuatao ni muhtasari wa mapendekezo ya mwaka 2008/2009 ambayo bado hayajatekelezwa:-

3.2.1. Mgongano wa Maslahi kwa Wabunge kwa Kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali

Bunge ndicho chombo kikuu kinachowakilisha wananchi na chenye majukumu ya kutathmini utendaji kazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kupitia kwa

Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC). Hivyo basi, siyo utawala bora kwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma. Katika mkutano wa Uwajibikaji uliofanyika tarehe 23 hadi tarehe 24 Januari, 2009 iliamuliwa kuwa Wabunge wasiteuliwe kuwa wajumbe katika Bodi za Mashirika ya Umma. Ili kuondoa mgongano wa kimaslahi, Wabunge hawapaswi kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo. Mwenendo huu ni wa kipekee na upo tu Tanzania na hautumiki mahali popote katika Jumuiya ambayo Tanzania ni mwanachama, kwa mfano EAC, SADCOPAC, SADC, AFROSAI-E, AU na hautumiki katika nchi yoyote duniani.

3.2.2. Uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi

Serikali inapaswa kuingia mikataba ya utendaji na Wakurugenzi wa Bodi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo. Wakurugenzi hao wanapaswa kuwajibika kwa Serikali kwa matokeo ya utendaji kazi, vilevile Wakurugenzi wa Bodi hizo wanatakiwa kuingia mikataba na Watendaji Wakuu ambao nao wataingia mikataba na wafanyakazi waliopo chini yao katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo. Kwa Kufanya hivyo ni dhahiri itaboresha uwajibikaji na utendaji kazi katika Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

3.2.3. Haja ya Kuanzishwa Mfuko wa Umma wa Uwekezaji

Siyo siri kwamba Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zimegubikwa na matatizo mengi, kubwa ikiwa ni ukosefu wa mitaji ya kutosha ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo. Serikali inapaswa kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kuweza kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazokabili uwekezaji wa serikali kwenye taasisi mbali mbali. Gawio na misaada ya wahisani inayopatikana katika nyanja hii zinaweza kuwekwa katika mfuko huu. Fedha hizo hazipaswi

kutumiwa katika shughuli za matumizi ya kawaida bali zinaweza kutumika kwenye miradi ya maendeleo kama vile miradi mipya, kuongeza mitaji na kutoa mikopo nafuu kwa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zinazohitaji.

3.2.4. Kuchelewa Kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali

Serikali na Mamlaka husika za uteuzi zinapaswa kuhakikisha kuwa Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa mapema pale muda wa Bodi unapokwisha, kutokana na ukweli kwamba kuna madhara makubwa yanayotokana na kuchelewa kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo. Katika mwaka huu ukaguzi, mashirika 12 hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi kama zilivyoonyeshwa Kiambatisho V cha taarifa hii.

3.2.5. Ajira za Kudumu za Pensheni Vis-a-Vis Ajira za Mkataba kwa Wafanyakazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali

Kuna haja ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM), kuhusishwa katika kupitisha miundo ya ajira ya aina hii kwa wafanyakazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo kutoka kwenye ajira za kudumu na pensheni kwenda kwenye ajira za utendaji na mikataba.

3.2.6. Kutokuwepo kwa Usawa Katika Marupurupu Yatolewayo na Mashirika ya Umma

Kuna haja ya Serikali kuhakikisha kuwa kuna uwiano katika marupurupu wanayopata Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma, na Taasisi Nyinginezo, kutokana na ukweli kwamba rasilimali wanazotumia ni rasilimali za umma kama ilivyokuwa kabla ya kuvunjwa kwa Kamati ya Kudumu ya Mashirika ya Umma (SCOPO).

3.3. Ukaguzi Maalum Uliofanyika TRL

3.3.1 Malipo ya Nyongeza ya Mishahara

Kiasi kilichotakiwa kudaiwa na TRL na kulipwa na Serikali kama nyongeza ya mishahara kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Julai 2008 kingelikuwa sahihi kama kingekuwa Shilingi bilioni 1.4 na siyo Shilingi bilioni 9.8 zilizodaiwa. Kwa hiyo, TRL ilidai zaidi Shilingi bilioni 8.4 kutoka Serikalini.

3.3.2 Ada ya Makubaliano ya Maridhiano Kati ya Serikali na TRL Isiyolipwa Shilingi Bilioni 16.1

Serikali inapaswa kufanya tathmini ya ubia wake na RITES, na Serikali ihakikishe kuwa kiasi cha Shilingi bilioni 16.1 kinalipwa.

3.4 Mkopo wa PSPF Shilingi Bilioni 58 na Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi Bilioni 51.1

Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba bakaa ya deni lote la mkopo (ikiwa ni kiasi cha mkopo na riba) uliokopwa kutoka PSPF unalipwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mkopo huo. Bodi inapaswa kuanza kutekeleza hatua za kisheria kwa waajiri na wakopaji binafsi ambao hawatoi ushirikiano kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 19A-23 ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004 ili kurejesha mikopo ya kiasi cha Shilingi bilioni 51.1.

3.5. Matokeo ya Ukaguzi Maalum Yaliyofanyika TANESCO

Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO inapaswa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya 2004 na Kanuni zake za 2005, na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana wakati wa kusimamia shughuli za kila siku za Shirika hilo.

3.6. Katika ripoti ya mwaka 2009/2010, nilitoa mapendekezo mengi ambayo hayajatekelezwa, na

Serikali haikutoa majibu yanayopelekea kufanyia kazi mapendekezo hayo, ambayo yanatolewa kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

3.6.1. Usimamizi wa Mapato na Matumizi

Mapato

Usimamizi mbovu wa mapato ulionekana kufuatia kuwepo kwa kutotoa bili za wateja kwa wakati, ucheleweshaji katika ukusanyaji mapato na kutokuwa na mikakati madhubuti ya kukusanya mapato. Pia, kulikuwepo ucheleweshwaji wa kukusanya mapato na madeni kutoka kwa wateja mbali mbali, kutokuwepo kwa usahihi na uwekaji wa kumbukumbu za mapato na kutokuwepo kwa ulinzi madhubuti wa kuhifadhi fedha zilizokusanywa. TANESCO inapaswa kuongeza uzalishaji umeme ili kukidhi mahitaji ya wateja yanayoongezeka na kubuni mbinu za kudhibiti umeme unaopotea ili kuongeza mapato. Mamlaka za maji zinapaswa kuongeza jitihada za kusimika na kuboresha miundo mbinu ya maji, mifumo ya kuandaa bili za maji iboreshwe na kuwa ya kisasa zaidi sambamba na mita za maji kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mauzo katika Mamlaka hizo.

Ucheleweshwaji wa Fedha za Bajeti Kutoka Hazina

Ili kupunguza migogoro ya Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu, ambayo inaathiri elimu ya wanafunzi katika vyuo hivyo na maendeleo ya Taifa, Hazina inapaswa kutafuta njia na mikakati madhubuti ya kuhakikisha fedha za mikopo ya wanafunzi zinapelekwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya juu kwa wakati bila kuchelewa.

Matumizi

Kwa upande mwingine tathimini iliyofanyika katika matumizi ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo, ilidhihirisha kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali hazina usimamizi na udhibiti

madhubuti wa mifumo ya matumizi. Jambo hili, hupelekea matumizi mengi kufanyika bila kuwa na vibali na matumizi mengine kutokuwa na viambatanisho vya kuthibitisha kufanyika kwa matumizi hayo. Kumekuwa pia na kutorejeshwa kwa masurufu kinyume na matakwa ya sheria za fedha na hairuhusiwi kutolewa kwa masurufu mapya kabla ya masurufu ya zamani kurejeshwa na mtumishi husika.

3.6.2. Usimamizi wa Sheria za Manunuzi na Mikataba

Mamlaka ya Udhubiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) iendelee na jitihada zake za kuendeleza mradi wake wa kuyajengea uwezo Mashirika ya Umma na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi katika Mashirika ya Umma unaimarika.

Pia, Bodi ya Ugavi na Manunuzi iweke mkazo katika kuendeleza uandaaji wa wataalamu wa manunuzi, kuhakikisha kuwa yanatoa mafunzo na kuendeleza mitaala ili kufikia mahitaji ya soko nchini.

Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wahakikishe kuwa sheria za manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za 2005 zinazingatiwa. Pia, wahakikishe kuwa kunakuwepo na mfumo maalum wa kusimamia mikataba ili kuleta ufanisi.

3.6.3. Usimamizi wa Rasilimali

Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Maafisa Watendaji wa mashirika wahakikishe wanawekeza kwenye kampuni zinazofanya vizuri kiutendaji ili kuweza kupata faida kwenye uwekezaji. Pia, bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma wahakikishe wanapata umiliki wa mali na mitambo. Vile vile, Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wakubaliane kuweka viwango vya uchakavu ambavyo vinaendana na hali halisi ya matumizi na

muda wa maisha ya mitambo na mali zinazomilikiwa na mashirika ya Umma.

3.6.4. Usimamizi wa Raslimali Watu

Kuhusiana na upungufu wa wafanyakazi, hasa nafasi za uongozi, tunashauri kwamba nafasi zote zilizo wazi kama ilivyo katika chati za uongozi na zile zinazokaimiwa zijazwe. Pia, mashirika yahakikishe kuwepo kwa mpango mzuri wa kurithisha madaraka.

Menejimenti za Mashirika ya Umma zichukue hatua zinazofaa kwa lengo la kupitia upya mishahara na marupurupu ya wafanyakazi ili yaendane na masharti ya ajira ya mamlaka husika pamoja na maelekezo ya Serikali. Mashirika ya umma yahakikishe kuwa mishahara inalipwa kwa wakati. Usimamizi mzuri katika suala la ulipaji mishahara utawapa motisha wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa muda mrefu na itasaidia kupunguza idadi ya wafanyakazi wanaoacha kazi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Kwa upande wa tathmini ya utendaji kazi, inapasa menejimenti kufanya juhudi ya kutosha kuwezesha mawasiliano bora, na ya wazi mara kwa mara kati ya kiongozi na mwajiriwa; kuhusiana na wajibu na majukumu ya kazi ya mwajiriwa na malengo ya ufanisi yaliyowekwa kwa kipindi husika; kutambua na kutatua masuala ya kiufanisi na kuipatia menejimenti taarifa muhimu kwa ajili kusaidia maamuzi ya watumishi ambao huhitaji tathmini juu ya utendaji kazi wa kila mmoja wao. Njia nzuri ya kufikia lengo hili ni kutumia mfumo wa wazi wa upimaji utendaji kazi na kuhakikisha kwamba fomu za kupima utendaji kazi zinajazwa na kuhifadhiwa ipasavyo katika jalada la mwajiriwa husika ili kuweka mtiririko wa utendaji kazi wa mfanyakazi.

Kuhusiana na suala la utunzaji wa kumbukumbu za waajiriwa, inashauriwa kwamba Mashirika ya Umma yahakikishe kuwa kumbukumbu za waajiriwa zinatunzwa vizuri pamoja na kumbukumbu zote zinazohusiana na mabadiliko ya masharti ya ajira na taarifa nyinginezo kama vile fomu za tathmini ya utendaji kazi na nyinginezo kwa ajili ya utambulisho wa mfanyakazi zinatunzwa vizuri.

3.6.5. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Menejimenti za mashirika ya umma zinapaswa kuhakikisha kuwa sera za teknolojia ya habari na mawasiliano zinaandaliwa vizuri kabla ya kuzitumia, sera zipate idhini ya menejimenti na kisha kusambazwa kwa watumiaji ndani ya shirika husika. Kompyuta na mifumo yake inapaswa kutazamwa na kuboreshwa kila wakati, pia kuwepo na sera ya kujilinda dhidi ya virusi viharibifu. Menejimenti za mashirika ya umma zinapaswa kutumia kikamilifu mifumo ya kompyuta kutengeneza taarifa za hesabu. Vile vile, mashirika yanapaswa kuwa na mipango na mikakati ya udhibiti dhidi ya majanga ili kulinda kompyuta na mifumo yake pale majanga yanapotokea.

3.6.6. Kupima Utendaji Kazi wa Mashirika Yaliyopo na Yale Yaliyobinafsishwa

Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa madeni ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo ambazo marejesho yake yalikuwa yameiva lakini yalikuwa hayajarejeshwa, yanarejeshwa ili kuepuka Serikali kulipa mikopo hiyo na bakaa ya mapato ya kipindi cha nyuma yanayokusanywa bila kuchelewa.

Shirika Hodhi la Mali za Serikali zilizobinafsishwa (CHC) linapaswa kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa Mashirika yaliyobinafsishwa yanajiendesha kulingana na makubaliano ya mikataba ya mauzo, na kuchukua

hatua madhubuti kwa kampuni zote zinazojiendesha bila kuzingatia makubaliano ya mikataba ya mauzo.

3.6.7. Ucheleweshwaji wa Kuwasilisha Hesabu kwa Ajili ya Ukaguzi

Msajili wa Hazina, kama mtunzaji na msimamizi wa uwekezaji katika Mashirika ya Umma kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anapaswa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na uwasilishaji hesabu kwa ajili ya ukaguzi kwa wakati muafaka bila kuchelewa kama inavyotakiwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

3.7. Utawala Bora

3.7.1. Kanuni za Mgawanyo wa Madaraka katika Utendaji wa Mashirika ya Umma

Ninapendekeza kuwa Serikali, Bunge na Mahakama wasisitize na kulisimamia suala la mgawanyo wa madaraka na majukumu katika utendaji wa Serikali na taasisi zake. Pia, juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha kuwa kanuni za utawala bora katika mashirika zinaelekezwa hadi ngazi za chini za utendaji.

3.7.2. Udhaifu Katika Utendaji wa Bodi za Wakurugenzi

Msajili wa Hazina anapaswa kuhakikisha mashirika ya umma yanafanya kazi kwa ufanisi katika kufikia malengo ya uanzishwaji wa mashirika husika na pale ambapo mashirika hayo yanashindwa kufikia malengo yake, hatua madhubuti zichukuliwe katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa.

3.7.3. Utendaji wa Kamati za Ukaguzi na Wakaguzi wa Ndani

Ninapendekeza kwamba miundo ya ukaguzi wa ndani na ya kamati za ukaguzi iimarishwe ipasavyo kwa ajili tathmini ya udhibiti wa ndani madhubuti.

3.7.4. Bodi za Wakurugenzi Kuingilia Kazi za Menejimenti

Masuala ya kiutendaji ya shirika yanatakiwa kutekelezwa na menejimenti za shirika husika. Bodi za Wakurugenzi zinapaswa kutathmini utendaji wa

menejimenti katika kufikia mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati wa shirika.

3.7.5. Kutokufuata Waraka wa Msajili wa Hazina (Waraka Na.8)

Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zinapaswa kuhakikisha kuwa zinafuata maagizo yanayotolewa na Serikali na pia kutoa michango yao kwa Hazina kama waraka ulivyoeleza. Pale ambapo Mamlaka haziwezi kutimiza maagizo ya serikali, basi zitoe taarifa kwa mamlaka husika ili kupata idhini ya kufanya vinginevyo. Msajili wa Hazina anapaswa kuonyesha kuwa, ndiye mmiliki wa Mashirika na aanzishe sera za kudumu za kuwa mmiliki. Zaidi ya hayo, Msajili ahakikishe utawala wa Mashirika ya Umma unakuwa wa uwazi na endelevu na wa ufanisi. Inategemewa kuwa Msajili wa Hazina ataanzisha sera ya umiliki ambayo itaainisha malengo ya Msajili wa Hazina na majukumu ya utawala bora kwenye Mashirika ya Umma na namna ya utekelezaji wa sera hiyo.

3.8. Mashirika Yaliyotengwa kwa Ajili ya Kubinafsishwa

Serikali inapaswa kuangalia upya ubinafsishwaji wa mashirika 34 yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji yaliyotoka PSRC na kuchukuliwa na CHC ili kuepuka uharibifu na uchakavu wa rasilimali zinazomilikiwa na mashirika yaliyotengwa au Serikali kutoyabinafsisha na kuyaongezea mitaji na yaanze kazi upya. Mashirika hayo ni pamoja na NMB, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), Shirika la Reli la Tanzania (TRC), Shirika la Posta la Tanzania (TPC), Shirika la Maendeleo ya Viwanda na Utafiti (TIRDO), Shirika la Usafiri la Dar es Salaam (UDA) na Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL).

3.9. Mashirika ambayo Umiliki na Usimamizi Wake Unapaswa Kuwa Chini ya Serikali

Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa umiliki wa Mashirika yote muhimu ambayo hutoa huduma za msingi kwa umma unakuwa chini ya Serikali. Zaidi ya hayo, menejimenti za mashirika haya zinapaswa kutoa huduma za uhakika na kuaminika kwa wadau wake. Panapotokea matatizo ya kifedha, Serikali ihakikishe inatoa msaada unaohitajika na kwa wakati. Mashirika hayo ni pamoja na TANESCO, Shirika la ndege la Tanzania (ATCL), DAWASCO, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASA), Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA) na STAMICO.

SURA YA NNE

UKAGUZI WA MISHAHARA KATIKA VYUO VIKUU

4.0 Utangulizi

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha ina jukumu la kulipa mishahara ya watumishi katika Vyuo Vikuu vya umma. Ili kukamilisha jukumu hilo, Wizara inahitaji taarifa muhimu kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Vyuo vikuu husika. Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma inahifadhi kumbukumbu za watumishi walioajiriwa, waliohama idara kwa muda, walioacha kazi kwa hiari, waliofukuzwa kazi na wale waliostaafu.

Kumbukumbu zilizopo Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu idadi ya watumishi zinapaswa ziwe kama zilivyo katika Vyuo Vikuu vya Umma. Nilifanya ukaguzi ili kubaini ufanisi wa mfumo wa mishahara, usahihi wa taarifa kwa kila upande, usahihi wa viwango vya mishahara vilinavyotumika na udhibiti uliowekwa kusimamia fedha zinazotumwa kutoka Wizara ya Fedha. Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi:-

4.1 Ukosefu wa Ulinganishi wa Taarifa Baina ya Idara ya Fedha na Idara ya Rasilimali Watu Katika Vyuo Vikuu vya Umma

Kazi ya kuandaa mishahara katika Vyuo Vikuu imekasimiwa katika Idara ya Fedha. Kwa upande mwingine, Idara ya Rasilimali watu inatunza kumbukumbu husika za kila mfanyakazi. Kumbukumbu kutoka pande hizi mbili zinahitaji kuoainishwa ili kubaini kama zinafanana.

Mapitio ya kumbukumbu kati ya Idara ya Fedha na ile ya Rasilimali watu katika Vyuo Vikuu mbalimbali imeonyesha kutofautiana kwa idadi ya wafanyakazi

katika idara hizo. Pia imebainika kuwa baadhi ya Idara za rasilimali watu hazina kumbukumbu sahihi na za kuaminika. Ukaguzi ulibaini kuwa kuna mfanyakazi mmoja ambaye alikuwa ameacha kazi muda mrefu ambaye aliendelea kuonekana katika orodha ya mishahara ya Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi. Japokuwa mfanyakazi huyo hakuwa akilipwa mishahara yake bali hali hii ikiachwa inaweza kushawishi ubadhirifu wa fedha za mishahara.

Tulipokagua kumbukumbu za Chuo Kikuu cha Mzumbe, tulibaini kutokukubaliana kwa kumbukumbu za Idara ya Fedha na Idara ya Rasilimali Watu. Mlinganisho wa takwimu za mwaka wa 2008/09 ulionyesha kuwa, idadi ya wafanyakazi katika idara ya rasilimali watu ilikuwa kubwa kwa wafanyakazi ishirini na watatu (23) zaidi ya wale walioonyeshwa na idara ya fedha. Katika mwaka wa fedha wa 2009/10 idadi ilikuwa ndogo kwa mtu mmoja (1) na mwaka wa 2010/11 idadi katika idara ya fedha ilikuwa kubwa kwa watu ishirini na wanne (24).

4.2 Tofauti Isiyoelezeka Katika Fedha Zilizotumwa na Hazina na Zile Zilizopokelewa Katika Vyuo Vikuu Kadhaa

Mapitio ya malipo ya mishahara na marupurupu yaliyolipwa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MUCCoBS), ilionyesha tofauti ya Shilingi milioni 82.2 ikilinganishwa na mishahara kwa mujibu wa kumbukumbu za Hazina. Kumbukumbu za Hazina zinaonyesha kuwa mwezi wa Januari, 2009 fedha zilizotumwa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ni Shilingi milioni 443.2 wakati Chuo kikionyesha kupokea Shilingi milioni 360.9 tu na hivyo kusababisha tofauti hiyo. Fedha zilizopokelewa na Chuo zilithibishwa kwa kuhakikiwa katika akaunti ya Chuo na kubainika kuwa Chuo kilipokea fedha hizo kwa Hundi Na. CQ 114326. Pia tuliweza kuhakiki kuwa hiki ndicho kiasi sahihi kilichopokelewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi Stadi kutoka Hazina kwa kupitia hati ya fedha Na.000258329.

Kwa Mwezi Mei, 2010 kumbukumbu zimeonyesha kuwa Hazina ilituma kiasi cha Shilingi bilioni 1.2 kwenda Chuo Kikuu Cha Afya na Sayansi ya Tiba Muhimbili (MUHAS). Hata hivyo, kumbukumbu zilizopatikana Chuoni hapo zinaonyesha kuwa Chuo kilipokea Shilingi milioni 781.2 na hivyo kusababisha tofauti ya Shilingi milioni 372.9 ambazo maelezo yake hayakupatikana.

4.3 Makato na Ulipaji wa Kodi ya Mapato Kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Shilingi Milioni 3.95

Wakati tunapitia makato ya kodi yaliyofanywa katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), tulibaini kuwa, mtu mmoja ajulikanaye kwa jina la Stephen Ndazi aliajiriwa na Chuo mwezi Januari, 2010. Hata hivyo mtu huyo hakuweza kuripoti katika kituo chake cha kazi japokuwa aliingizwa kwenye malipo ya mshahara. Pia, imebainika kuwa pamoja na kuwepo katika orodha ya mshahara, fedha yake haikulipwa kwa mtu yeyote na makato yaliendelea kukatwa na kupelekwa katika taasisi zilizo husika na kufikia jumla ya Shilingi milioni 3.95.

4.4 Ucheleweshwaji wa Kutekeleza Maelekezo ya Waraka Namba 4 Uliotolewa na Hazina Mwezi Agosti, 2010 Kuhusu Ongezeko la Ngazi za Mishahara ya Watumishi

Katika kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa Waraka Na. 4 uliotolewa na Hazina mwezi Agosti, 2010 kuhusu ongezeko la mishahara ya watumishi, tulibaini tofauti katika mishahara iliyolipwa kwa wafanyakazi wanne (4). Tuliona kuwa wafanyakazi hao wanne hawakulipwa mishahara kulingana na viwango vipya kama vilivyoelekezwa katika Waraka wa Hazina. Kufikia mwezi Juni, 2011 kulikuwa na malimbikizo ya mishahara yenye jumla ya Shilingi milioni 14.8

Malimbikizo haya ni tofauti kati ya mishahara kwa mujibu wa ngazi sahihi za mishahara na mishahara uliolipwa kwa watumishi hao.

Katika Chuo Kikuu cha Mkwawa, tulikuta kuwa wafanyakazi walilipwa mishahara kwa kutumia ngazi za zamani hadi mwezi Novemba, 2010 ilipobadilishwa katika orodha ya mishahara ya Hazina. Kufuatia madiliko hayo, katika ngazi za mishahara, malimbikizo ya jumla ya Shilingi milioni 256.3 yalilipwa mwezi Februari, 2011. Hata hivyo, mpaka wakati ukaguzi unamalizika bado kulikuwa na malimbikizo ya jumla ya Shilingi milioni 93.7 yaliyotokana na kupandishwa vyeo watumishi wa kada ya ualimu na watumishi wengine.

Kulikuwa pia na malimbikizo ya mishahara ya jumla ya Shilingi bilioni 1.7 kwa watumishi wa Chuo Kikuu Cha Dodoma hadi kufikia Disemba 2010. Malimbikizo haya yalitokana na kuchelewa kutekeleza waraka Na.4 wa Hazina.

Pia, hali ya kuchelewa kulipa mishahara ya watumishi kwa kutumia ngazi mpya ilijitokeza katika Chuo Cha Usimamizi wa Fedha (IFM).

4.5 Serikali Kushindwa Kulipa Nyongeza ya Mwaka kwa Watumishi wa Chuo Cha Ustawi wa Jamii (ISW)

Katika Chuo cha Ustawi wa Jamii, tulibaini kuwa serikali kupitia Hazina ilishindwa kulipa nyongeza za mishahara zipatazo Shilingi milioni 20.9 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011. Hii ilibainika wakati wa kupitia nyaraka za mawasiliano kati ya Chuo cha Ustawi wa Jamii na Hazina, hususani barua yenye kumb. Na. ISW/AC/M.10/74 ya tarehe 29 Disemba, 2010 ambayo ilitumwa Hazina kama sehemu ya ufuatiliaji wa jambo hilo.

4.6 Hazina Imekuwa Ikituma Fedha Kwa Watu Ambao Siyo Waajiriwa wa Vyuho Vikuu

Wakati wa ukaguzi uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Elimu Mkwawa (MUCE), ilibainika kuwa serikali kupitia Hazina imekuwa ikituma fedha za mishahara kwa watumishi arobaini na wawili (42) ambao siyo waajiriwa wa Chuo. Tulibaini kuwa Hazina ilipeleka jumla ya Shilingi milioni 612.1 kwa ajili ya watumishi ambao waliondoka kazini kati ya mwezi Oktoba, 200 na Juni, 2010.

Katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), tulibaini kuwa serikali iliendelea kupeleka Chuoni hapo fedha za mishahara kwa ajili ya watumishi wasiokuwa watumishi halali wa chuo hicho. Watumishi ambao mishahara yao ilipelekwa wakiwa siyo watumishi halali wa Chuo ni wale walioacha kazi au waliostaafu miezi kadhaa nyuma lakini bado wameendelea kuwepo katika orodha ya mishahara ya Hazina pamoja na Hazina kupelekwa taarifa juu ya watumishi kutokuwepo katika ajira ya Chuo. Hazina ilipeleka jumla ya Shilingi milioni 134.7 chuoni kwa ajili ya watumishi wasiokuwepo kazini japokuwa fedha hizo hazikulipwa kwa watumishi hao wastaafu.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, tulibaini kuwa watumishi ambao hawako kazini waliendelea kuonekana kwenye orodha ya mishahara kutoka Hazina kwa miezi kadhaa pamoja na kuwepo taarifa mbalimbali zilizopelekwa Hazina kuhusiana na jambo hilo. Kwa kipindi cha miezi minne yaani Oktoba, 2010; Machi, 2011; Mei, 2011 na Juni, 2011 zilitolewa fedha zenye jumla ya Shilingi milioni 194.4 kwa watumishi ambao hawakuwepo kwenye ajira ya chuo.

Katika Chuo Cha Ustawi wa Jamii (ISW) watumishi waliostaafu pia wameendelea kuonekana katika orodha ya mishahara kutoka Hazina kwa miezi kadhaa. Kwa

kipindi cha mwaka 2008/2009 na 2010/2011 Hazina ilikipelekea Chuo jumla ya Shilingi milioni 181 kwa ajili ya watumishi ambao hawakuwepo kwenye ajira ya Chuo cha Ustawi wa Jamii.

Pia mapitio ya kumbukumbu na taarifa mbalimbali za Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam (DUCE) yalibaini kuwa watumishi 56 walioonekana katika orodha ya mishahara kutoka Hazina wakati siyo waajiriwa wa Chuo cha Ualimu cha Dar es Salaam. Katika kipindi cha kutoka mwaka 2008/09 na 2010/11, Hazina ilikipelekea Chuo jumla ya Shilingi milioni 778.7 kwa ajili ya watumishi ambao siyo waajiriwa wa Chuo. Kumbukumbu tulizozipitia zinaonyesha kuwa fedha hizo hazikurudishwa Hazina.

4.7 Serikali Kushindwa Kulipa Malipo ya Kiinua Mgongo kwa Watumishi wa Vyuo Vikuu Waliopo Katika Kazi kwa Mikataba

Wakati wa ukaguzi katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, tulibaini kuwepo kwa jumla ya Shilingi milioni 112.2 ambazo ni malimbikizo ya viinua mgongo kwa watumishi ambao waliajiriwa na Chuo kwa mikataba. Kiasi hiki cha fedha ni malimbikizo ya madai kwa watumishi mbalimbali waliostaafu hadi tarehe 30 Juni, 2011. Pamoja na kuwa fedha hizi ni miongoni mwa kiasi kilichowasilishwa wakati wa makadirio ya mishahara (PE) katika bajeti ya mwaka, Hazina haikupeleka Chuoni fedha hizo pamoja na mishahara. Chuo kimeshindwa kulipa malipo haya kutoka kwenye matumizi ya kawaida 'OC' kutokana na kiasi kidogo ambacho kimekuwa kikipokelewa kutoka Hazina kila mara.

Malipo ya kiasi cha Shilingi milioni 75.8 kwa ajili ya watumishi walioko katika mikataba hakikupelekwa Chuo Kikuu cha Mkwawa (MUCE). Kiasi hiki cha Fedha ni kwa ajili ya watumishi tisa (9) ambao mikataba yao

iliisha katika mwaka 2010/2011. Hazina ilitakiwa kupeleka asilimia ishirini na tano (25%) ya mishahara ya watumishi wenye mikataba ambayo hulipwa pindi mtumishi anapomaliza mkataba wake. Hata hivyo, tulibaini kuwa Hazina ilipeleka Chuoni asilimia kumi na tano (15%) wakati wa kupeleka mishahara na kuacha kupeleka asilimia kumi (10%) ambayo ni sawa na Shilingi milioni 75.8.

4.7.1 Hazina Kupeleka Fedha Nyingi Zaidi ya Zinazotakiwa Kulipa Malimbikizo ya Mishahara

Hazina ilipeleka fedha nyingi zaidi kwenye Taasisi ya Uhasibu Tanzania ili kulipa malimbikizo ya mishahara. Fedha zilizopelekwa Chuoni zilizidi fedha zilizotakiwa kulipa madeni kwa kiasi cha Shilingi milioni 18.7. Malimbikizo haya yalikuwa yametokana na nyongeza ya mishahara kuanzia Julai, 2010 ambayo ililipwa kati ya mwezi wa Februari na Machi, 2011. Hatukuweza kupata maelezo zaidi kutoka chuoni kwa taarifa kuwa hesabu hii ilikokotolewa na Hazina.

Pia Hazina ilipeleka Shilingi milioni 55.4 zaidi ya fedha iliyotakiwa kulipia michango ya Bima ya Afya (NHIF) kwa wafanyakazi wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA). Hata hivyo, iligundulika kuwa fedha hizo za ziada hazikupelekwa Bima ya Afya na wala hazikurudishwa Hazina.

4.7.2 Hazina Ilituma Shilingi Milioni 277.5 Zaidi ya Fedha Ilizotakiwa Kulipa Mishahara ya Watumishi wa Chuo Kikuu cha Mkwawa

Mapitio ya kumbukumbu katika Chuo Kikuu cha Mkwawa yameonyesha kuwa Hazina ilikipeleka Chuoni hapo fedha nyingi zaidi kuliko zilizotakiwa kulipa mishahara kwa kiasi cha Shilingi milioni 277.5. Pia ilibainika kuwa fedha hizo zilizozidi kwenye mishahara ya watumishi hazikurudishwa Hazina.

Taarifa kutoka Chuoni hapo zinaonyesha kuwa fedha hizo zilitumiwa kulipa mishahara ya watumishi ambao hawapo kwenye orodha ya mishahara ya Hazina nao walijajiriwa ili kuchukua nafasi za wafanyakazi waliostaafu, walioacha kazi, waliofukuzwa na waliofariki. Bila kuzingatia matumizi yaliyoainishwa, fedha nyingine katika hizo zilitumika kulipa posho mbalimbali ambazo hazikutolewa na Hazina kama vile posho ya majukumu. Hatukuweza kuona idhini iliyotolewa kubadili matumizi ya fedha hizo kwa kazi ambayo haikukusudiwa awali na Hazina.

4.8 Fedha Zisizotosheleza Malipo ya Mishahara Zimekuwa Zikitumwa Chuo Kikuu Cha Mzumbe (MU)

Ukaguzi uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Mzumbe ulibaini kuwa Hazina imekuwa ikituma fedha kidogo zisizotosheleza kulipia gharama za mishahara ya watumishi kila mwezi. Katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2008/09 mpaka 2010/11 chuo kimekuwa na nakisi ya jumla ya Shilingi bilioni 1.1 kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na.3: Nakisi Iliyokuwa Inapatikana Kutokana na Serikali Kutoa Fedha Kidogo za Mishahara.

Mwaka	2008/09 (Shs.)	2009/10 (Shs.)	2010/11 (Shs.)	Total (Shs.)
Iliyopokelewa	9,203,416,958	9,992,621,550	12,572,779,895	31,768,818,403
Iliyolipwa	9,735,756,140	10,026,158,854	13,090,938,382	32,852,853,378
Mapungufu	532,339,182	33,537,304	518,158,487	1,084,034,974

4.9 Hazina Kutopeleka Mishahara ya Watumishi Halali wa Chuo Kikuu Cha Mzumbe (MU)

Ulinganifu wa takwimu za mishahara kutoka Hazina na zile zinazotayarishwa na Chuo Kikuu Cha Mzumbe zilibaini kuwepo kwa majina ya watumishi wenye Cheki namba za mishahara lakini mishahara yao haikutolewa na Hazina. Fedha ambazo Hazina haikupeleka Chuoni ya watumishi hao ni kiasi cha Shilingi milioni 660.95 ya miezi ya Oktoba, 2010, Machi, 2011 na Juni, 2011.

4.10 Hazina Imekuwa Ikipeleka Fedha kwa Ajili ya Mishahara Vyuoni Ambayo ni Tofauti na Mishahara kwa Mujibu wa Mikataba ya Ajira

Wakati tunapitia kumbukumbu za malipo ya mishahara kwa watumishi wa Chuo Kikuu Cha Kilimo Cha Sokoine (SUA) tulibaini kuwa Hazina ilikuwa ikipeleka mishahara Chuoni hapo kwa ngazi tofauti na zile zinazoonekana katika mikataba ya ajira ya watumishi hao. Hazina ilitaarifiwa kuwepo kwa tofauti hizi kwa barua zenye Kumb. Na. SUA/CG/11 VOL.III ya tarehe 20 Juni, 2011 na Kumb.Na. SUA/ADMN ya tarehe 12 Mei, 2011 na SUA/CC/114 VOL.III ya tarehe 5 Oktoba, 2011. Barua hizi hazikujibiwa na Hazina. Hata hivyo, chuo kimekuwa kikilipa mishahara sahihi kama inavyoonyeshwa katika mikataba yao ya ajira na hivyo kulazimika kutumia fedha kutoka vyanzo vya ndani ili kufidia upungufu huo. Kwa wastani, Chuo kimekuwa kikipokea fedha pungufu takribani Shilingi milioni 5.1 kila mwezi. Wakati ukaguzi huu ukifanyika, upungufu huo ulikuwa umefikia jumla ya Shilingi milioni 61.6 ambao Chuo kilikuwa kimefidia kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani vya mapato.

4.11 Watumishi Walioondolewa Kwenye Orodha ya Mshahara ya Hazina Bila Mawasiliano na Vyuu Husika

Ukaguzi uliofanyika katika vyuo vikuu mbalimbali ulibaini kuwa Hazina imekuwa ikirekebisha kumbukumbu zake na kuwafuta katika orodha yake ya mshahara watumishi halali wa vyuo bila ya kuwa na mawasiliano na Vyuu Vikuu husika. Katika Chuo Kikuu Cha Sayansi ya Tiba Muhimbili (MUHAS) watumishi saba (7) waliondolewa kwenye Orodha ya mishahara ya Hazina kwa mwezi wa Novemba, 2010 bila ya Chuo kutoa taarifa ya kufanya hivyo kwa Hazina. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa watumishi hao walirudishwa kwenye orodha ya mshahara mwezi uliofuata yaani Disemba, 2010 baada ya kutaarifiwa juu ya jambo hilo na MUHAS.

Katika Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM) idadi ya watumishi themanini na watano (85) hawakuonekana katika orodha ya mishahara ya Hazina mwezi wa Oktoba, 2010, tisini (90) mwezi wa Novemba, 2010 na pia tisini (90) mwezi wa Disemba, 2010. Watumishi hao waliondolewa katika orodha ya mishahara bila taarifa kwa Chuo au Taasisi husika. Katika kipindi hicho, Hazina haikupeleka mishahara ya watumishi hao. Hatimaye walirejeshwa katika orodha ya Hazina katika miezi ya Januari, Februari na Machi, 2011. Kwa Chuo Kikuu Cha Ualimu Dar es Salaam (DUCE) tulibaini kuwa watumishi kumi na saba (17) waliondolewa katika orodha ya mishahara ya mwezi wa Juni, 2010 bila ya taarifa kwa Chuo cha Ualimu Dar es Salaam.

Hazina pia, iliondoa majina ya watumishi mia moja hamsini na wanane (158) wa Chuo Kikuu Cha Sokoine (SUA) katika orodha ya mishahara ya mwezi Novemba, 2010. Sababu za watumishi hao kuondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Hazina haikuweza kujulikana. Katika kipindi ambacho Hazina haikupeleka fedha za watumishi walioondolewa katika orodha, Chuo kiliwalipa watumishi hao kwa kutumia vyanzo vya fedha za ndani. Kufikia mwezi Disemba, 2010 watumishi hao walikuwa wamerudishwa katika orodha ya Hazina isipokuwa watumishi kumi na mmoja (11).

4.12 Watumishi wa Vyuo Wanaolipwa Mishahara Nje ya Utaratibu wa Kawaida wa Malipo ya Mshahara Kutoka Hazina

Katika kulinganisha orodha za malipo zinazotumiwa na Vyuo Vikuu kulipia mishahara pamoja na orodha zinazoandaliwa na Hazina kwa ajili ya mishahara, ilibainika kuwepo watumishi wa Vyuo Vikuu ambao majina yao hayapo katika orodha ya mishahara kutoka Hazina. Watumishi hao wamekuwa wakilipwa mishahara yao kwa kutumia fedha za vyanzo vya ndani za vyuo hivyo. Kwa miezi ya Oktoba, 2010, Machi, Mei

na Juni, 2011, Chuo Kikuu Cha Mzumbe kilitumia jumla ya Shilingi milioni 850.7 ili kulipa watumishi ambao hawakuwapo katika orodha ya mishahara ya Hazina.

Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kilikutwa na idadi ya watumishi mia mbili na ishirini (220) ambao hawakuwahi kuingizwa katika orodha ya Hazina tangu walipoajiriwa. Kutokana na hali hiyo, mishahara imekuwa ikilipwa na Chuo nje ya utaratibu wa mishahara kutoka Hazina. Katika kipindi cha miaka mitatu (2008/09 mpaka 2010/11) Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kililipa jumla ya Shilingi bilioni 1.4 kutoka vyanzo vya ndani ya Chuo, fedha ambazo hazijalipwa kutoka Hazina. Pia Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kina utaratibu wa kuajiri watumishi wa muda katika fani ya wahadhiri, utawala, wasomaji kwa ajili ya wanafunzi vipofu kwa kipindi cha kati miezi 12 na 24. Watumishi hawa wa muda hawako katika orodha ya mishahara ya Hazina, na wamekigharimu Chuo jumla ya Shilingi bilioni 2.3 kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia 2008/2009 hadi 2010/2011. Pia tuliona katika Chuo Kikuu Cha Ualimu Dar es Salaam (DUCE) palikuwa na watumishi thelathini na watano (35) wanaolipwa nje ya utaratibu wa kawaida wa mishahara ya Hazina. Hawa ni wale watumishi ambao hawana Cheki Namba za mishahara. Kwa wastani palikuwa na watumishi wa masharti wa muda mfupi wapatao mia moja kumi na mbili (112) ambao nao pia walilipwa nje ya utaratibu wa mishahara wa Hazina. Fedha iliyolipwa kwa watumishi hawa wa muda mfupi kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2008/09 mpaka 2010/11 ilifikia jumla ya Shilingi bilioni 1.2.

Katika mapitio ya kumbukumbu za mishahara katika Chuo Kikuu Cha Kilimo Cha Sokoine (SUA) ilionekana kuwa watumishi sitini na saba (67) walioajiriwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari, 2010 hadi Juni, 2011 hawakuingizwa katika orodha ya mishahara ya

Hazina. Kufikia Juni, 2011 watumishi hawa walikuwa wamelipwa jumla ya Shilingi milioni 502.3 kwa kutumia vyanzo vya ndani vya Chuo hicho. Pamoja na malipo hayo, pia Chuo Kikuu Cha Sokoine kililipa jumla ya Shilingi milioni 75.5 kwa Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) na hivyo kufikia deni la Shilingi milioni 577.6 ambazo chuo kinadai kutoka Hazina. Kuwepo kwa watumishi wengi nje ya mfumo wa mishahara wa Hazina ulisababishwa na kuchelewa kuingiza takwimu muhimu za watumishi kama ilivyodhihirishwa na barua yenye Kumb. Na. TYC/200/595/17 ya tarehe 27 Mei, 2011.

Chuo Cha Afya na Sayansi ya Tiba Muhimbili (MUHAS) kililipa mishahara kwa watumishi arobaini na wawili (42) ambao wako kwenye kazi za masharti ya muda mfupi. Katika Chuo Cha Usimamizi wa Fedha (IFM) watumishi thelathini na sita (36) ambao hawapo katika orodha ya mishahara ya Hazina walilipwa jumla ya Shilingi milioni 424.6 kwa kipindi cha kuanzia mwezi Disemba, 2009 hadi Juni 2011. Pia gharama hizi zililipwa kutumia vyanzo vya mapato vya ndani vya Chuo.

Aghalabu, malipo ya mishahara nje ya orodha ya mishahara kutoka Hazina ilijitokeza katika Chuo cha Uhasibu Arusha na Chuo Kikuu Cha Dodoma.

4.13 Watumishi Wenye Cheki Namba za Mshahara Zaidi ya Moja

Cheki namba za mshahara ni namba ya pekee ambayo anapewa mtumishi wa serikali ili kuweza kumtofautisha mtumishi mmoja na mwingine. Namba hii huweza kupunguza uwezekano wa kumlipa mtumishi mara mbili. Katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika Moshi (MUCCoBS) ilibainika kuwepo kwa watumishi wenye cheki namba za mshahara mbili tofauti. Watumishi hao ni kama walivyotajwa hapa chini:

Jedwali Na.4: Watumishi Wenye Cheki Namba za Mshahara Zaidi ya Moja

Cheki Na.	Jina	Kiasi (Sh.)
11352350	J. Messy, M	503,230
11352372	Messy, J.M	503,230
11352361	Kaombwe, L	503,230
11352383	Kaombwe, L	503,230
11358743	T. Chipanjiro	268,550
11358754	T. Chipanjiro	261,950
11826567	Nathaniel H	763,000
11351412	Nathaniel H	763,000
11351744	Simon L.M	1,628,440
11826730	Simon L.M	1,628,440

Katika kupitia orodha ya mishahara iliyotoka Hazina kwa ajili ya watumishi wa Chuo Kikuu Cha Mzumbe kwa kipindi cha kuanzia Aprili, 2010 mpaka Juni, 2011 ilibainika kuwepo kwa mtumishi mmoja mwenye Cheki Namba mbili tofauti. Cheki Namba hizo ni 11874834 na 11914163 ambazo ziko kwa jina moja. Cheki Namba 11874834 ilikuwa na mshahara wa daraja la PGSS16 yaani Shilingi 1,401,310 kuanzia Aprili, 2010 mpaka Oktoba, 2010 na mshahara wa Shilingi 1,776,830 kuanzia Novemba, 2010 mpaka Juni, 2011. Cheki Namba 11914163 ambayo ndiyo sahihi na ndiyo inayotumika ilikuwa na mshahara wa daraja la PGSS 16 yaani Shilingi 1,203,580 kuanzia Aprili 2010 mpaka Oktoba, 2010 na Shilingi 1,509,100 kuanzia Novemba, 2010 hadi mwezi Juni, 2011. Chuo cha Mzumbe kilikuwa kimepeleka taarifa Hazina lakini hakuna hatua za marekebisho zilizochukuliwa na Hazina.

Pia kuwepo na watumishi wenye Cheki Namba zaidi ya moja kulijitokeza katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chuo kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

4.14 Mapungufu Katika Mfumo wa Mawasiliano Kati ya Vyuo Vikuu, Hazina na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Ubora wa mawasiliano ni nyenzo muhimu katika kuiwezesha serikali kutimiza majukumu yake ya utoaji huduma. Katika kutathmini ubora wa mfumo wa mawasiliano katika idara mbalimbali za serikali hususani Hazina, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Vyuo Vikuu vya Umma yalibainika mapungufu mbali mbali katika mfumo wa mawasiliano. Ilionekana kuwa barua ambazo Vyuo Vikuu vimekuwa vikituma kwenda Hazina, Wizara mama, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu masuala yanayohusu mishahara zimekuwa hazijibiwi kwa wakati. Kwa Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi (MUCCoBS) barua mbili zilizoandikwa mwezi Disemba, 2010 na Machi, 2011 hazikuwa zimejibiwa hadi kufikia Julai, 2011. Hapa chini ni mfano wa barua ambazo hazikuwa zimejibiwa mpaka mwezi Julai, 2011.

Jedwali Na 5: Barua Kutoka MUCCoBS

Tarehe	Kwenda	Maelezo	Majibu
MUCCoBS 20/12/2010	MoEVT	Ombi la kibali cha ajira (kuziba pengo la walioondoka)	Hakuna majibu
MUCCoBS Kumb.Na. MF/C/4/4a/VOL.III 14/03/2011	PO-PSM	Ombi la kibali cha kuajiri watumishi 40	Hakuna majibu
MUCCoBS Kumb.Na. NHIF/1/60 09/06/2011	MoF	Madai ya michango ya Bima ya Afya (NHIF)	Hakuna majibu

Kucheleweshwa kutoa majibu ya barua zinazotumwa na Vyuo Vikuu kwenda Hazina na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM) kulijitokeza pia katika Taasisi ya Uhasibu ya Tanzania (TIA), ambapo kati ya barua kumi na nane (18) zilizotumwa, barua saba (7)

hazikujibiwa kabisa, barua nne (4) zilijibiwa kati ya miezi mitatu (3) na miezi kumi na nne (14). Barua sita (6) zilijibiwa kwa Hazina kulipa moja kwa moja madeni ya mishahara wakati barua moja ilijibiwa baada ya siku tisa (9).

Wakati mwingine barua zilizohitaji kujibiwa haraka zilikaa bila kujibiwa kwa kipindi cha takribani mwaka mzima. Ucheleweshaji wa kujibu barua umejitokeza pia katika vyuo vya Usimamizi wa Fedha (IFM), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Chuo Kikuu cha Mkwawa (MUCE).

Pia nyaraka mbali mbali kutoka Hazina na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM) hazifiki kwenye Vyuo Vikuu. Kwa mfano, tulibaini kuwa Waraka Na.2 wa mwaka 2010 Uwajibikaji na Udhibiti wa malipo ya mishahara haujapokelewa Chuo Cha Ustawi wa Jamii (ISW).

SURA YA TANO

UKAGUZI WA MENEJIMENTI

5.0 Utangulizi

Kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 kinampa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uwezo wa kufanya aina nyingine yeyote ya ukaguzi kama atakavyo ona inafaa. Ni kutokana na uwezo huo wa kisheria hapo juu ambapo Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa menejimenti kwenye mashirika manne ambayo ni; Shirika la Ndege Tanzania, Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Shirika la Madini la Taifa na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ukaguzi wa Menejimenti unamaanisha uchambuzi na tathmini ya uwezo wa kusimamia shirika husika ili kutathmini ufanisi wa menejimenti, na hasa katika malengo, mkakati na sera ya shirika na kutoa mapendekezo kwa kuzingatia matokeo ya jinsi ya kuboresha hali hiyo. Lengo kuu la ukaguzi wa menejimenti si kupima uwezo wa kiutendaji wa mtu binafsi au watendaji wakuu mmoja mmoja, bali ni kutathmini uwezo wa timu inayosimamia utendaji wa shirika kwa ujumla.

Mbinu za ukaguzi zilizotumika ni pamoja na kuangalia mifumo ya usimamizi wa shirika, utendaji wa shirika kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwa kuzingatia kanuni, sheria na sera, uwajibikaji kwa umma, ufanisi, umadhubuti, uwekevu na mifumo bora ya usimamizi wa taratibu zilizowekwa na zile zilizo zoeleka zenye kuleta ufanisi kwenye shirika “*Best Practices*”. Katika zoezi hili, ushahidi kwa ajili ya ukaguzi ulikusanywa kupitia mapitio ya makabrasha mbali mbali, mahojiano

na maofisa mbali mbali, kwa kufanya utafiti na kwa kuangalia utendaji wa maofisa husika ndani ya shirika. Ukaguzi ulifanywa kwenye maeneo yafuatayo; (i) miundo ya shirika na utawala (ii) usimamizi wa rasilimali watu, (iii) mifumo ya fedha na uhasibu, (iv) mifumo ya bajeti na udhibiti wa matumizi katika shirika, (v) usimamizi wa mifumo ya taarifa na (vi) usimamizi wa mifumo ya mikakati. Pia, kulifanyika ukaguzi wa ufanisi, na kiwango cha kuridhika mteja na wadau wengine kutokana na huduma zitolewazo na shirika. Mapendekezo ya kurekebisha mapungufu yaliyoonekana ni kama ifuatavyo:

5.1 Miundo na Masuala ya Kiutawala

Njia zilizotumika kutathmini miundo na masuala ya kiutawala zilikuwa ni; viwango vya miundo na taratibu, mifumo ya udhibiti ikiwa ni pamoja na ukaguzi na usimamizi wa viashiria hatari.

5.1.1 Mapungufu Yanayohusiana na Miundo ya Kiutawala

Taasisi zote zilizokaguliwa zilikuwa na mapungufu, ya kimuundo kama; Wabunge kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi (STAMICO), miundo dhaifu ya kiutawala kwenye idara ya utafiti na kazi ya ushauri (UDOM). Hata hivyo miundo mbinu ya kiutawala ya Shirika la Ndege la Taifa ndiyo ilionekana kuwa na mapungufu makubwa zaidi. ATCL ni kama kampuni binafsi kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria iliyoianzisha. Na hivyo utawala wake, mfumo wa muundo wa uongozi, na taratibu za kibiashara zina mtazamo wa kampuni binafsi. Hii ni kwa sababu, Sheria ya Makampuni inahitaji makampuni binafsi kuwa na kiwango cha chini cha wanahisa wawili. Kuwa na kampuni iliyosajiliwa kwa hisa moja ni kinyume cha sheria. Lakini ukweli ni kwamba ATCL inamilikiwa na Serikali ya Tanzania, kwa hivyo, ni chombo cha umma.

Tatizo jingine kubwa lililokuwa likiikabili shirika la ATCL lilikuwa ni kuendesha shuguli zake bila Bodi ya Wakurugenzi ambayo ingekuwa ikiangalia shuguli zake na kutoa maamuzi ya msingi. Kipindi cha Bodi iliyopita kiliishia mwezi Machi, 2010 na Bodi nyingine haikuundwa mpaka Agosti, 2010 ambapo serikali iliiongezea muda Bodi ya zamani hadi tarehe 31 Machi, 2011. Kwa hiyo tangu mwezi Aprili, 2011 mpaka muda wa kuandika hii ripoti Machi 2012, ATCL haina Bodi ya Wakurugenzi.

Zaidi ya hayo, shirika halina mfumo wa kibiashara wa kutambua viashiria hatari, kinachofanyika kwa sasa ni kusimamia viashiria hatari vya kiutendeshaji kwa lengo la kutimiza matakwa ya Mamlaka ya Anga ya Taifa, na IOSA. Hakuna ushahidi wa namna ATCL inavyosimamia viashiria hatari vinavyohusiana na ugaidi, kimkakati, na kifedha. Mwaka 2007, mwekezaji kutoka Kampuni ya China ya Sonangol International Holdings Limited alisaini mkataba wa makubaliano na ATCL wa kununua asilimia 49 ya hisa za ATCL. Hata hivyo, hakuna dalili za mwekezaji huyo kulipia hisa hizo hadi sasa. Hivyo basi, tangu Juni, 2011, serikali ya Tanzania iliendelea kuifadhili ATCL wakati mwekezaji mwingine akiendelea kutafutwa.

5.1.2 Mapungufu ya Kiutawala

Taasisi zote zilizokaguliwa zinakabiliwa na matatizo yanayohusiana na utawala. Mapungufu makubwa zaidi yanahusiana na kukosekana kwa mifumo ya udhibiti, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na kamati za kaguzi na miongozo ya kamati hizo (ATCL na STAMICO). Hata hivyo, ATCL inakabiliwa na matatizo makubwa zaidi ya kiutawala ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

(a) Serikali kutoa maamuzi ya kiutendaji ya ATCL bila kuihusisha bodi ya wakurugenzi ya ATCL. Hili ni tatizo kubwa, kwa mfano maamuzi ya kununua ndege mbili

“Dash8-400 Series” ambazo kwa sasa zinatumiwa na ATCL yalifanywa kati ya serikali na M/s China Sonangol Internal Holding Limited (CSIL). Serikali ndiyo iliyo ingia mkataba wa makubaliano (MoU) na CSIL na Baraza la Mawaziri likapitisha uamuzi huo mwaka 2008 kwa kumkaribisha CSIL kama mwekezaji pekee wa ATCL. Ilibainika kuwa, mwekezaji huyo alikuwa anunue ndege tano mpya aina ya Dash 8 Q-400 series, lakini aliishia kununua ndege mbili tena zilizo kuwa zimetumika. Nilijulishwa na menejimenti ya ATCL kuwa uamuzi wa kuingia mkataba na ununuzi ndege hizo haukuihusisha Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Shirika la Ndege Tanzania. Uamuzi huu ulifahamika kwa menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi pale ATCL ilipotakiwa kutoa dola za Kimarekani laki tano (5) kama ada ya kuonyesha nia halisi, lakini Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti hazikuwa sehemu ya mazungumzo.

(b) Mkaguzi wa ndani wa shirika alikuwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Galileo, kampuni tanzu ya ATCL na pia ni mkuu wa kitengo cha mipango cha Shirika. Hii ni kinyume na kanuni za utawala bora za uendeshaji.

(c) Menejimenti ya ATCL kushindwa kurekebisha tofauti kwenye hesabu na kupelekea kuchelewa kukamilisha maandalizi ya taarifa za fedha za miaka inayoishia Disemba 2007, 2008, 2009, na 2010.

5.2.0 Usimamizi wa Mifumo ya Kimikakati

Usimamizi wa mifumo ya kimikakati ni uendeshaji wa shughuli zinazoendelea na zinazohusiana. Utaratibu huu ni pamoja na kupanga mikakati, utekelezaji wa mipango ya kiutendaji, na tathmini ya utendaji. Katika kutekeleza ukaguzi huu, taratibu zifuatazo zilifanyika: (i) kupitia upya mfumo wa sera kwa ajili ya usimamizi wa mkakati; (ii) kupitia upya ubora wa mpango

mkakati wa sasa na, (iii) kupitia upya mipango ya utekelezaji. Taasisi tatu ambazo ni UDOM, ATCL na STAMICO zilionekana kuwa na nyaraka pungufu.

5.2.1 Ubora wa Mpango Mkakati

Ili mpango uwe mzuri na unaotekelezeka, ushiriki mpana na umiliki wa mchakato wa kupanga mikakati ni muhimu sana. Taasisi zote nne zilizokaguliwa zilishindwa katika eneo hili. Mpango mzuri kwa kawaida huwa na maeneo makubwa manne ambayo ni: (i) uchambuzi wa hali halisi, (ii) mipango inayobainisha dira, dhima, misingi ya maadili ya shirika na maeneo muhimu (KRAs), malengo ya mkakati na malengo ya utoaji wa huduma (iii) Utekelezaji wa Mipango (v) Ufuatiliaji na Tathmini ya mipango mikakati. Kwa viwango tofauti, taasisi zote nne zilizokaguliwa zina matatizo katika eneo hili.

ATCL inafanya vibaya zaidi katika ubora wa mpango mkakati na mapungufu yake ni pamoja na yafuatayo: (i) Mpango wake wa kibiashara wa kipindi cha 2008-2013 si mzuri, una jumla ya malengo 11 ambayo hayajitoshelezi na si ya kina. (ii) malengo hayo hayapimiki, hayatekelezeki, si halisi na hayaendani na wakati (SMART) na (iii) dira ya shirika haikupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi.

5.3. Usimamizi wa Rasilimali Watu

Mapitio ya Usimamizi wa mifumo ya rasilimali watu ilifanyika kwenye maeneo yafuatayo: (i) mipangilio ya usimamizi wa rasilimali watu, (ii) usimamizi wa Sera za Rasilimali watu, (iii) mikakati na mipango inayohusiana na rasilimali watu, (iv) kuajiri na kuachisha kazi, (v) mafunzo na maendeleo, (vi) tathmini ya utendaji, na (vii) motisha kwa watumishi na mazingira ya kazi. Mapungufu na mapendekezo yake yako katika sura ya nane (8) ya ripoti hii inayohusiana na usimamizi wa rasilimali watu.

5.4. Mifumo ya Kiuhasibu

Mifumo ya kiuhasibu ni utaratibu uliopangwa, uwe wa kompyuta au usiwe wa kompyuta, njia, na miongozo ya kiuhasibu yenye mfumo na udhibiti imara wa kukusanya, kurekodi, kuainisha, kuchambua, kufupisha, kutafsiri, na kuweka kumbukumbu za fedha kwa usahihi na kwa wakati kwa ajili ya maamuzi ya uongozi. Sifa muhimu ya mifumo madhubuti ya uhasibu ni pamoja na yafuatayo; kupunguza makosa, kuboresha usahihi na mwendelezo wa kumbukumbu za fedha, kuzingatia sheria na kanuni za miongozo ya kusimamia maandalizi ya kumbukumbu za kifedha na kuzifanya taarifa zake kukubalika na watumiaji, iwawezeshe viongozi kufanya maamuzi sahihi yanayohusiana na kimikakati, kuongeza uwezo wa uongozi wa kutambua na kuibua fursa mpya za kuongeza mapato kwa njia ya taarifa za kina na uchambuzi mahili, na kusaidia makampuni kujiepusha na viashiria hatari na adhabu zinazohusishwa na kutofuata sheria na miongozo ya kutayarisha na kuripoti taarifa za fedha. Mapungufu makubwa yaliyojitokeza ni; (i) kuongezeka kwa idadi ya hoja za ukaguzi na hoja zisizo na majibu (UDOM & TCRA), (ii) kiwango cha juu cha hoja zinazohusiana na Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari, na (iii) udhibiti kwenye manunuzi (UDOM), na (iv) kutokuwepo miongozo ya masuala ya kiuhasibu (STAMICO). Mfumo huu unakabiliwa na makosa ya kiutendaji na mapungufu mengine hasa katika udhibiti wa mifumo ya ndani ya shirika ambayo udhibiti wake unaweza kuboreshwa. Hoja zenye uzito zaidi zilikuwa za ATCL ambapo mifumo ya kompyuta ya kiuhasibu haitoi taarifa sahihi. Kwa mfano, urari kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2009 na ule wa tarehe 30 Juni, 2008 haukuweza kulingana. Urari kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2008 ulikuwa na tofauti ya Shilingi bilioni 14.8 wakati ule wa tarehe 30 Juni, 2009 ulikuwa na tofauti ya Shilingi bilioni 28.

5.5. Mifumo ya Kusimamia Bajeti

Bajeti ni mpango uliowekwa katika hesabu na, kwa kawaida huwa katika hali ya kifedha, kwa kipindi maalum, kwa kawaida mwaka mmoja hadi mitano. Katika shirika la kibiashara, bajeti huwakilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi husika. Mchakato wa kudhibiti bajeti ni pamoja na; maandalizi ya bajeti yenyewe, kuendelea kulinganisha utendaji halisi na bajeti na marekebisho ya bajeti kwa mtizamo wa mabadiliko mbalimbali. Mapungufu makubwa yalikuwa ni tofauti kubwa kwenye bajeti ya mapato na matumizi, na hii ni dalili kwamba baadhi ya bajeti zilikuwa na mapungufu (UDOM & TCRA). Mapungufu makubwa zaidi yalikuwa ATCL, ukweli ni kwamba ATCL ilikuwa inaendesha shughuli zake bila bajeti. Hii inamaanisha kuwa mfumo wa kutumia bajeti kama chombo cha kudhibiti haukuwepo.

5.6 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa

Mfumo wa usimamizi wa taarifa (MIS) ni mfumo ambao hutoa taarifa zinazohitajika kusimamia mashirika kwa ufanisi. Usimamizi wa mifumo ya taarifa huhusisha rasilimali tatu za msingi: teknolojia, habari, na watu. Mapungufu makubwa yaliyotokana na tathmini ya usimamizi wa mifumo ya taarifa yalikuwa ni pamoja na; (i) kukosekana kwa mfumo wa taarifa ulio wazi (ATCL & STAMICO), kukosekana kwa Sera ya Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari, (Taasisi zote); na ukosefu wa usimamizi wa mifumo ya taarifa iliyounganishwa pamoja (taasisi zote).

5.7 Utafiti Juu ya Wateja Kuridhika

Mapitio ya kiwango cha kuridhika wateja yalizingatia vigezo vifuatavyo; uongozi, mazoea ya usimamizi kwa jumla, usimamizi wa rasilimali watu, huduma za fedha, mazingira ya kazi na maoni ya ujumla. Taasisi mbili ambazo ni TCRA na UDOM zilifanya vizuri kwenye ubora wa uongozi wa juu na uongozi wa jumla, usimamizi wa

rasilimali watu, huduma za fedha, mazingira ya kazi na maoni ya ujumla, ingawa kuna maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa zaidi. Hata hivyo, ATCL inafanya vibaya kwenye maeneo yote.

TCRA na UDOM zinafanya vizuri kwenye kuhudumia wateja kwa ujumla ingawa maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi; Ukaguzi wa wateja na bei ya huduma (TCRA), Mfumo wa ushauri kwa wanafunzi, (UDOM) vyama vya wafanyakazi, huduma za chakula na usafiri, huduma za matibabu, huduma za ushauri nasaha na ofisi ya fedha (Cash Office), mahusiano kati ya Wakurugenzi wa kozi na wanafunzi, utoaji wa masomo wa wahadhiri, na usuluhisho wa malalamiko ya wanafunzi, mifumo ya kutunza na kusimamia kero yalionekana ni mapungufu yanayohitaji marekebisho katika Chuo Kikuu Dodoma (UDOM).

Mapungufu machache yaliyoonyeshwa hapo juu kuhusiana na menejimenti ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo, yachukuliwe na Mashirika mengine vile vile kama kielelezo cha kuyafanyia marekesho kwa sababu ni mapungufu ambayo yanaweza kuwa kwenye Mashirika mengine Umma.

SURA YA SITA

UZINGATIAJI WA SHERIA ZA MANUNUZI NA MENEJIMENTI YA MIKATABA

6.0 Utangulizi

Tanzania ilifanya mabadiliko makubwa katika manunuzi na hivyo kupelekea kuanzishwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Maamuzi haya yalikuwa ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba manunuzi katika Wizara, Serikali za Mitaa na Idara zote za Serikali yanafuata taratibu zinazokubalika. Kifungu Na.44 (2) cha Sheria ya Manunuzi kinamtaka Mkaguzi wa taasisi yeyote ya umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama taratibu zote za manunuzi zimefuatwa na Taasisi husika.

Vilevile, kanuni ya 31 ya Sheria za Manunuzi ya Umma (Bidhaa, Ujenzi, Huduma zisizo za kiushauri na uuzaji wa mali za Umma kwa zabuni), inamtaka Mkaguzi wa Hesabu za taasisi ya Umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama manunuzi yaliyofanyika yalifuata taratibu za kuitisha zabuni na katika ushindani na pia kama ununuzi au uuzaji uliidhinishwa kwanza na bodi ya zabuni.

Kwa kuzingatia mamlaka niliyopewa katika vifungu vya sheria vilivyoainishwa hapo juu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu imekagua taratibu za manunuzi ya mashirika 125 katika ukaguzi wake wa kawaida kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hivyo, sura hii inajumuisha matokeo na mapendekezo ya kaguzi zilizofanywa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi husika. Kwa upande mwingine, Mamlaka ya Uthibiti wa Manunuzi katika Serikali (PPRA), ilifanya ukaguzi wa manunuzi katika Mashirika 51 ambayo matokeo yake yamejumuishwa kwenye kurasa za sura hii.

Sura hii pia, inatoa majumuisho ya taarifa za ukaguzi na utekelezaji wa mikataba iliyoonekana kuwa na mapungufu na hivyo kuonekana kuwa muhimu kutolewa taarifa yake katika ripoti hii. Ukaguzi wa mikataba ulifanyika sambamba na ukaguzi wa kawaida wa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba 2010, 31 Disemba 2010 na 30 Juni 2011. Matokeo ya zoezi la ukaguzi wa mikataba kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo yameainishwa katika sehemu ya pili ya sura hii.

6.1 Usimamizi wa Manunuzi

Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya umma ya Mwaka 2004, neno manunuzi linamaanisha kununua, kukodisha, au vinginevyo kupata bidhaa, ujenzi au huduma inayofanywa na taasisi kwa kutumia fedha za umma, kwa niaba ya Wizara au Idara ya Serikali au Shirika la Umma na ikijumuisha na kazi zote zinazohusiana na kupatikana kwa bidhaa au huduma ikiwa ni pamoja na kuainisha mahitaji, kuteua na kutangaza zabuni na kutoa mikataba. Yafuatayo ni mambo ambayo yalionekana kuwa na kasoro kwenye ukaguzi wa usimamizi wa manunuzi.

6.1.1 Manunuzi ya Bidhaa na Huduma Bila Kufuata Sheria za Manunuzi

Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 inahitaji manunuzi yote ya umma na mauzo ya mali za umma kufanywa kwa mujibu wa kanuni za msingi zilizoainishwa kwenye sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka, 2005. Imeandikwa katika Sheria kwamba, manunuzi yote na uzaji wa mali za umma ufanyike kwa kufuata ushindani, kwa lengo la kuongeza ufanisi, uwazi na thamani ya fedha. Kwa mfano katika Baraza la Kiswahili Tanzania, ukaguzi ulibaini kuwa Baraza lilinunua seti sita za viti kutoka kampuni ya “Quality Furniture and General Appliance” kwa kutumia ankara kifani moja kinyume na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004

ambayo inahitaji angalau hati ya mauzo (Quotation) tatu kupatikana kabla ya muuzaji wa bidhaa kuchaguliwa na manunuzi kufanyika.

Katika Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) iliripotiwa kuwa Baraza lilionua tiketi za ndege zenye thamani ya Shilingi milioni 25.7 kutoka kampuni ya Travel Antelope and Tours bila ya kutumia zabuni au mfumo wa GPSA. Wakati huo huo, katika Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) manunuzi ya vitu mbali mbali yanayokadiriwa kufikia Shilingi milioni 683.3 yaliripotiwa kuwa yalifanyika bila kuzingatia kifungu Na.58 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Kifungu hiki kinazitaka Taasisi za Umma kutumia njia ya ushindani katika ununuzi wa bidhaa na huduma.

6.1.2 Manunuzi Yaliyofanywa Nje ya Mpango Ulioidhinishwa na Nje ya Bajeti

Kwa lengo la kupata thamani ya fedha na kupunguza gharama za manunuzi, Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka, 2004 na Kanuni zake za mwaka, 2005 inahitaji vyombo vya Umma kupanga manunuzi yake katika hali inayoleta mantiki

Mapitio ya mipango ya manunuzi ya Taasisi za Umma katika mwaka 2010/2011 yalibaini kuwa, baadhi ya manunuzi yalifanywa nje ya mpango wa manunuzi ulioidhinishwa kinyume na kifungu Na.45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni ya 45 (5) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005. Baadhi ya mapungufu yaliyoanishwa ni pamoja na manunuzi ya bidhaa na huduma mbali mbali kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.9 katika Chuo Kikuu Mzumbe. Katika Mamlaka ya Maji safi na Maji taka ya Mjini Dodoma iliripotiwa kwamba jumla ya bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.5 zilionuliwa nje ya mpango wa manunuzi uliopitishwa. Dosari kama hii iliripotiwa pia katika Bodi ya Utalii Tanzania ambapo vifaa vya kompyuta vyenye thamani ya Shilingi milioni

30.8 vilinunuliwa nje ya mpango wa manunuzi ulioidhinishwa na Bodi.

Ukaguzi wa mpango wa manunuzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mjini Dodoma kwa mwaka 2010/2011 ulibaini kuwa Mamlaka ilifanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi milioni 33.8 nje ya bajeti iliyopitishwa. Manunuzi haya ambayo yalikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa maji katika Chuo Kikuu cha Dodoma ni asilimia 84 (84%) ya manunuzi yote yaliyofanywa na Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2010/2011

6.1.3 Manunuzi ya Huduma Bila Mkataba Halali

Tatizo la kutokuwepo kwa mikataba halali kati ya Taasisi za Umma na watoa huduma na wauzaji bidhaa limeendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Baadhi ya Taasisi za Umma zilinunua bidhaa na huduma mbalimbali bila ya kuwa na mikataba ya kisheria kama inavyoelekezwa katika sheria ya manunuzi ya umma.

Ukaguzi wa Mikataba katika Baraza la Uwezesaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ulibaini Baraza kununua huduma ya usafi kwa gharama ya Shilingi milioni 10.6 kutoka kwa kampuni ya Ledso Ltd bila kuwa na mkataba halali. Dosari kama hii ilijitokeza pia, katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ambapo Mamlaka ilifanya biashara na wamiliki wa hoteli za kitalii na watoa huduma mbalimbali bila ya mkataba. Katika Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) mapungufu kama haya yaliripotiwa ambapo manunuzi ya mafuta ya magari yalikuwa yakifanyika bila ya mkataba uliosainiwa kati ya watoa huduma na Baraza.

6.1.4 Upungufu wa Watumishi na Kutoanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi

Ni matakwa ya Sheria ya Manunuzi kwamba, kila Taasisi ya Umma iwe na kitengo cha usimamizi wa manunuzi (PMU) chenye watumishi wa kutosha na wenye sifa sahihi. Kwa mujibu wa kifungu Na.34 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kitengo cha manunuzi (PMU) kinapaswa kuwa na wataalam wa manunuzi, wataalam wengine wa kiufundi pamoja na wafanyakazi muhimu wa kusaidia shughuli za utawala. Hata hivyo, katika kipindi cha taarifa hii baadhi ya Mamlaka za Umma ziliripotiwa kuwa na watumishi pungufu tofauti na idadi iliyoko kwenye ikama zao. Hali hii ilionekana katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Shinyanga Kahama, Bodi ya Kahawa Tanzania na Bodi ya Leseni Tanzania.

6.1.5 Taarifa za Mikataba Kutowasilishwa PPRA

Kanuni ya 21 (1) ya tangazo la Serikali Na. 97 (2005) inahitaji katibu wa bodi ya zabuni na vyombo vingine vya Umma, kuwasilisha taarifa za mikataba yote iliyofanyika kwenye Mamlaka ya Udhubiti na Ununuzi wa Umma (PPRA) wakieleza wazi nani ambaye amepewa mkataba, kiasi cha fedha kwa kila mkataba na tarehe ya mkataba. Aidha, kanuni ya 21 (2) na (3) inataka pawepo na uwazi katika zoezi zima la uingiaji wa mikataba sahihi ya manunuzi. Kwa kuzingatia vifungu vya sheria vilivyotajwa hapo juu, ukaguzi wa taratibu za manunuzi katika Mamlaka za Umma ulibaini kwamba baadhi yao hawakuwasilisha taarifa za mikataba ya manunuzi waliyoingia na wakandarasi na wazabuni mbalimbali kwa Mamlaka ya Udhubiti na Ununuzi wa Umma (PPRA).

6.1.6 Utendaji Huru wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi

Chini ya masharti ya Sehemu ya 38 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, Mtendaji Mkuu, Bodi ya Zabuni, Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi,

Idara ya mtumiaji na Kamati ya Tathmini, wanapaswa kutenda kazi zao kwa uhuru bila kuingiliana. Wakati wa ukaguzi wa taratibu za ununuzi katika Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) ilibainika kuwa shughuli za manunuzi ziko chini ya idara ya utawala. Utaratibu huu ni kinyume na matakwa ya sheria ya manunuzi inayotaka uwepo wa uhuru katika shughuli za ununuzi.

6.1.7 Uidhinishwaji wa Zabuni Zaidi ya Kiwango Kinachokubalika Kisheria

Ukaguzi wa mikataba ya manunuzi kati ya Shirika la Posta na watoa huduma mbalimbali ulibainisha kuwa katika kipindi husika cha taarifa hii, Shirika liliingia mkataba wa kununua jozi 196 za “Electronic Tax Register (ETR)” na jozi 142 za “Electronic Signature Devices (ESD)” kwa gharama ya Shilingi milioni 787.9. kwa kutumia njia ya vikwazo zabuni (restricted tendering method). Kwa mujibu wa jedwali la 2 la Kanuni za Ununuzi wa Umma mwaka, 2005 manunuzi ya bidhaa chini ya njia ya vikwazo zabuni ni muhimu yawe ya kiwango kisichozidi Shilingi milioni 400. Kwa kuzingatia sheria tajwa Shirika lilifanya kosa kuingia mkataba wa manunuzi kwa njia ya vikwazo zabuni iliyozidi kiwango kilichoidhinishwa bila hata ushauri kutoka Mamlaka ya Udhhibiti na Ununuzi wa Umma (PPRA).

6.1.8 Ukaguzi wa Manunuzi Katika Mashirika 51 Uliofanywa na Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)

Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004, inaipa uwezo Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) kufanya ukaguzi wa manunuzi yaliyofanyika na kutoa taarifa baada ya ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi wa manunuzi ya mwaka, 2010/2011 yalionyesha kiwango cha utekelezaji wa sheria kwa kufuata viashiria kumi na tatu vilivyowekwa na Mamlaka ni cha wastani wa asilimia 63 ukilinganisha na asilimia 75 kwa mwaka uliotangulia. Kwa hiyo, wastani wa jumla wa kiwango

cha utekelezaji wa sheria katika mwaka wa fedha 2010/2011 ni wastani wa asilimia 68.

Matokeo haya yanaonyesha maboresho makubwa katika kutekeleza sheria ya manunuzi tangu mwaka wa fedha 2006/2007 Mamlaka ilipofanya ukaguzi wake kwa mara ya kwanza. Kiwango cha utekelezaji kimeongezeka kutoka asilimia 39 katika mwaka wa fedha 2006/2007 hadi asilimia 68 katika mwaka wa fedha 2010/2011 ambapo hii ni chini ya lengo lililoazimiwa la asilimia 80 kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Ufanisi wa Mashirika ya Umma

Wakati wa kipindi cha kuandika taarifa hii, Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) ilifanya ukaguzi katika Mamlaka na Taasisi 51 za Umma. Matokeo ya ukaguzi huu yalionyesha kiwango cha wastani wa asilimia 64 ya utekelezaji wa sheria. Utekelezaji wa sheria kwa wastani ulikuwa chini ya asilimia 50 katika moja ya kiashiria yaani: Matangazo ya mikataba (41%). Hata hivyo utekelezaji wa sheria ulikuwa juu ya wastani (50% na zaidi) katika viashiria vingine kumi na viwili yaani: Uanzishaji na muundo wa Bodi za Zabuni (80%); Uanzishwaji na miundo ya kitengo cha manunuzi (61%); Uhuru wa kuamua juu ya masuala ya manunuzi kati ya Afisa Mtendaji Mkuu (CEO), Bodi za zabuni (TB) na kitengo cha manunuzi (62%); Uandaaji wa mpango wa mwaka wa manunuzi (55%); Utekelezaji wa maidhinisho ya lazima (68%); Matangazo ya fursa za zabuni (80%); Muda wa kuandaa zabuni (80%); na matumizi ya njia sahihi ya manunuzi (79%); matumizi ya nyaraka za viwango vya zabuni kama ilivyoainishwa katika kanuni (67%); Utunzaji wa kumbukumbu (54%); Viwango vya ubora na udhibiti (52%); na Usimamizi wa mikataba (61%). Chini ya vigezo hivi, Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) yalipata alama za juu za utekelezaji wa sheria yaani asilimia 87 wakati Mamlaka

ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Lindi ilipata alama ya chini wastani yaani asilimia 25.

Nashauri kuwa Menejimenti za Mashirika ya Umma ziongeze jitihada za kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi inazingatiwa kikamilifu.

6.2 Usimamizi wa Mikataba

Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, mkataba wa manunuzi unamaanisha leseni, kibali au makubaliano ya aina yoyote yaliyoingiwa na taasisi za umma na wazabuni au mjenzi unaotokana na mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kununua bidhaa, ujenzi au kupata huduma. Mambo yafuatayo yalitokana na ukaguzi wa mikataba kwa kipindi husika.

Kwa mujibu wa sheria ya Manunuzi, Taasisi ya Umma ina wajibu wa kuhakikisha kunakuwepo na usimamizi madhubuti wa mikataba yoyote ya bidhaa, huduma au kazi. Kwa kufanya hivyo Taasisi inapaswa kufuatilia upatikanaji wa haraka wa bidhaa na huduma kwa njia sahihi na kuchukua hatua madhubuti pale ambapo ukiukwaji wa sheria unaonekana kuwa wa wazi. Kwa mujibu wa kifungu Na.121 cha kanuni za sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka, 2005, mapitio ya ukaguzi katika mikataba mbalimbali yalibaini kuwepo kwa mapungufu yafuatayo:-

6.2.1 Kushindwa Kusimamia na Kutekeleza Mikataba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Mapitio ya mkataba wa pango la ofisi katika jengo la Mwl. Nyerere Pension Towers yaliyofanyika kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (Mpangaji) kwa kipindi cha Julai 2010 hadi Juni 2012 umebaini kuwa mkataba huo haukutiwa saina na mpangaji kwa wakati. Kwa mujibu wa mkataba huu mpangaji alitakiwa kulipa kiasi cha Dola za Kimarekani elfu 10.2 kila mwezi ambapo zilishaanza kulipwa kabla hata mkataba haujatiwa saina na pande

husika. Katika hali isiyokuwa ya kawaida uongozi wa Mfuko ulishindwa kutekeleza masharti ya mkataba wa kukusanya kodi ya pango kwa miezi kadhaa na hivyo kusababisha limbikizo la kodi. Hata hivyo ukaguzi ulibaini kwamba mpangaji alikuwa na limbikizo kubwa la deni pamoja na kwamba masharti ya mkataba yanamtaka kulipa kodi miezi mitatu kabla.

6.2.2 Usimamizi Mbaya wa Mkataba wa Ujenzi Katika Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia katika mkataba na kampuni ya AF MULT-Con LTD kujenga nyumba ya makazi ya Msimamizi mkuu wa Bandari ya Tanga kwa gharama ya Shilingi milioni 500. Taratibu za zabuni na maridhiano ya mkataba huo yalihakikiwa na hapakuwa na dosari. Hata hivyo, katika kupitia upya utekelezaji na mafanikio ya mradi huu kwa kuzingatia sheria na masharti ya mkataba, ilibainika udhaifu wa usimamizi na kutotekelezwa kwa masharti ya mkataba huo ambao baadae yalisababisha mradi kushindwa kuendelea licha ya Mkandarasi kulipwa asilimia 20 ya bei ya mkataba yaani Shilingi milioni 100. Ziara ya ukaguzi katika eneo ambapo ujenzi ulikuwa ukifanyika, haukuweza kushuhudia maendeleo yoyote kama vile ujenzi wa jengo husika au hata vifaa vya ujenzi vilivyoweza kuhalalisha malipo ya awali ya Shilingi milioni 100 alizolipwa mkandarasi.

6.2.3 Usitishwaji wa Mkataba Uliosababisha Malipo Batili

Wakati wa ukaguzi wa taarifa ya fedha ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kwa mwaka wa fedha 2010/2011 tulibaini kwamba Mamlaka iliingia katika mkataba wa ujenzi wa ukuta wa uzio katika Bandari ya Mtwara na kampuni ya Chibeshi Contruction, Mkataba huu ambao uligharimu shirika Jumla ya Shilingi milioni 679.8 ulisainiwa tarehe 14 Aprili 2009 na kukubaliana kuwa utakamilika baada ya wiki 26 kuanzia tarehe ya kusaini mkataba.

Hata hivyo, kabla ya Mkandarasi kuanza kazi, Mamlaka iliamua kuvunja mkataba kwa madai kuwa hapakuwa na mgao wa fedha kwa ajili ya shughuli hiyo. Usimamizi na uamuzi wa kuvunja mkataba uliifanya Mamlaka kulipishwa faini ya Shilingi milioni 92.5 na Mkandarasi. Kanuni ya Na. 46 (5) na (6) GN 97 ya mwaka 2005 inaeleza bayana kwamba, gharama za mahitaji ya manunuzi ni lazima zikadiriwe na kulinganishwa na uwezekano wa upatikanaji wa fedha ili kuweka vipaumbele katika manunuzi muhimu. Hili halikuweza kuzingatiwa na Uongozi wa Mamlaka na hivyo kutoa nafasi kwa Mkandarasi kulipwa Tozo ya Shilingi milioni 92.5.

6.2.4 Kutolipwa kwa Tozo ya Fidia za Uvunjifu wa Mikataba

Mapitio yetu ya mkataba kati ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Kampuni ya WIA yamebaini kuwa Mamlaka iliingia katika mkataba wa kubuni, kusimika, na kuwezesha huduma za mtandao kwa ajili ya Bandari Makao Makuu na Bandari nyingine. Kulingana na kandarasi, muunganisho wa mawasiliano kwenye mtandao mmoja kati ya Bandari za Maziwa na Bandari Kuu ulitakiwa kukamilika katikati ya mwezi Julai 2010 na kuanza kutumika Oktoba 30, 2010. Mkataba huu ulikuwa kwa ajili ya kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai 2010 hadi Oktoba 2010. Hata hivyo, mradi haukuweza kukamilika kwa muda wa kipindi cha mkataba hivyo kupelekea Mamlaka kumuongezea Mkandarasi muda hadi Februari, 2011. Licha ya Mkandarasi kuongezwa muda, hakuweza kukamilisha kazi aliyopewa. Kwa mapungufu haya, ilipaswa Mkandarasi ailipe Mamlaka fidia ya ucheleweshaji ya asilimia 10 ya bei ya mkataba Dola za Kimarekani elfu 95.3 fedha ambazo hazikulipwa kwa sababu ambazo hazikuwekwa bayana.

6.2.5 Ucheleweshwaji wa Kandarasi za Kampuni ya CATS Tanzania LTD Kinyume na Makubaliano ya Mkataba

Katika kipindi cha ukaguzi wa hesabu za Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) ilibainika kuwa Shirika lilingia katika mkataba na kampuni ya CATS Tanzania Limited unaohusiana na matengenezo ya kawaida, na ufungaji wa vifaa vya mawasiliano na vifaa vingine katika mkataba wa jumla ya dola za Kimarekani milioni 1. Ada kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya LAN na gharama za kuunganisha ilikuwa Shilingi milioni 64.7. Mkataba ulisainiwa tarehe 27 Mei 2009 na ulikuwa unatarajiwa kukamilika baada ya wiki 5 yaani Novemba 27, 2009. Hata hivyo, mkandarasi hakufanikiwa kumaliza kazi hadi Septemba 3, 2010. Ucheleweshaji huu ni sawa na muda wa siku 280 sawa na wiki 40.

Aya ya 3.5 ya mkataba uliosainiwa kati ya TANAPA na Mkandarasi CATS Tanzania Limited umeweka wazi kwamba ucheleweshwaji wowote wa ufanisi wa mkataba utatozwa asilimia 0.1 hadi 0.15 ya bei ya mkataba kwa idadi ya siku ambazo mkataba umechelwa kukamilika.

Zaidi ya hayo, kanuni Na.117 ya Sheria ya Manunuzi ya umma inahitaji kwamba, mkataba au makubaliano ya maandishi yakishasainiwa hayawezi kubadilishwa, ila wakati mabadiliko ni muhimu kwa faida ya mnunuzi au mabadiliko hayatamweka mnunuzi katika nafasi ya hasara na pale tu wakati Bodi ya Zabuni iliyopitisha mkataba wa awali itakaporuhusu mabadiliko hayo. Licha ya Mkandarasi kutolipa fidia ya ucheleweshaji kazi, hakuna ushahidi kwamba bodi ya zabuni ilipitisha ongezeko la muda alilopewa Mkandarasi la siku 280.

6.2.6 Udhaifu wa Usimamizi wa Mikataba katika Bandari ya Dar es Salaam

Mamlaka ya Bandari Tanzania iliingia katika mkataba na kampuni ya Singapore PTE Ltd wa kufunga na

kusambaza “Redio Data” katika vituo vya Bandari mwezi Februari 2010 kwa gharama ya dola za Kimarekani Laki tatu thelathini na tisa (339) Mara baada ya Mamlaka kupokea “Redio Data” mfululizo wa matukio uliojitokeza. Kama ifuatavyo:- Kwanza, Mamlaka ilibaini kwamba redio data zilionunuliwa zisingeweza kufanya kazi bila ya kupata “access point” hivyo ilisababisha Mamlaka kusaini mkataba mwingine wa kununua “access point 68” kutoka kwa M/s Singapore PTE Ltd mwezi Juni 21, 2010 kwa gharama ya dola za Kimarekani Laki nne bila ushindani. Baada ya kununua “access point” ilibainika pia kwamba hazitaweza kufanya kazi bila ya kuwekwa juu ya mnara maalum kwa hiyo Mamlaka ikaingia mkataba mwingine na CATS M/s (T) LTD ya Septemba 17, 2010 wa kununua mnara kwa gharama ya jumla ya dola za Kimarekani Laki moja thelathini na tatu (133) kwa mara nyingine bila ushindani. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa hata baada ya ufungaji wa “access point” “Radio data terminal” vituoni hazikuweza kufanya kazi kama ilivyotolewa kwa kuwa zilihita kuwa “fiber optic”. Hili pia liliilazimu Mamlaka kuingia katika mkataba mwingine wa kununua “fiber optic”. kutoka kwa kampuni ya EMEC mara nyingine tena bila ushindani kwa gharama ya dola za Kimarekani elfu laki tano hamsini na nne (554) Jumla ya gharama za ziada zilizotumika kwenye manunuzi haya zilikuwa dola za Marekani milioni 1. Hata hivyo mradi huu haukuweza kukamilika hadi wakati wa kuhitimisha ukaguzi kwa kuwa vifaa vyote vinavyohitajika vilikuwa havijaletwa na kuunganishwa.

Chini ya Kanuni Na. 46 (5) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005 imetajwa kuwa Taasisi ya Umma kabla ya kununua mahitaji yake ni lazima ifuate mpango wa manunuzi uliopitishwa na kutengewa fedha kwenye bajeti.

6.3 Changamoto zinazoikabili Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) Katika Kutekeleza Majukumu Yake

Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ni chombo muhimu kinachohusika na udhibiti wa fedha za katika manunuzi yanayofanywa na Serikali. Pamoja na umuhimu wa chombo hiki zipo changamoto mbalimbali ambazo zinazuia utekelezaji wa majukumu yake katika kiwango kinachotakikawa. Mapitio ya ripoti ya mwaka 2010/2011 ya Mamlaka hii yanaonyesha kuwa Mamlaka iliweza kukagua na kutoa ripoti ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo hamsini na moja (51) tu kati ya mashirika mia moja sabini na sita (176) yaliyopaswa kukaguliwa. Hii ni sawa na asilimia 28.9 ya malengo ya ukaguzi wa manunuzi ya umma yaliyokusudiwa kufanywa na Mamlaka. Mapungufu haya ya kiutendaji yalisababishwa kwa kiasi kikubwa na ukosefu wa fedha za kutosha kutoka Serikalini kama ilivyoainishwa katika bajeti ya Mamlaka.

Katika mapitio ya ukaguzi uliofanywa na Mamlaka kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 nilibaini kwamba Mamlaka ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni 4.8 kutoka Serikalini ikiwa ni asilimia 32 ya bajeti. Mapungufu haya yalikwamisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka katika kudhibiti upotevu wa fedha za Umma kwenye manunuzi yasiyofuata taratibu. Katika kukabiliana na hali hii ninaishauri Serikali kutenga na kutoa fedha za kutosha kwa Mamlaka hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Napenda kuripoti pia kwamba ili taasisi yeyote iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kufikia malengo iliyojiwekea ni lazima iwe na

rasilimali watu ya kutosha. Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi na Umma (PPRA) inakabiliwa na tatizo kubwa la rasilimali watu. Kufuatana na muundo wa Mamlaka hii kunahitajika jumla ya wafanyakazi 142. Kwa sasa Mamlaka ina jumla ya wafanyakazi 48 tu kiasi ambacho ni pungufu ya mahitaji halisi. Mipango ya ajira ya kujaza nafasi zilizo wazi ipo ila Mamlaka inashindwa kuajiri kutokana na kutokuwa na kibali toka mamlaka husika (Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma). Kutokana na hali hii natoa rai kwa Serikali kutoa kipaumbele kwa Mamlaka na Taasisi muhimu hapa nchini zipatiwe vibali vya ajira ili ziweze kuhudumia jamii.

Hali kadhalika ili kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kutekeleza majukumu yake ipasavyo Serikali inapaswa kuhakikisha juhudi za Mamlaka za kuwa na jengo lake la ofisi. Kwa sasa Mamlaka inalipa kodi ya pango kwa ajili ya ofisi ya kiasi cha Shilingi milioni 280 kwa mwaka fedha ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za kimamendeleo kama Mamlaka ingekuwa na jengo lake la ofisi. Hata hivyo ningependa kuishukuru Serikali kwa jitihada ilizoonyesha kwa kuipatia Mamlaka hii jengo la ghorofa tatu la iliyokuwa mali ya NAFCO-Kurasini Dar es Salaam. Natoa tena rai kwa Serikali ili ione umuhimu wa kuipatia Mamlaka fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati wa jengo tajwa hapo juu.

Mwisho napenda kuishauri Mamlaka ione uwezekano wa kuanzisha ofisi za kanda pia katika ngazi za Mikoa nchini. Hii itarahisisha utendaji kazi na ufanisi katika kudhibiti upotevu wa fedha za Umma katika manunuzi yasiyofuata taratibu.

SURA YA SABA

USIMAMIZI WA RASILIMALI

7.0 Utangulizi

Usimamizi wa rasilimali unahusu mfumo wa usimamizi na uangalizi yakinifu katika mchakato mzima wa utaratibu wa uendeshaji, udumishaji na uboreshaji rasilimali za taasisi, mashirika au vikundi. Kihisibu rasilimali ni mali zinazomilikiwa na Taasisi au Shirika kwa ajili ya matumizi yake ya kila siku. Rasilimali zinajumuisha mali zisizohamishika, mitambo, vifaa mbalimbali, uwekezaji, fedha taslimu, madeni yanayodaiwa, akiba ya vifaa, mifumo ya ndani ya kompyuta, tovuti na malipo tangulizi.

Sura hii inajumuisha muhtasari wa mambo muhimu yaliyojitokeza katika ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo na kuchukuliwa umuhimu kutokana na changamoto kubwa zinazoyakabili Mashirika mengi ya Umma katika ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali. Pamoja na changamoto hizo, hapa ni eneo ambalo kuna uwezekano mkubwa wa wafanyakazi ambao sio waaminifu kufanya ubadhirifu wa mali za umma. Matokeo ya kaguzi katika usimamizi wa rasilimali katika Mashirika ya Umma ni kama ifuatavyo:-

7.1 Wadaiwa wa Muda Mrefu Shilingi Bilioni 70.9

Madeni ya kibiashara ni fedha zinazodaiwa na Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo kwa wateja na hurekodiwa kama mali kwenye taarifa ya biashara ya hali ya kifedha. Madai ni sehemu ya mapato ya biashara, pamoja na mtiririko wa fedha na faida. Kwa mujibu wa uchambuzi wa kifedha, wastani wa kipindi cha ukusanyaji wa madeni kinachokubalika ni ndani au chini ya siku tisini (90) ili kuepuka kushikilia rasilimali za shirika mikononi mwa watu. Hata hivyo ukaguzi

ulibaini katika taarifa ya fedha ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo kuwepo madeni ya kipindi kirefu (zaidi ya miezi 12). Katika mtazamo huu, Mamlaka na Mashirika ya Umma yanayodai madeni ya muda mrefu yanaweza kupata hasara na kushindwa kuendesha shughuli zake za kila siku kutokana na wadaiwa kushindwa kulipa madeni yao au kushuka kwa thamani ya fedha zilizo mikononi mwa wadaiwa. Kwa mfano, jedwali hapa chini linaonyesha baadhi ya mashirika ambayo hayajalipwa kwa kipindi cha muda mrefu na wadaiwa. Mchanganuo katika jedwali unaonyesha viwango vya madeni dhidi ya mauzo ya mwaka:

Jedwali Na. 6: Wadaiwa wa Zaidi ya Mwaka Mmoja

Na:	Shirika	Wadaiwa (Tshs.)	% ya Mauzo
1	TCRA	19,928,696,984	
2	TPDC	12,543,903,262	6
3	Mamlaka ya Maji Kahama Shinyanga	882,215,062	29
4	Mamlaka ya Maji Tabora	1,026,997,395	62
5	Bodi ya Korosho	544,032,000	28
6	Mamlaka ya Maji Tanga	767,640,199	20
7	Bohari kuu ya Madawa ya Serikali	35,198,035,311	19

7.2 Ukosefu wa Hati za Miliki za Mali

Umiliki wa mali zisizohamishika unamaanisha umiliki wa kisheria unaohitishwa na hati miliki au nyaraka nyingine zinazoweza kuthitishwa kisheria. Kinyume cha hapo shirika au taasisi haina uhalali wa kisheria juu ya mali inayomiliki. Uhakiki wa mitambo, vifaa na majengo yanayomilikiwa na Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo ulibainisha kuwa nyingi ya mali hizi hazikuwa na uthibitisho wa umiliki wa kisheria. Kwa mfano mashirika kama TPDC halina hati ya sehemu ya

ghorofa "A" ya Jengo Benjamin William Mkaapa inayomiliki na inayotumika kama ofisi; Pia mapungufu hayo yameripotwa katika Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji Mkuu Dodoma (CDA), Bodi ya Korosho ni miongoni mwa Mamlaka nyingi za kusambaza maji safi na maji taka mijini ambazo hazina hati miliki.

7.3 Tathimini ya Mali na Mitambo

Kulingana na miongozo ya kimataifa ya kihasibu Sura ya 16 Kifungu cha 31 kinasema, baada ya utambuzi wa mali na mitambo ambayo thamani yake inaweza kuainishwa kwa uhakika, mali na mitambo hiyo itakua ikirekodiwa kwa thamani halisi. Kifungu cha 34 kinahitaji tathimini iwe inafanyika na mtaalam wa uhakiki mali kila baada ya miaka mitatu au mitano. Kwa mtazamo huo, Sera ya kihasibu ya mashirika ya umma inasema vitabu vya mahesabu huandaliwa kwa kulingana na gharama za awali na kurekebisha kwa kufanya tathimini ili kuonyesha thamani halisi. Hata hivyo uhakiki uliofanywa wakati wa kaguzi za mashirika mbalimbali ulibaini kwamba uthamini wa mali na mitambo haujawahi kufanywa kwenye mashirika mengi ya usambazaji wa maji safi na maji taka mijini. Pia kwa mashirika mengine utathimini haukufanywa kwa wakati kama muongozo wa kimataifa wa kihasibu unavyotaka.

7.4 Mkopo wa Muda Mrefu kwa Shirika la Ndege Tanzania

Mkopo ni makubaliano ya utoaji wa fedha kwa kipindi fulani kati ya mkopeshaji na mkopaji ambapo mdaiwa ana wajibu wa kulipa kiasi sawa cha fedha kwa mkopeshaji kulingana na makubaliano. Kwa kawaida, fedha hurejeshwa kwa awamu, au marejesho ya kiasi kwa kila baada ya kipindi fulani. Hata hivyo, katika ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo ilibaini kuwa TCRA ilitoa mkopo maalum wa jumla ya Shilingi bilioni 1.2 kwa Shirika la Ndege la Tanzania

(ATC) kama jitihada za kusaidia ufufuaji wake, lakini kwa kadiri muda unavyosonga mbele kuna kila dalili ya kwamba uwezekano wa marerejesho ya fedha hizi ni mgumu; na kwamba mkopo huo haulipiwi riba.

Zaidi ya hayo ilibainika kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ilifanya malipo kabla ya kupokea mali (advance payment) ya kiasi cha Shilingi milioni 643.76 kwa Toyota Tanzania Ltd mwezi Aprili, 2008 kwa ajili ya ununuzi wa magari. Katika kiasi kilichotolewa magari yenye thamani ya Shilingi milioni 471.3 yaliletwa mnamo tarehe 15 Agosti 2008 na mengine yenye thamani ya Shilingi milioni 137.9 tarehe tarehe 30 Juni 2010. Hivyo kiasi cha shilingi milioni 34.4 kati ya fedha zilizolipwa kwenye fedha za awali hazijarejeshwa kwenye mamlaka yapata takribani miaka mitano sasa. Hakuna makubaliano juu ya jinsi fedha zitakavyorejeshwa. Huu ni uvunjifu wa sheria za usimamizi wa fedha za umma ambapo imeelezwa wazi kwamba fedha zisilipwe kwa wauzaji wa bidhaa au huduma kabla ya kupokea mali na kama makubaliano ya mkataba yanaruhusu basi ni muhimu zirejeshwe ndani ya kipindi cha miezi 12. Kama muuzaji au mtoa huduma atashindwa kutimiza wajibu wake, kinyume cha hapo adhabu kali inapaswa kutolewa.

7.5 Udhaifu Katika Usimamizi wa Vifaa Ghalani

Sura ya pili na Aya ya 6 (c) ya kanuni za kihasibu za kimataifa (IAS.2) inaeleza kuwa vifaa ghalani ni mali ambayo inategemewa kutumika katika mchakato wa uzalishaji au katika utoaji huduma. Vifaa ghalani vinawakilisha sehemu kubwa ya mali za shirika na hivyo zinahitaji kusimamiwa vyema ili kuondoa uwezekano wa upotevu, wizi au matumizi mabaya. Katika ukaguzi ilibainika kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yamekuwa yakipata hasara inayosababishwa na usimamizi mbovu au matumizi yasiyo sahihi ya mali ghalani. Niliweza kuona udhaifu kwenye baadhi ya

mashirika kama yalivyoainishwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 7: Mashirika yenye Udhaifu Katika Usimamizi wa Vifaa Ghalani

Na:	Shirika	Mapungufu Yaliyoonekana
1	Banki Kuu ya Tanzania	Hakukuwa na uwiano sahihi kati ya 'inventory receivable control account' mwishoni mwa mwaka.
2	TANESCO	<ul style="list-style-type: none"> • Ilionekana kuwa "CONDUCTOR (ACSR) BARE" zenye namba za usajili 01B3030 zilirekodiwa kwa mapungufu ya kiasi cha mita 79,860 na pia kuonekana kwenye vitabu zikiwa na thamani pungufu ya Shilingi milioni 233.1. Hii ina maana kwamba uhalisia wa mali katika ghala ulirekodiwa kwa mapungufu. • Udhaifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa mali ghalani umechangia matatizo katika usuluhishi wa makosa yaliyoonekana wakati wa kuhesabu vifaa na idadi iliyorekodiwa kwenye mifumo ya kompyuta ya shirika.
3	Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC)	Vitabu vya kutunza kumbukumbu za vifaa havikuonyesha thamani halisi ya vifaa husika.
4	Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Kahama Shinyanga	Pampu za maji, vipuri, mabomba pamoja na vishikizo mbalimbali katika mtambo wa kutakasa maji wa lhelele, pamoja na vifaa vya umeme havikuonyeshwa thamani yake.
5	Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Mtwara	<ul style="list-style-type: none"> • Ukaguzi ulibaini tofauti katika karatasi za kuhesabia vifaa. • Kulikuwa na tofauti ya Shilingi milioni 116.92 kati ya "Bin Tally Cards" na makabrasha ya uhakiki.
6	Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Arusha	Uhakiki uliofanywa ulibaini tofauti kati ya kadi ya kutunza mali ghalani (bin card).

7.6 Kutokuwa na Daftari la Kumbukumbu za Mali Zisizohamishika

Ili kuweka kumbukumbu ya mali zisizohamishika na ili kuhakikisha udhibiti wa matumizi mabaya ya mali hizo, Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo zinapaswa kuweka kumbukumbu sahihi za rasilimali za kudumu.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi ilibainika kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo hazikuwa au hazikuhuisha kumbukumbu katika daftari la mali za kudumu. Madhaifu yaliyobainika yanajumuisha kutokuwa na daftari la mali, kutohuisha daftari la mali na vifaa kutorekodiwa kwenye daftari la mali za kudumu. Pia mali za kudumu zilizonunuliwa mwaka wa ukaguzi, hazikuwa zimeingizwa kwenye daftari la mali za kudumu. Mambo hayo yalibainika katika mashirika ya KUWASA, TANESCO, MWAUWASA, BAWASA, CDA na PPF.

7.7 Usimamizi wa Uwekezaji Katika Mifuko ya Pensheni

Usimamiaji wa uwekezaji ni usimamizi wa kitaalam wa dhamana mbalimbali (hisa, na dhamana nyingine) na mali (kwa mfano, mali zisizohamishika) ili kufikia malengo ya uwekezaji kwa ajili ya faida ya wawekezaji. Hii inaweza kuhusisha upembuzi wa mali, hisa, utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango inayoendelea kwenye uwekezaji. Hata hivyo, katika hili, mapungufu kadhaa yameonekana wakati wa ukaguzi wa uwekezaji unaofanywa na kusimamiwa na mifuko ya hifadhi ya Jamii kama ilivyoelezwa hapa chini:

(i) Uwekezaji Katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Ukaguzi wa uwekezaji wa NSSF katika Chuo Kikuu cha Dodoma ulibaini mapungufu kadha wa kadha. Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko haukusaini mkataba wa mradi kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Mfuko ulitumia jumla ya Shilingi bilioni 234 katika mradi huu lakini ulisaini mkataba wa awamu ya kwanza wa Shilingi bilioni 35.2 tu. Majengo kwa ajili ya awamu ya kwanza yalikamilika na kuwekwa katika matumizi mwezi Septemba, 2008. Mpaka wakati wa ukaguzi, Mfuko haujaweza kukusanya malipo ya pango kutoka Serikalini na hadi sasa limbikizo la riba limefikia thamani ya Shilingi bilioni

14. Zaidi ya hayo, kiasi kilichotumika kufadhili mradi awamu ya kwanza kimekuwa kikitambuliwa kama mkopo na sehemu ya riba kuwa mtaji kinyume na masharti ya mkataba ambayo yanasema mradi ambao ni aina ya kubuni, kujenga, kumiliki na kuhamisha (Design Build, Own and Transfer), ambapo Mfuko utapokea kodi iliyokokotolewa kwa gharama za uwekezaji na riba ambayo ni 15% kwa kipindi cha miaka 10. Mifuko mingine ambayo imewezeza katika Chuo Kikuu cha Dodoma katika mikataba kama hiyo ni kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na.8: Mifuko ya Pensheni Iliyotoa Mikopo Chuo Kikuu Dodoma

Na:	Mfuko	Salio hadi 30 Juni, 2011	Maoni
1	PPF	39,987,406,969.60	Marejesho hayarejeshwi kulingana na makubaliano
2	PSPF	105,921,805,194.00	Marejesho hayarejeshwi kulingana na makubaliano
3	LAPF	22,030,563,286.00	Marejesho hayarejeshwi kulingana na makubaliano
4	NHIF	13,403,753,000.00	Marejesho hayarejeshwi kulingana na makubaliano
Jumla		181,343,528,449.60	

- ii) **Uwekezaji Katika Taasisi ya Serikali ya Kiusalama**
 Ukaguzi ulibaini kuwa NSSF walikopesha Taasisi ya Kiusalama jumla ya Shilingi bilioni 5.33 kwa riba ya mwaka ya 15% ya mkopo ambao utarejeshwa katika kipindi cha miaka kumi (10) tangu mwaka 2007 kwa

ajili ya ujenzi wa majengo. Masharti ya mkataba yanasema mradi huo ni aina ya kubuni, kujenga, kumiliki na kuhamisha (Design Build, Own and Transfer). Hivyo mfuko ulipaswa kupokea kodi iliyokokotolewa kwa msingi wa gharama halisi za uwekezaji kwa muda wa miaka kumi (10). Taasisi hiyo ya Umma ya Kiusalama hadi sasa bado haijaanza kulipa deni pamoja na sehemu ya riba ya mkopo. Taasisi hiyo ya Umma ya Kiusalama ilipaswa kuanza kulipa riba na kufanya malipo ya sehemu ya mkopo tangu Disemba 31, 2010. Mfuko mwingine uliowekeza katika mradi huu kwa masharti kama yalivyoainishwa hapo juu ni PSPF ambapo hadi Juni 30, 2011 mfuko unadai jumla ya Shilingi bilioni 6.4.

(iii) Ukumbi wa Bunge Dodoma

Ukaguzi ulibaini kuwa mkopo wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa Bunge Dodoma haulipwi kwa mujibu wa ratiba na makubaliano, na kiwango kilichokuwa kinadaiwa kutoka serikalini hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2011 kwa NSSF kilikuwa ni Shilingi bilioni 8.96 na PPF Shilingi bilioni 7.9 na LAPF Shilingi bilioni 2.91 jumla Shilingi bilioni 19.77.

(iv) Nyumba za Polisi Chini ya Wizara ya Usalama wa Raia

NSSF ilikopesha Wizara ya Usalama wa Raia kiasi cha Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za polisi kwa riba ya mwaka ya 15% mwaka tangu 2007. Mwaka 2008 mkataba wa nyongeza ulisainiwa ili kuongeza kiwango cha mkopo kwa ulipaji wa kipindi cha miaka 10. Hadi sasa mkopo haujaanza kulipwa kama Mkataba wa upangaji unavyoelekeza.

(v) Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Machinga Complex)

Ukaguzi ulibaini kuwa mwaka 2007 NSSF ilitoa mkopo wa kiasi cha Shilingi bilioni 12.9 wenye riba ya 14.9% kwa mwaka. Hadi sasa hakuna malipo ya riba wala

sehemu ya mkopo yaliyofanyika kinyume na mkataba. Kufikia tarehe 30 Juni, 2011 kiasi cha Shilingi bilioni 15.3 kilikuwa bado kinadaiwa na mfuko.

Mikopo mingine ambayo hailipwi kulingana na mikataba iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni mikopo iliyotolewa kwa Continental Venture Tanzania Limited, Meditech Industrial Co. Ltd, General Tyre, Kiwanda cha Sukari Kagera, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Mgodhi wa Makaa ya Mawe Kiwira. Kushindwa kulipa madeni kwa taasisi hizi ambazo baadhi yake zilipata udhamini wa serikali kunatia shaka kama upembuzi wa kina wa wakopaji ulifanywa na mifuko ya kijamii kabla ya kutoa mikopo hiyo. Pamoja na hayo ukubwa wa kibiashara kati ya Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unatia shaka kutokana na kusuasua kwa serikali katika ulipaji wa madeni yake. Hii inahatarisha uendelevu wa mifuko hii.

7.8 Udhaifu Katika Udhubiti na Usimamizi wa Fedha

Usimamizi wa fedha ni muhimu kwa kila shirika au taasisi ya umma. Kwa kujua hilo ni muhimu kiasi cha fedha kinachotegemewa kupokelewa au kutumika kiweze kusimamiwa vyema kwa ajili ya maendeleo ya taasisi husika. Kwa maoni hayo, wakati wa ukaguzi yalibainika mapungufu juu ya udhubiti wa fedha ambao umesababisha hasara kwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma. Miongoni mwa madhaifu yalionekana ni ucheleweshaji wa maandalizi ya usuluhishi wa kibenki, ukosefu wa uangalizi wa utawala juu ya makusanyo ya kila siku, ucheleweshaji wa kupeleka makusanyo ya siku benki kwa wakati kama sheria zinavyotaka, kutokuwepo kwa mgawanyo wa kazi za usimamizi wa fedha. Mapungufu hayo yamesababisha hasara ya jumla ya Shilingi milioni 421.9 kwenye Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Mwanza. Pia mapungufu kama hayo yalibainika kwenye mamlaka na taasisi zifuatazo; Baraza la Kiswahili

Tanzania, Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Moshi, Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Kahama Shinyanga, na Benki ya Rasilimali Tanzania.

7.9 Viwango vya Uchakavu Visivyokuwa Sahihi

Aya ya 58 ya viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu Sura ya 16 inaelekeza ardhi na majengo kutenganishwa wakati wa kukokotoa thamani zake hata kama vimenunuliwa kwa pamoja. Hata hivyo wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa baadhi ya mashirika ya umma hayazingatii maelekezo hayo na hivyo kusababisha viwango vya uchakavu vilivyokokotolewa kutokuwa sahihi ikizingatiwa thamani ya ardhi haipungui bali hupanda kila wakati tofauti na ile ya majengo ambayo huenda ikashuka na kupanda kutegemea na hali halisi ya jengo husika. Makosa haya yanasababisha kiasi kilichoripotiwa kama faida au hasara kutokuwa sahihi. Pia Aya ya 33 ya viwango vya kimataifa vya kihasibu (IAS) Sura ya 8 inaelekeza kufanyika makadirio ambayo ni ya uhakika. Ukaguzi umebaini kuwa Mashirika mbalimbali yanatumia viwango tofauti tofauti, ambavyo vimeleta utofauti pia katika kuandaa mahesabu.

7.10 Udhaifu Katika Usimamizi wa Fedha na Mikopo

Kanuni za kibenki na taasisi za fedha za mwaka, 2008 zinaelekeza wakopaji kulipa riba yote za iliyotangulia ambayo haikulipwa pamoja na gharama zote za mkopo na angalau asilimia kumi ya mkopo. Hata hivyo mapitio ya mpango wa marekebisho ya mikopo ya Benki ya Rasilimali ulibainisha zoezi hilo kutofuata kanuni na miongozo kama inavyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Marekebisho hayo ya mikopo katika Benki ya Rasilimali yasiyozingatia miongozo sahihi inayotolewa na Benki Kuu yanahatarisha kuongezeka kwa madeni yasiyolipika hapo siku za baadae. Pamoja na hayo, tathmini ya mikopo hiyo iliyofanyiwa marekebisho na kutolewa katika makampuni mbalimbali kati ya mwaka

2004 na 2005 ikiwa ni kwa ajili ya kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi, inaonyesha walionufaika na marekebisho hayo hawakurejesha au kuheshimu wajibu wao wa kulipa riba au sehemu ya mikopo yao kwa wakati uliokubalika katika mikataba yao mipya baada ya marekebisho.

Hii inaonyesha umuhimu wa kufanya mapitio ya kina ili kuweza kujua kiasi kitakachopatikana kutokana na mpango huu ikiwa Serikali itaendelea kufadhili miradi hii na kuishauri Wizara ya Fedha ipasavyo.

7.11.Vyanzo vya Uhakika vya Fedha kwa Ajili ya Uwekezaji

Maendeleo ya Taifa lolote lile hutegemea sana uchumi imara, na ili kufikia lengo hili upatikanaji wa vyanzo vya kuaminika vya fedha kwa ajili ya uwekezaji ni muhimu sana. Kwa hiyo, Tanzania kama Taifa ni muhimu sana ikabuni mikakati ya kutafuta vyanzo vya kuaminika vya fedha kwa gharama nafuu.

7.11.1 Vyanzo vya Kuaminika vya Fedha

Tanzania tuna fursa ambazo bado hazijatumika na ambazo zinaweza kuwa vyanzo vya fedha kwa ajili ya uwekezaji kama vile; Soko la Mitaji, Ubia kati ya Watu Binafsi na Serikali, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mali ambazo zimetelekezwa na wamiliki wake.

a) Soko la Mitaji la Dar es Salaam

Kwa sasa Soko la Hisa la Dar es Salaam lina idadi ndogo ya makampuni ambayo yamejisajili. Hii imesababishwa na kutokuwa na uelewa kwa baadhi ya makampuni na watanzania kwa ujumla. Kuna haja ya Serikali kutunga sheria itakayoyataka makampuni makubwa hapa Tanzania kusajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam mfano makampuni ya uchimbaji madini, makampuni ya simu za mkononi, makampuni ya saruji,

makampuni ya vinywaji baridi n.k. Kwa kuwa na idadi kubwa ya washiriki katika Soko la Hisa inaweza kuwa ni chanzo kikuu cha fedha kwa ajili ya maendeleo ya Taifa kupitia mauzo ya hisa. Makampuni makubwa na watu binafsi wanaweza kupata mitaji kwa ajili ya uwekezaji kutoka kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

b) Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya Hifadhi ya jamii inaweza kutoa fedha kwa ajili ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali za uchumi kama ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo na mengineyo. Hata hivyo, fedha za mifuko hiyo ni za wanachama, kwa hiyo umakini unatakiwa kuhakikisha kwamba uwekezaji unafanywa katika biashara zenye manufaa, na maandiko ya uwekezaji yanaandaliwa vizuri, yanachambuliwa kwa umakini, yanaidhinishwa bila muingiliano wa kisiasa katika maamuzi.

c) Fedha na Mali Zisizo na Wamiliki

Nimebaini kwamba kuna fedha na mali nyingi katika taasisi mbalimbali ambazo zimebaki bila kudaiwa na wenyewe kwa muda mrefu. Mali hizi ni pamoja na akiba za wateja zilizoko kwenye mabenki mbalimbali, hisa ambazo hazina mmiliki katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, makato ya kisheria kwa wafanyakazi walioachishwa kazi au kufariki ambao makato yao yanaendelea kupelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii, mifuko ya bima ya afya na gawio kwa makampuni yaliyosajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Kimsingi rasilimali hizi si mali ya taasisi hizi ila ni mali ya wamiliki wasiojulikana. Kama rasilimali hizi zitaachwa bila uangalizi makini kuna hatari ya kutumiwa vibaya au zinaweza kubaki bila kutumika.

Kuna haja ya Serikali kutunga sheria itakayozitaka taasisi za umma kurejesha mali hizo Hazina ili ziwe mapato ya Serikali kama ilivyo kwa akiba ambazo zimekaa bila kutumika kwa zaidi ya miaka mitano (5) na hazitarajiwi kutumika. Mali hizo ambazo hazina wamiliki zingeweza pia kuwekwa katika Mfuko Maalum wa Uwekezaji ili zitumike kama chanzo cha fedha za uwekezaji.

d) Ubia Kati ya Serikali na Taasisi Binafsi

Wawekezaji binafsi wanaweza kuingia ubia na Serikali katika shughuli za maendeleo kwa kuwa Serikali ina ardhi na rasilimali ambazo zinaweza kutumika kuingia ubia na wawekezaji binafsi katika maeneo kama kilimo, uchimbaji madini, uchimbaji na usambazaji wa gesi, ujenzi wa barabara n.k. Hata hivyo umakini unatakiwa wakati wa kuingia katika mikataba ya aina hiyo kwani baadhi ya wawekezaji si waaminifu na wanaweza kutumia mikataba hiyo kujinufaisha na hata kukiuka makubaliano.

Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inaweza kutafuta uwezekano wa kutumia ubia kati ya Serikali na Taasisi binafsi katika mipango ya kutafuta fedha za kuboresha barabara za Dar es Salaam - Chalinze - Morogoro na Moshi - Arusha ili kupunguza msongamano kwa kuzifanya ziwe za njia mbili. Marejesho ya gharama za huduma hii yanaweza kupatikana kupitia ulipaji wa kodi za barabara. Kwa kufanya hivyo Serikali itaweza kutatua tatizo la msongamano wa magari linalowakabili watu, kupata mapato na kwa wakati huhuo kupunguza ajali za barabarani zinazoweza kuepukika.

7.11.2 Kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma

Serikali inapaswa kuwa na mpango mkakati wa kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ili iweze kutekeleza shughuli za kimaendeleo nchini. Katika

kutengeneza uwekezaji, ajira zaidi zitaundwa, wigo wa mapato utapanuka na hivyo kuwawezesha watu na kuondoa umaskini. Pia ikumbukwe kuwa pasipo uwekezaji wigo wa kodi hautapanuka.

Fedha za uwekezaji zinaweza zikatokana na gawio kutoka kwenye uwekezaji wa umma. Mapato yatakayotokana na mauzo ya mali za Serikali yanaweza pia kuwa chanzo cha fedha katika Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ili kuongeza ukwasi. Kwa upande mwingine Serikali inaweza ikawa na tengo katika bajeti zake za mwaka kwa ajili ya kutunisha mfuko huu. Kwa hali hiyo basi, Serikali inapaswa iweke msisitizo katika kuelekeza mapato yake katika kufadhili mfuko huu kwa kuwa haitatokea siku mapato ya Serikali yakatosheleza.

SURA YA NANE

USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

8.0 Utangulizi

Usimamizi wa Rasilimali Watu ni kazi ndani ya taasisi ambayo inahusika na uajiri, kusimamia na kutoa mwelekeo kwa watu wanaofanya kazi katika taasisi husika.

Sura hii inajumuisha muhtasari wa hoja muhimu ambazo zinaelezea mapungufu ya usimamizi wa rasilimali watu katika mashirika ya umma, zilizotokana na ripoti za mashirika husika ambazo zimeonyesha umuhimu wa taarifa zake kutolewa katika ripoti hii ya mwaka. Hoja hizo ni kama ifuatavyo:-

8.1 Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wafanyakazi

Upimaji wa utendaji kazi wa wafanyakazi ni njia ambayo utendaji kazi wa watumishi hupimwa na msimamizi wa kazi au meneja wake. Hii ni mojawapo ya njia ya kuelekeza na kusimamia maendeleo ya taaluma.

Kama ilivyoripotiwa katika ripoti ya mwaka uliopita, mashirika ya umma yanapaswa kufuata utaratibu wa kupima utendaji kazi wa wafanyakazi ili kuipa menejimenti vigezo sahihi vya kumzawadia mfanyakazi kama vile kutoa nyongeza ya mshahara, kupandisha vyeo au kupendekeza mafunzo kwa wafanyakazi. Ni muhimu pia kuelewa kwamba ili kuwa na matumizi mazuri ya matokeo ya upimaji wa utendaji kazi, upimaji huu ni lazima ufanywe katika mwaka husika wa fedha.

Tathmini ya kuangalia kama utaratibu wa upimaji kazi unafuatwa ulifanywa na kubaini kwamba, baadhi ya mashirika ya umma bado yana tatizo la kufuata

utaratibu huu ingawa limeelezwa vizuri katika taratibu za utumishi za shirika husika. Hii imethibitishwa kwa kukosekana kwa taarifa za upimaji wa utendaji kazi katika majalada ya wafanyakazi na katika kumbukumbu nyingine za shirika. Upungufu huu waweza kumnyima mfanyakazi haki ya kuzawadiwa kulingana na upimaji kazi ambao ungefanywa. Kwa kujua kuwa hakutakuwa na upimaji wa utendaji kazi wafanyakazi wanaweza kupunguza ari ya kufanya kazi. Mfano wa mashirika yenye mapungufu haya ni shirika la Magazeti Tanzania (TSN) na SUMATRA.

8.2 Uajiri wa Wahasibu au Wakaguzi Wasiokuwa na Sifa

Kifungu cha 24 cha Sheria Na. 33 ya usajili wa wahasibu na wakaguzi ya mwaka 1972, kama ilivyorekebishwa inatamka kwamba taasisi yeyote inayofanya shughuli zake za kibiashara au kitaaluma Tanzania na kuwa na mali zenye thamani ya Shilingi milioni 100 au zaidi au kuwa na mauzo ya bidhaa ya asilimia 50 au zaidi ni lazima iajiri mkuu wa kitengo cha uhasibu na ukaguzi aliyefuzu na kusajiliwa na bodi ya uhasibu. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya mashirika ya umma wana wakuu wa vitengo vya uhasibu na ukaguzi ambao hawana sifa kinyume na matakwa ya sheria ya usajili wa wahasibu na wakaguzi. Mapungufu haya yapo katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba. Ni muhimu kutambua kuwa kufuata sheria na kanuni mbalimbali zitolewazo na Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi kutaongeza ufanisi katika utendaji kazi katika eneo la uhasibu na ukaguzi.

8.3 Upungufu wa Wafanyakazi Katika Nafasi Muhimu za Kiutendaji

Katika kaguzi za mwaka huu tumebaini, nafasi muhimu kiutendaji katika baadhi ya Mashirika ya Umma zilikuwa wazi. Katika Bodi ya Korosho muundo wa kiuongozi uliopopitishwa na bodi ya wakurugenzi mwezi Machi, 2007 na baadaye kupitishwa na Msajili wa

Hazina mwezi Mei, 2007 ulikuwa na idadi ya wafanyakazi 73 wanaotakiwa. Hata hivyo, mpaka wakati wa ukaguzi idadi ya wafanyakazi ilikuwa ni 58 tu na hivyo kuacha nafasi 15 zikiwa wazi. Si hivyo tu, katika Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji Mkuu Dodoma nafasi za Mkuu wa Mazingira, Meneja wa Rasilimali Watu, Meneja Uhusiano, na Afisa Usalama Mkuu zilikuwa wazi kwa muda mrefu na baadhi kwa zaidi ya miaka mitatu (3). Upungufu huu husababisha udhaifu wa menejimenti na hivyo kuzorotesha michakato ya utoaji maamuzi. Pia ukaguzi katika Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma ulibaini kuwa baadhi ya nafasi zilishikiliwa kwa kukaimu kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini;

Jedwali Na.9: Upungufu wa Wafanyakazi Katika Nafasi Muhimu za Kiutendaji Kwenye Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji Mkuu Dodoma

	Nafasi	Juni 2011	Juni 2010
1.	Mkurugenzi wa Fedha na Utawala	Nafasi wazi (imekaimishwa)	Nafasi wazi (imekaimishwa)
2.	Director of Estates Development	Nafasi wazi (Imekaimishwa)	Nafasi wazi
3.	Director of Planning	Nafasi wazi (Imekaimishwa)	Nafasi wazi
4.	Head of Land Division	Nafasi wazi (Imekaimishwa)	Nafasi wazi

Imebainika pia katika Baraza la Uwezeshaji la Taifa (NEEC), kati ya nafasi 18 zilizoanishwa katika muundo wa kiuongozi, nafasi nane zilikuwa wazi. Kwa kiwango kikubwa kama hicho cha nafasi kuwa wazi ni vigumu kwa baraza kuwa na ufanisi kiutendaji. Zaidi ya hayo, nafasi ya Meneja wa Huduma za Kitaalam ya Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi (NBAA) ambayo ni muhimu katika

utendaji wa bodi imekuwa wazi toka mwaka 2008. Hii imesababisha pia nafasi hii kukaimishwa.

8.4 Kucheleweshwa kwa Uwasilishaji wa Kodi ya Mapato ya Wafanyakazi na Kutowasilishwa kwa Michango ya Pensheni ya Wafanyakazi

Waajiriwa hulipa kodi za mapato kwa kila mwezi. Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato 2004. Mwaka wa mapato unaanzia tarehe 1 January na kuishia tarehe 31 Disemba ya kila mwaka. Mishahara yote ya wafanyakazi na malipo mengine yahusuyo ajira hukatwa kodi ya mapato na kiasi cha kodi kinachokatwa na kuzuiwa na mwajiri hupelekwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato kabla ya siku ya saba (7) ya mwezi unaofuatia mwezi wa makato.

Mapitio yaliyofanywa kuhusu uwasilishaji wa makato hayo katika mashirika ya umma ulibaini kuwa, makato ya kodi kwa baadhi ya miezi hayakuwasilishwa kwenye Mamlaka ya Mapato Tanzania katika tarehe husika. Ucheleweshwaji huu wa makato ya kisheria unaweza kusababisha tozo za adhabu na hivyo kusababisha malipo yasiyopangwa. Kutofuatwa kwa sheria kunaweza kukaharibu sifa ya shirika la umma ambalo linatarajiwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na kwa upande wa waajiriwa hali hii inaweza kupunguza ari yao ya kufuata sheria za kodi wakitambua kuwa makato yao ya kodi hayafiki kwenye mamlaka husika au yanacheleweshwa. Mifano ya mashirika ya umma ambapo udhaifu huu ulibainika ni katika Soko la Mitaji (CMSA).

Pamoja na hitaji la kuwasilisha makato ya kodi katika mamlaka ya mapato, pia kuna mifuko mingine inayohitaji michango ya wanachama ambao ni wafanyakazi wa mashirika ya umma. Mifano ya mifuko hiyo ni NHIF, PPF, NSSF na LAPF. Mapitio ya ukaguzi kuangalia uwasilishwaji wa makato hayo ulibaini kuwa

baadhi ya mashirika ya umma hayawasilishi makato hayo kwa wakati, au huwasilisha kiasi tu au kutowasilisha kabisa. Katika mwaka huu ufuatiliaji wa makato ya mishahara kuangalia uwasilishwaji wa makato ya Bima ya Afya uliofanywa na Shirika la Elimu Kibaha ulibaini kwamba mwajiri aliwasilisha asilimia tatu (3) tu iliyochangwa na mwajiriwa bila ya kiasi anachongia mwajiri. Katika suala hili kati ya Shilingi milioni 163 zilizotakiwa kuwasilishwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya ni Shilingi milioni 77.9 tu ndizo zilizowasilishwa na kuacha kiasi cha Shilingi milioni 85 ambacho kimeonyeshwa kama deni ambalo shirika linadaiwa. Hali hii inaweza kushusha ari ya wafanyakazi kutokana na kutokuwa na uhakika na bima yao ya afya unaosababishwa na mwajiri kutowasilisha michango katika mfuko. Zaidi ya hayo uhakiki wa uwasilishaji wa makato ya PPF katika Taasisi ya Elimu Kibaha ilibainika kuwa Shilingi milioni 24.8 zilikuwa bado hazijawasilishwa katika mwaka huu. Hii inaweza kusababisha wafanyakazi kutolipwa haki zao wakati wa kustaafu na pia kunaweza kusababisha tozo za adhabu. Mifano mingine ya Mashirika ya Umma yaliyoshindwa kuwasilisha makato ya lazima kwa wakati au hayakuwa na ushahidi wa kuwasilisha makato hayo ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kibaha, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

8.5 Kutohibitishwa kwa Wafanyakazi

Ilibainika kuwa baadhi ya mashirika ya umma hayana mfumo wa kuhakikisha kuwa tarehe za kuthibitisha wafanyakazi zinatambulika kwa urahisi ili kuondoa uwezekano wa kukaa na watumishi ambao hawajathibitishwa kwa muda mrefu. Njia mojawapo ambayo inaweza kutumika ni kutumia mfumo maalum wa kusimamia rasilimali watu (Human Resources Management System) ambao unaweza kutoa taarifa kuashiria kufikia kwa tarehe ya mfanyakazi kuthibishwa ili upimaji utendaji kazi wa mfanyakazi

ufanyike kwa ajili ya kuthibitishwa. Uchambuzi wa taarifa za wafanyakazi wa mashirika ya umma ulibaini kuwa baadhi ya wafanyakazi wamekaa kwa kipindi kirefu baada ya tarehe zao za kuthibitishwa kupita bila kuthibitishwa. Kwa mfano katika Shirika la Elimu Kibaha wafanyakazi watano (5) walibaki kwa kipindi hadi cha miezi sita baada ya kumalizika kwa kipindi chao cha majaribio bila kuthibitishwa. Kushindwa kuwathibitisha wafanyakazi kwa wakati ni kuwanyima haki zao.

8.6 Kuondolewa kwa Wafanyakazi 115 wa Shirika la Elimu Kibaha Kutoka Katika Orodha ya Malipo ya Mishahara ya Hazina

Mishahara ya wafanyakazi wa baadhi ya mashirika ya umma hutegemea fedha kutoka Hazina. Kwa mfano Shirika la Elimu Kibaha hutayarisha orodha yake ya malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wake lakini inategemea fedha kutoka Hazina. Katika kupitia orodha ya malipo ya mishahara ya kituo cha Elimu Kibaha ilibainika kuwa majina ya wafanyakazi 115 waliondolewa kutoka orodha ya malipo ya mishahara ya Hazina mwezi Machi, 2011 na kusababisha kituo kushindwa kulipa mishahara. Hata hivyo, kituo kilitumia chanzo kingine cha fedha kulipa mishahara ya wafanyakazi walioondolewa kutoka orodha ya malipo ya Hazina na kusababisha nakisi katika bajeti ya kituo kwa Shilingi milioni 86.1. Fedha hizi zilitengwa kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya shughuli za maendeleo na zikahamishiwa kulipa mishahara hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

8.7 Kumbukumbu za Rasilimali Watu na Mifumo ya Taarifa za Rasilimali Watu

Baadhi ya mashirika ya umma yenye idadi kubwa ya wafanyakazi yana matatizo katika kusimamia kumbukumbu za rasilimali watu. Shirika la Posta Tanzania lenye wastani wa watumishi 1,200 ni

miongoni mwa mashirika yenye changamoto katika utunzaji wa kumbukumbu za rasilimali watu. Tatizo hili la kushindwa kuweka kumbukumbu hizo linatokana na kutokuwepo mifumo ya kutunza kumbukumbu iliyobuniwa kupunguza kazi za mikono kwa ajili ya kazi za kiutawala. Mifumo hii ni kama vile Mfumo Maalum wa Utunzaji Kumbukumbu za Rasilimali Watu (HRMS) au Mfumo wa Utunzaji Taarifa za Rasilimali Watu (HRIS). HRMS na HRIS ni mifumo inayounganisha dhana ya usimamizi wa rasilimali watu na teknolojia ya mawasiliano.

Kazi za idara za rasilimali watu ni za kiutawala na zinazofanana kwa taasisi zote, HRMS na HRIS zinaweza kutumiwa na mashirika ya umma kusaidia uchaguzi wa wafanyakazi wakati wa uajiri, kufanya tathmini na kufanya kazi za kuandaa mishahara. Kazi nyingine zinazoweza kufanywa na mifumo hiyo ni kufuatilia taarifa za mfanyakazi husika zikiwemo historia ya mfanyakazi, ujuzi, uwezo na ulipaji wa mishahara.

8.8 Miongozo ya Utumishi Iliyopitwa na Wakati

Ufuatiliaji wa miundo ya utumishi ya baadhi ya mashirika ya umma umebaini kuwa, baadhi yake imepitwa na wakati. Kwa mfano katika Shirika la Magazeti la Taifa (TSN) imebainika kuwa, muundo mpya wa kiuongozi hauendani na miongozo ya utumishi iliyopo. Hii inaweza kusababisha migongano ya maelekezo ya utendaji inayotokana na tofauti zilizopo kati ya miongozo ya utumishi ya shirika na muundo wa kiuongozi.

8.9 Mifumo ya Usimamizi wa Rasilimali Watu

Katika mwaka huu wa ukaguzi, ulifanyika ukaguzi wa menejimenti kwa baadhi ya mashirika ya umma ambayo ni Mamlaka ya Udhubiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA), Chuo Kikuu Dodoma, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na Shirika la Ndege la

Taifa (ATCL). Mojawapo ya maeneo ambayo yamepitiwa ni mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, ambayo ni:

- (i) Mipangilio ya Usimamizi wa Rasilimali Watu;
- (ii) Sera za Usimamizi wa Rasilimali watu;
- (iii) Mikakati na mipango ya rasilimali watu;
- (iv) Kuajiri na kutumia rasilimali watu;
- (v) Kutoa mafunzo;
- (vi) Kupima utendaji kazi; na
- (vii) Kutoa motisha kwa wafanyakazi na mazingira ya kazi.

Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

- **Sera na Taratibu za Usimamizi wa Rasilimali Watu**

Ili kuwa na usimamizi bora wa rasilimali watu inabidi kila shirika la umma liwe na sera za rasilimali watu kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa rasilimali watu za kila siku. Katika viwango tofauti taasisi zote zilizokaguliwa zilishindwa katika kipimo hiki. Baadhi ya taasisi hazikuwa na sera za ajira na uajiri (TCRA), mashirika mengine hayakuwa na mwongozo wa usimamizi wa rasilimali watu (STAMICO) na kukosa mwongozo wa kiutumishi kwa watumishi wa vitivo vya vyuo (UDOM).

- **Mikakati na Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali Watu**

Mkakati wa kitaasisi wa rasilimali watu unaweza kujumuisha sera za uajiri na uchaguzi, taratibu za maadili, sera za kuwazawadia watumishi, mipango wa rasilimali watu au sera za mafunzo na kuendeleza wafanyakazi. Sehemu zote hizi za usimamizi wa rasilimali watu zinapaswa zioanishwe ili kuendana na mkakati wa kiujumla wa shirika.

Kati ya mashirika manne yaliyofanyiwa ukaguzi wa menejimenti, hakukuwa na shirika ambalo lilikuwa na

mkakati wa rasilimali watu au ambalo limewatumia wafanyakazi wake kadiri ya mpango wa rasilimali watu. Baadhi ya mashirika hayakuwa na ikama ya wafanyakazi ambayo inaeleza idadi ya wafanyakazi wanaohitajika (TCRA na UDOM). Ukosefu huu wa idadi ya wafanyakazi inayohitajika umegundulika pia katika ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2011. Hii inaweza kusababisha kushindwa kutambua kama menejimenti inafuata mahitaji ya idadi sahihi ya wafanyakazi katika kila idara. Bila idadi ya wafanyakazi iliyothibishwa kwa kila idara, taasisi inaweza kuajiri watumishi zaidi ya mahitaji.

- **Uajiri na Upangaji wa Rasilimali Watu**

Uajiri ni kazi muhimu katika usimamizi wa rasilimali watu inayolenga kupata idadi inayostahili ya wafanyakazi wenye ujuzi, uzoefu na umahiri unaostahili katika kazi sahihi na katika wakati unaostahili ili kutekeleza majukumu ya shirika la umma. Mashirika ya umma yanahitajika kuwa na nyenzo au mwongozo utakaokuwa na taratibu zote zinazohusu uajiri na uendeleu wa mfanyakazi. Pamoja na jitihada za kuajiri, baadhi ya mashirika ya umma yaliyokaguliwa yalikuwa na upungufu wa wafanyakazi. Mifano ni UDOM, TCRA na ATCL. Shirika lingine lililokuwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi ni PPRA.

- **Mafunzo na Uendelezaji Wafanyakazi**

Mafunzo kwa wafanyakazi yanalenga kuongeza maarifa na kumwezesha mfanyakazi kupata njia mpya za kufanya kazi. Kwa kuwa mafunzo ni muhimu na yenye gharama, inahitajika kupangwa katika njia nzuri, mtazamo mkubwa katika kutambua mahitaji ya mafunzo; kuandaa mipango ya mafunzo na kutengeneza bajeti ya mafunzo na uendelezaji

wafanyakazi. Mapungufu yaliyoonekana katika taasisi zote ni:-

- (i) Kukosekana kwa uchambuzi wa mahitaji ya mafunzo kwa ajili ya kuandaa mpango wa mafunzo;
- (ii) Ukosefu wa mpango na bajeti ya mafunzo;
- (iii) Kutokuwa na mafunzo ya utangulizi kwa waajiriwa wapya,
- (iv) Bajeti ndogo za mafunzo na ukosefu wa usimamizi na tathmini ya mafunzo na uendelezaji wa wafanyakazi. Pamoja na hoja hizo zilizotokana na ukaguzi wa menejimenti, ufuatiliaji wa kuangalia kama sera za mafunzo za Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) zinafuatwa, uliofanyika na ukaguzi wa kawaida wa mwaka ilibainika kuwa mpango wa mafunzo unaotokana na sera za mafunzo haukufuatwa inavyopaswa. Ilionekana kwamba baadhi ya wafanyakazi walihudhuria mafunzo ambayo hayakuwa na bajeti na hayakuwa kwenye mpango wa mafunzo. Baadhi ya wafanyakazi walihudhuria mafunzo ambayo hayana mahusiano ya moja kwa moja na shughuli zao za kila siku. Baadhi ya wafanyakazi walihudhuria mafunzo zaidi ya mara moja wakati wafanyakazi wengine kwenye idara hiyo hiyo hawakuhudhuria mafunzo hata mara moja. Ilibainika pia kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro haikuwa na mpango wa mafunzo na haikufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo. Kutokufuatwa kwa sera ya mafunzo na baadhi wa wafanyakazi kutopewa fursa ya kuhudhuria mafunzo kunaweza kusabisha kupungua kwa tija kwa sababu ya ari ya kazi kuwa chini ya kiwango. Hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo inafanywa, mipango ya mafunzo inaandaliwa na vigezo vya uchaguzi kama vilivyo katika sera za mafunzo vinafuatwa wakati wote, na kwamba wafanyakazi wote wanapewa fursa sawa za mafunzo kulingana na tathmini ya mahitaji ya mafunzo.

- **Mifumo ya Upimaji wa Utendaji Kazi**

Mfumo wa Tathmini na Upimaji Utendaji kazi ni mfumo wa kupitia na kujadili utendaji kazi wa mfanyakazi kwa kazi na majukumu aliyopangiwa. Serikali ilianzisha Mfumo wa Tathmini na Upimaji Utendaji kazi (OPRAS) mwezi Julai, 2004 kupitia waraka No. 2 wa 2004. OPRAS iliondoa mfumo wa upimaji utendaji kazi wa siri ambao ulionekana kutochochea ubora wa utendaji kazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Mashirika hayo manne yalishindwa katika viwango tofauti kuhusiana na mifumo ya upimaji na utendaji kazi.

- **Motisha kwa Wafanyakazi na Mazingira ya Utendaji Kazi**

Motisha kwa wafanyakazi ni sababu kubwa ya mafanikio au kushindwa kufanikiwa kwa taasisi. Wakati watu wengine wanaweza kuhamasishwa kwa fedha, wengine wanaweza kuhamasishwa kwa kupewa nafasi za kujiendeleza kitaaluma, ratiba za kazi ambazo zaweza kubadilishwa na hamu ya kumaliza kazi. Hivyo basi, kwa Menejimenti na Viongozi wengine wa juu kuelewa sababu ambazo zinaweza kutoa motisha kwa wafanyakazi ni ufunguo wa kuweza kupata manufaa kutoka rasilimali watu.

Taasisi zote nne zilishindwa katika vipimo tofauti kuhusu mifumo ya motisha. Ingawa taasisi hizi zimeweka mazingira bora ya kazi. Ilibainika kuwa masuala ya motisha hayakupewa msukumo wa kutosha kwa kuwa mifumo ya motisha iliyopo haizingatii utendaji kazi. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Chuo Kikuu Dodoma (UDOM).

SURA YA TISA

UTAWALA BORA

9.0 Utangulizi

Sura hii inajadili masuala ya utawala bora yaliyotokana na kaguzi za mashirika ya umma na ambayo yaliripotiwa katika ripoti husika za Mashirika ya Umma kwa vipindi vinavyoishia tarehe 30 Juni, 2010, tarehe 31 Disemba, 2010 na tarehe 30 Juni, 2011. Sura hii pia itahusu mambo ya ujumla ya utawala bora ambayo yanahusu shughuli za Mashirika ya Umma na ambayo yameonekana kuwa ya msingi kuelezwa katika ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Utawala bora ni mfumo uhusuo utoaji wa mwelekeo na usimamizi wa mashirika ya umma. Ni mfumo unaoangalia mahusiano baina ya menejimenti ya kampuni, Bodi ya Wakurugenzi, wanahisa na washika dau wengine; Ni mfumo unaohusu uondoaji wa migongano ya kimaslahi kati ya washikadau husika. Njia za kuzuia migongano hii ya kimaslahi ni ya michakato, desturi, sera, sheria pamoja na taasisi ambazo zina athari juu ya kampuni inavyodhibitiwa. Ni muhimu kutambua kuwa dhana kuu ya utawala bora ni juu ya kiwango cha uwajibikaji wa watu na njia ambayo inajaribu kupunguza tatizo la kimahusiano yaani “principal - agent problem”.

Mwitikio wa utawala bora kwa makampuni unatoa uthibitisho kuwa makampuni hayo yanaongozwa na kutawaliwa kwa uwajibikaji, kitaaluma na kiuwazi kwa lengo la mafanikio ya muda mrefu. Inalenga pia kuongeza imani ya wanahisa na wawekezaji wa soko la mitaji, na pia imani kwa walipa kodi juu ya ubora kwa mashirika ya umma.

Tangu nilipotoa ripoti yangu ya kwanza mwaka 2006/2007, sura hii ya utawala bora imekuwa ikitoa mapendekezo mbalimbali kwa nia ya kuamsha utekelezaji wa utawala bora katika mashirika ya umma. Baadhi ya mapendekezo yametokelezwa na mengine bado hayajatekelezwa. Haijawekwa wazi sababu za serikali kushindwa kutekeleza mapendekezo yangu kwa kuwa majibu mahususi kuhusu udhaifu ulioainishwa hayajatolewa. Mtazamo wangu ni kwamba, itakuwa vyema iwapo serikali itabaini sababu za kushindwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kama njia ya kuweka mkakati wa utekelezaji wake. Aya zifuatazo zinatoa kwa muhtasari mapendekezo yaliyokwisha tolewa ambayo bado hayajatekelezwa.

Mapendekezo hayo ni yale yahasuyo ufanisi wa bodi za wakurugenzi, uteuzi wa wajumbe wa bodi wenye nyadhifa mbalimbali katika jamii hivyo kushindwa kutekeleza ipasavyo wajibu wao. Utaratibu wa uteuzi wa wakurugenzi, watendaji wa mashirika ya umma na wenyeviti wa bodi unaofanywa na mamlaka moja hivyo kupelekea mvutano wa kiutendaji, ucheleweshaji wa uteuzi wa bodi za wakurugenzi pale muda wa bodi unapoisha, kukosekana kwa mifumo ya uwajibikaji wa bodi za wakurugenzi, kukosekana kwa mwongozo unaoleta uwiano katika stahili za wajumbe wa bodi za wakurugenzi katika mashirika ya umma, udhaifu mbalimbali wa kiutendaji katika bodi za mashirika ya umma, utata katika muundo wa bodi ya Benki Kuu ya Tanzania, suala la wabunge kuwa wajumbe wa bodi mbalimbali za mashirika ya umma, udhaifu katika uundaji wa kamati za ukaguzi na masuala ya utendaji katika vitengo vya ukaguzi wa ndani katika mashirika ya umma. Mapendekezo haya ambayo hayajatekelezwa yameelezwa kwa undani katika sura ya tatu ya ripoti hii.

Ni muhimu kutambua kuwa, iwapo mapendekezo hayo hayatatekelezwa na Serikali kwa kuweka miongozo ya wazi juu ya jinsi ya kufuata kanuni za utawala bora katika mashirika ya umma. Mashirika hayo yatabaki bila mwongozo na hivyo kuendelea kutofuata kanuni za utawala bora.

Katika ripoti ya mwaka huu, nitaweka msisitizo katika mapungufu juu ya utawala bora ambayo yamekuwa yakijirudia, pamoja na mambo mapya ambayo hayakuwahi kuripotiwa katika ripoti zilizopita. Kupata uelewa kuhusu mambo haya ni muhimu kutafakari kwamba kufuata utawala bora ni wito unaopinga migongano ya kimaslahi katika pande zinazokinzana kwenye utawala bora.

9.1 Mapungufu Katika Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Ukaguzi wa ndani ni moja ya nguzo ya utawala bora ambayo inapaswa kutekelezwa katika mashirika ya umma. Ili kufanya kazi kwa ufanisi kitengo hiki kinapaswa kuwa na miongozo ya kiutendaji ya kitengo, na mipango ya kiukaguzi itakayogusa maeneo yote yaliyomo kwenye mpango mkakati wa mwaka. Mpango mkakati huo lazima ufanye upembuzi wa viashiria ya hatari juu ya utendaji wa shirika. Mambo mengine muhimu ambayo yanajenga vitengo vya ukaguzi wa ndani yanajumuisha; mwongozo wa ukaguzi wa ndani uliohibitishwa, njia za kunakili na kuhifadhi nyaraka za ukaguzi na kuwa na watumishi wa kutosha na ambao wamepata mafunzo stahiki.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika mwaka huu katika mashirika ya umma ulibainisha mapungufu mbalimbali katika vitengo vya ukaguzi wa ndani. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni ukosefu wa miongozo wa ukaguzi wa ndani na kanuni za ukaguzi wa ndani. Miongozo na kanuni za ukaguzi ni zana za kuongoza utendaji wa ukaguzi wa ndani na hivyo upungufu au ukosefu wake unaweza kudhoofisha utendaji wa

kitengo cha ukaguzi wa ndani. Mashirika ya Umma ambayo mapungufu hayo yalibainika ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza, Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji Mkuu wa Dodoma, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali, Shirika la Elimu Kibaha, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi na Chuo cha Mipango Dodoma. Zaidi ya udhaifu huo katika utendaji wa vitengo vya ukaguzi, imebainika kuwepo kwa idadi isiyotosha ya watumishi katika vitengo vya ukaguzi wa ndani kuweza kuhimili majukumu yake. Kwa mfano kuwepo kwa mkaguzi mmoja wa ndani katika Chuo cha Mipango Dodoma haitoshi kiutendaji kufanya mapitio yote ya shughuli za chuo. Mashirika mengine ya umma yaliyo na idadi ndogo ya watumishi ni; Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama Shinyanga, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba na Bodi ya Korosho Tanzania. Imebainika pia kuwa, wakaguzi wa ndani wa baadhi ya mashirika ya umma hawana ujuzi wa kutosha kuhusiana na ukaguzi wa mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na hivyo kushindwa kufanya ukaguzi juu ya viashiria hatari vinavyohusu teknolojia ya mawasiliano. Mfano wa mashirika ambayo udhaifu huu umegundulika ni Baraza la Mitihani la Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Madhara ya udhaifu huu ni kushindwa kwa vitengo vya ukaguzi kufikia malengo na hivyo kutoa wigo finyu wa kazi za ukaguzi wa ndani.

9.2 Kuidhinishwa kwa Mpango wa Mwaka wa Ukaguzi

Kiutaratibu, kitengo cha ukaguzi wa ndani, huandaa mpango wa mwaka wa ukaguzi na kuupeleka kwa kamati ya ukaguzi ambao hupelekwa kwenye bodi ya wakurugenzi kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa. Utaratibu huu unashauriwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mpango wa mwaka wa ukaguzi unazingatia maeneo yote ya shirika yanayotia shaka kwa ajili ya kupitiwa na wakaguzi wa ndani. Hata hivyo, uchambuzi

wetu umebaini kuwa mpango wa mwaka wa ukaguzi kwa baadhi ya mashirika ya umma haikuidhinishwa na bodi za wakurugenzi wa shirika husika. Mfano ni Chuo Kikuu cha Mzumbe, mifano mingine ni Mfuko wa Benjamin William Mkapu ambapo kazi ya ukaguzi ilifanywa na mkaguzi mshauri mtaalam. Udhaifu huu pia ulibainika katika Bodi ya Bima za Amana.

9.3 Mapungufu Katika Muundo wa Kamati za Ukaguzi

Ukaguzi juu ya muundo wa kamati za ukaguzi ulibaini kuwa katika baadhi ya mashirika ya umma, wakurugenzi wakuu ni wajumbe na makatibu wa kamati za bodi, ikiwemo kamati ya ukaguzi wa ndani. Msimamo wa wanaotetea utaratibu huu ni kwamba, wakurugenzi wakuu kuwa wajumbe wa bodi ni kwa mujibu wa sheria zilizoanzisha mashirika hayo. Hata hivyo kwa maoni yangu ni kwamba utaratibu huu uko kinyume na kanuni za utawala bora na si vyema kuachwa uendeleo. Mifano ya mashirika ya umma ambayo udhaifu huu ulionekana ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa na Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma.

Zaidi ya hayo, imebainika pia katika baadhi ya mashirika, kamati za ukaguzi zinaundwa na wajumbe kutoka kwenye menejimenti na watendaji waandamizi. Kitendo hiki pia ni kinyume na kanuni za utawala bora ambazo zinahitaji kamati za ukaguzi kuwa kamati ndogo za bodi za wakurugenzi. Mfano halisi ambapo tatizo hili lilionekana ni katika Chuo Kikuu cha Mzumbe.

9.4 Kutoundwa kwa Kamati za Ukaguzi

Kamati ya ukaguzi ni kamati ndogo ya bodi ya wakurugenzi ambayo inayo majukumu ya kuunda taratibu za udhibiti wa ndani wa shirika na kusaidia bodi ya wakurugenzi kuzichambua hesabu za shirika zilizokaguliwa kabla hazijapitishwa na bodi. Katika

mwaka huu wa ukaguzi ilibainika kuwa baadhi ya mashirika ya umma hayakuunda kamati za ukaguzi. Kasoro hii ina athari hasi kwa mashirika haya kwa kukosa mfumo wa kulinda udhibiti wa taasisi husika. Tatizo hili lipo kwenye Mamlaka ya Kuendeleza Biashara Tanzania, Bodi ya Korosho na katika Baraza la Taifa la Kiswahili.

9.5 Mikutano ya Kamati za Ukaguzi

Utawala bora unataka kamati za ukaguzi angalau mara moja kwa kila robo ya mwaka zijadili na kutoa maamuzi kuhusu mambo mbalimbali yahasuyo udhibiti katika mashirika ya umma. Kushindwa kukutana kwa kamati za ukaguzi kunaashiria kutotimizwa kwa wajibu wa kamati hizo. Kaguzi zilizofanyika zimebaini kwamba katika baadhi ya mashirika ya umma mikutano ya kamati za ukaguzi ilikuwa pungufu ikilinganishwa na idadi ya mikutano inayohitajika na sheria zilizoanzisha mashirika hayo ambapo ni kinyume na utawala bora.

Kwa mfano, kamati ya ukaguzi ya Shirika la Magazeti la Taifa ilikutana mara moja tu katika mwaka huo, hivyo kujenga wasiwasi kama kamati hiyo iliweza kutekeleza majukumu yake iliyokasimiwa na bodi ya wakurugenzi. Pia ilibainika, kuwa kamati za ukaguzi za baadhi ya mashirika ya umma hazifanyi mikutano yote. Mifano ya mashirika hayo ni Chuo cha Usimamizi Wanyamapori na Baraza la Kiswahili la Taifa.

9.6 Kutokuwepo kwa Mtaalam wa Fedha Katika Kamati za Ukaguzi

Kama ilivyoelezwa katika ripoti ya mwaka uliopita, baadhi ya kamati za ukaguzi za mashirika ya umma hazina mtaalam wa masula ya fedha au uhasibu ambaye angesaidia kamati kutafsiri masuala ya kitaalam ya uhasibu na masuala ya fedha kwa madhumuni ya kutoa maamuzi yanayojenga kuhusu utendaji wa bodi. Hivyo, inasisitizwa kuwa mashirika ya umma yaunde kamati za ukaguzi ambazo angalau

mjumbe mmoja awe mtaalam wa masuala ya fedha au uhasibu. Kama bodi ya wakurugenzi iliyoundwa haina mjumbe mwenye sifa hizo ni vyema mjumbe huyo atoke nje ya bodi ya wakurugenzi. Pia ni vyema baadhi ya wajumbe wa kamati ya ukaguzi watoke nje ya shirika husika kwani kuna baadhi ya kamati zinaundwa na wakuu wa idara za shirika husika.

9.7 Kuchanganya Majukumu ya Kamati za Ukaguzi na Kamati Nyingine za Bodi

Bodi za wakurugenzi za mashirika ya umma hukasimu majukumu yake kwa kamati zake ndogo ili kuongeza ufanisi kiutendaji. Kwa kufuata utawala bora, huundwa kamati huru za ukaguzi na kamati nyingine kama kamati ya Mipango na Fedha na Kamati ya Uajiri, Uteuzi na Hali bora kwa wafanyakazi, ikiwa ni baadhi ya mifano. Kamati hizi zinapaswa kufanya kazi huru. Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya mashirika ya umma hususan mamlaka za maji zimeunganisha kazi za kamati ya mipango na fedha na kamati ya ukaguzi na kuunda kamati ya mipango, fedha na ukaguzi. Utaratibu huu, unaondoa uhuru wa kamati hizi hasa kamati ya ukaguzi ambayo inapaswa kufanya kazi za usimamizi wa mambo yanayohusiana na ukaguzi katika shirika. Kama kasoro hii haitarekebishwa, itasababisha kushindwa kwa kamati hizi kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mifano ya mashirika ambayo yametekeleza utaratibu huu kinyume na utawala bora ni Mamlaka ya maji safi na maji taka Morogoro na Mamlaka ya maji safi na maji taka Moshi.

9.8 Mamlaka ya Kukagua Hesabu za Mashirika ya Umma na Utoaji wa Hati za Ukaguzi

Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inampa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kukagua hesabu za mashirika ya umma ambayo serikali ina hisa zinazozidi asilimia hamsini 50. Ibara hii imefafanuliwa na sehemu ya 5,9,30 and 33 ya Sheria Na.11 ya Ukaguzi

wa Umma ya mwaka 2008. Licha ya kuwepo kwa sheria hizo, baadhi ya mashirika ya umma yanadai yana haki ya kumteua mkaguzi kwa sababu mbalimbali zikiwemo sheria zilizoanzisha mashirika hayo na makubaliano ya wanahisa wadogo na serikali. Kwa mfano katika kampuni ya simu Tanzania, sehemu ya 12(2) ya sheria iliyoanzisha kampuni ya simu Tanzania inatamka kwamba “kampuni katika mkutano mkuu (AGM) itamteua mkaguzi wa hesabu, kupanga malipo yake na kufuatilia utendaji wake wa kazi kulingana na sheria ya makampuni”. Hii ina maana kwamba ripoti za ukaguzi pia zitasainiwa na mkaguzi aliyeteuliwa na mkutano mkuu. Ni maoni yangu kwamba utaratibu huu unaingilia madaraka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kukagua na kutoa taarifa juu ya hesabu za mashirika ya umma kama ilivyoainishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utawala bora katika Serikali.

9.9 Idadi ya Wajumbe wa Bodi Katika Bodi za Wakurugenzi Iliyo Kinyume na Sheria Zilizoanzisha Mashirika

Idadi ya wajumbe wa bodi katika baadhi ya mashirika ya umma imeelezwa katika Sheria zilizoanzisha mashirika hayo. Ukaguzi ulibaini kwamba idadi ya wajumbe wa bodi katika baadhi ya mashirika ni kubwa kuliko iliyotajwa katika Sheria. Hali hii ina athari hasi kuhusu matumizi ya rasilimali fedha kama vile posho na ada zinazolipwa kwa wajumbe wa bodi. Mapungufu haya yalionekana kwenye baadhi ya mashirika, mojawapo likiwa ni Mamlaka ya Kuendeleza Biashara Tanzania (TANTRADE).

Kwa upande mwingine, imebainika kuwa, baadhi ya bodi za wakurugenzi wa mashirika ya umma wana wajumbe pungufu na mahitaji ya Sheria iliyoanzisha mashirika hayo, kwa mfano sehemu ya 7(1) ya sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini sura ya 413 inatamka kwamba shirika litaongozwa na bodi ya

wakurugenzi yenye wajumbe saba (7). Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa bodi ya wakurugenzi ilikuwa na wajumbe wanne (4) tu. Hali hii yaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya bodi, pia hali hii inaweza kuwa changamoto kwa Mamlaka ya Usafiri wa Nchi Kavu na Majini kushindwa kuendesha vikao pale ambapo mjumbe mmoja au wawili wanapokosekana.

9.10 Bodi za Wakurugenzi Kuingilia Kazi za Menejimenti

Wajumbe wa bodi katika baadhi ya mashirika mbalimbali ya umma wamekuwa wakijihusisha katika utendaji wa kazi za menejimenti. Kitendo hiki ni kasoro kubwa na inapunguza uhuru wa menejimenti kutoka kwa bodi na inaleta migongano ya kimaslahi kati ya pande hizi mbili. Mfano wa kasoro kama hii ilionekana katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo bodi ya wakurugenzi ilijihusisha mara kadhaa katika maonyesho ya kimataifa ya utalii katika kipindi kati ya Julai, 2010 na Juni, 2011. Hali hii ni kinyume na utawala bora na waraka wa Ikulu No. SHC/B.40/6/21 wa tarehe 28/03/1994 aya ya 3 na 5. Utaratibu huu huathiri kazi za bodi za usimamizi kwa kuwa zitakuwa zimegawanyika kimtazamo. Itakapotokea kutotekelezwa majukumu ya kiutendaji yaliyotolewa kwa wajumbe wa bodi, Wajumbe wa Bodi hawatakuwa na nguvu ya kufuatilia na kudai maelezo juu ya kushindwa kufikiwa kwa malengo hayo, na hivyo bodi itabaki kufanya maamuzi yanayolinda maslahi yao katika utendaji wa mamlaka husika.

9.11 Haja ya Kuwa na “Database” ya Wakurugenzi wa Bodi wa Mashirika ya Umma

Ukaguzi ulibaini kuwa bodi kadhaa za wakurugenzi wa mashirika ya umma zilikuwa zimepita muda wake hivyo kuyaacha mashirika hayo kuendesha bila ya kuwa na bodi za wakurugenzi. Hali hii husababisha kutokuwepo kwa utawala wa bodi kwa mashirika hayo ya umma. Kwa mfano kushindwa kupitishwa kwa hesabu zilizokaguliwa na hivyo kuathiri lengo la ofisi yangu la

kutoa ripoti zilizokaguliwa kwa wakati. Mashirika ya umma yasiyo na Bodi za Wakurugenzi yanaonyeshwa kwenye kiambatanisho 'V'.

Kwa kuzingatia kwamba kuisha kwa muda wa bodi za wakurugenzi hutokea katika nyakati/tarehe tofauti, kunaweza kukaleta ugumu kwa mamlaka za uteuzi kufuatilia kwa urahisi uanzishwaji na muda wa bodi hizo. Kwa msingi huo nashauri Msajili wa Hazina aandae "database" ya bodi za wakurugenzi ambayo itakuwa inaonyesha pamoja na mambo mengine tarehe ya kuisha kwa muda wa bodi, na hivyo kuziwezesha mamlaka za uteuzi kuwa na taarifa itakayowezesha kufanya uteuzi wa bodi mpya kwa wakati na hivyo kuwepo kwa mwendelezo wa uwepo wa Bodi za Wakurugenzi.

9.12 Kukosekana kwa Miongozo ya Utendaji wa Bodi

Miongozo ya utendaji wa bodi (charter) ni maandiko yanayowaelekeza wajumbe wa bodi kwenye shirika na mwelekeo wake na ambayo inafanya kazi kama mwongozo wa kiutendaji wa bodi kwa kutoa taarifa juu ya muundo wa bodi na utendaji ikiainisha kazi na majukumu ya wajumbe wa bodi. Pia, inajumuisha miongoni mwa mambo mengine kanuni za maadili ikiwemo sera ya migongano ya kimaslahi, sera ya uhudhuriaji wa vikao vya bodi, mwongozo wa kutathmini kazi za bodi, miongozo ya kutathmini utendaji wa mkurugenzi mkuu, historia za wajumbe wa bodi, kalenda ya bodi na mpango kazi wake. Ukosefu wa mwongozo huu yaweza kueleweka kuwa bodi husika haina mwelekeo.

Hata hivyo, uchambuzi wa shughuli za bodi katika mwaka huu umebaini kuwa baadhi ya mashirika ya umma hayakuandaa mwongozo wa bodi (Board Charter) na hivyo kujiweka katika mashaka ya kukosa mwongozo wa utendaji kazi. Mifano ya mashirika ya umma ambayo yalikosa mwongozo ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

9.13 Uanzishwaji wa Ofisi Huru ya Msajili wa Hazina

Msajili wa Hazina ni mhifadhi na mmiliki wa hisa kwa niaba ya Serikali katika mashirika ya umma na makampuni ambayo Serikali ina hisa. Anahusika kuhakikisha kuwa mashirika ya umma na makampuni ambayo serikali ina hisa yanafikia viwango vya utendaji vilivyokubaliwa. Kutokana na hayo, inaweza kujumuishwa kuwa kazi za Msajili wa Hazina ni kusimamia shughuli za mashirika ya umma ambayo yamo nchini kwa sasa.

Ingawa Msajili wa Hazina amepewa majukumu mbalimabli kama msimamizi wa mashirika ya umma lakini bado ofisi hii inafanya kazi kama Idara chini ya Wizara ya Fedha. Hali hii inaweza kupunguza nguvu za Msajili wa Hazina pia inapingana na kifungu cha 3(1) - (2) cha Sura ya 418 ya Sheria ya Msajili wa Hazina kuhusu nguvu na kazi za Msajili wa Hazina kinachoeleza kwamba; “Sheria hii itakapoanza kutumika, kutakuwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Atakayeteuliwa na Rais kuwa Msajili wa Hazina atakuwa mhimili wa ofisi kwa jina la Msajili wa Hazina na kwa jina hilo atakuwa na “perpetual succession” na muhuri rasmi (official seal) mwenye uwezo na mamlaka ya kununua, kuhifadhi, kusimamia na kuuza uwekezaji, kushitaki na kushitakiwa, kutekeleza uwekezaji (deeds and instruments), kuingia mikataba yeye mwenyewe na warithi wake wa ofisi, kutekeleza haki zote, alizopewa na uwekezaji yakiwemo madaraka ya kuhodhi mali zisizohamishika na mali nyinginezo, na kufanya mambo yeyote ya lazima kwa ajili ya kurahisisha na yatakayofanywa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake au ambayo yanahitajika kufanywa na Msajili wa Hazina kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyinginezo”.

Muundo wa sasa wa Ofisi ya Msajili wa Hazina na uwepo wake kama Idara chini ya Wizara ya Fedha inapinga malengo yaliyowekwa na sheria iliyonukuliwa hapo juu.

Pia, ingawa Msajili wa Hazina, kapewa majukumu ya usimamizi wa mashirika ya umma, imebainika kuwa, Msajili wa Hazina na Maafisa wake wamekuwa wakiteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika baadhi ya mashirika ya umma. Hii inaweza kusababisha migongano ya kimaslahi kati ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma ambayo maafisa wa msajili ni wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika kazi ya kiusimamizi.

9.14 Taasisi ya Wakurugenzi na Bodi za Wakurugenzi

Watu binafsi wenye kupenda utawala bora na wenye nia ya dhati juu ya taaluma ya ukurugenzi unaofuata utawala bora, hivi karibuni wameunda taasisi ya wakurugenzi nchini kama kampuni yenye ukomo wa dhamana. Baadhi ya malengo ya taasisi ya wakurugenzi ni;

Taasisi ina nia ya kuwa na sauti itakayoongoza kwenye masuala ya utawala bora ikiwa na wigo wa ubunifu na mawasiliano ulioundwa kuinua kiwango cha utawala bora Tanzania. Itatoa mapendekezo kwa Serikali na vyombo vya udhibiti juu ya mambo yanayoathiri utawala wa mashirika hapa Tanzania. Taasisi hii itasaidia pia kuinua viwango vya utawala kupitia maendeleo ya taaluma ya ukurugenzi na watumishi wengine, kutoa muongozo wa kanuni za utawala bora, taratibu za kiutendaji, nidhamu kwa wanachama wake na kusaidia makampuni ambayo yako katika hatua za kuanzishwa kueleza na kutumia utawala bora katika shughuli zao.

Kwa ujumla, taasisi inatarajia kutoa mwelekeo, mafunzo, huduma za kiushauri kwa wanachama wake na kuongoza na kufadhili utafiti juu ya ukurugenzi wa mashirika na juu ya masuala ya kiutawala.

Hata hivyo, taasisi iko katika hali ya uchanga na hivyo mambo muhimu yahasuyo uendeshaji wake kama kujenga uwezo, uandaaji wa miongozo ya uendeshaji na uandaaji wa kanuni za maadili za wajumbe wa bodi hayajatekelezwa.

SURA YA KUMI

VITEGA UCHUMI VYA SERIKALI, MAENDELEO YA UBINAFSISHAJI NA UFUATILIAJI WA TATHMINI YA MASHIRIKA YALIYOBINAFSISHWA

10.0 Utangulizi

Sura hii inatoa mwanga juu ya masuala yanayohusiana na Vitega Uchumi na maslahi mbali mbali ya Serikali katika mashirika na makampuni ambayo Serikali inamiliki hisa chini ya asilimia 50 na yale ambayo serikali inamiliki hisa zaidi ya asilimia 50. Pamoja na maendeleo ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma, pia huonyesha matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ya yale yaliyokwisha binafsishwa. Masuala yanayohusiana na vitega uchumi vya Serikali katika ripoti hii, yametolewa katika taarifa ya Msajili wa Hazina kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011.

Kwa upande mwingine masuala yanayohusiana na mchakato wa ubinafsishaji wa taasisi zilizotengwa kwa ajili ya ubinafsishaji, ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa kwa mwaka ulioishia Disemba 31, 2011, yametokana na taarifa ya ubinafsishaji na ripoti ya ufuatiliaji na tathmini ya mashirika yaliyokwisha binafsishwa. Sura hii imegawanywa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu hali ya vitega uchumi vya Serikali, sehemu ya pili inahusu masuala yanayohusiana na maendeleo ya ubinafsishaji wa mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa. Zaidi ya hayo, kuna matokeo yanayohusu ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa.

10.1 Vitega Uchumi na Maslahi Mengine ya Serikali

Kama ilivyokuwa mwaka 2009/2010, kwa mwaka 2010/11, uwekezaji kwenye vitega uchumi mbalimbali vya serikali siyo mzuri. Mambo yaliyochangia kutokufanya vizuri ni pamoja na urasimu katika sera ya mwongozo na ushauri wa kisheria wa Wizara husika, udhaifu wa mifumo ya kisheria na udhibiti wa shughuli za kiutendaji za Mashirika ya Umma, usimamizi dhaifu wa ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara na Bodi za Wakurugenzi kukosa uwezo wa kutekeleza majukumu yao kama vyombo vya kusimamia mashirika ya umma, ukosefu wa utamaduni wa ujasiriamali katika mashirika, na menejimenti zisizo na uwezo na ukosefu wa taaluma.

Mambo mengine yaliyochangia kutokufanya vizuri ni pamoja na miundo ya uongozi wa mashirika ya umma, michakato na mifumo iliyowekwa bila malengo. Kukosekana ufanisi kwenye mipango na bajeti, usimamizi wa fedha mbovu kutokana na ukosefu wa wafanyakazi wenye uwezo, ukosefu wa uwajibikaji, uwazi, njia mbaya katika michakato na taratibu za manunuzi, usimamizi mbaya wa rasilimali na mitaji midogo.

Utendaji kazi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ulihusisha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na madeni ambayo serikali imewawekea dhamana wakopaji, mapato yaliyo kusanywa na Msajili wa Hazina kama gawio, makusanyo kutokana na malipo ya mikopo na mapato mengine na malimbikizo ya maduhuli.

10.2. Vitega Uchumi vya Serikali

10.2.1. Vitega Uchumi Katika Taasisi za Ndani

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011, Serikali ilikuwa inahodhi hisa na fedha kwa kiasi cha Shilingi trilioni 10.3 kwenye Mashirika ya Umma 204 na Taasisi

Nyinginezo ambazo ziliwasilisha Hesabu zilizokaguliwa kwa Msajili wa Hazina. Uwekezaji huu umepanda ikilinganishwa na Shilingi trillion 7.7 kama ilivyokuwa tarehe 30 Juni 2010. Hii ni kutokana na Mashirika mengi ambayo yaliwasilisha hesabu zao zilizokaguliwa ambazo zinaonyesha thamani ya sasa ya fedha za hisa, mtaji na fedha za wabia wengine. Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2011, Taasisi 11 hazikuweza kuwasilisha hesabu zao zilizokaguliwa ikilinganishwa na mashirika 18 yaliyoripotiwa mwaka uliopita.

10.2.2 Uwekezaji Katika Mashirika ya Nje

Serikali ilikuwa inahodhi uwekezaji wenye thamani ya Shilingi bilioni 157.7 katika mashirika tisa nje ya nchi hadi tarehe 30 Juni, 2011 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 113.6 kwa mwaka uliopita sawa na asilimia 39. Umiliki wa hisa za Serikali katika Taasisi za Nje ulibaki kuwa sawa katika taasisi zote. Hata hivyo, thamani ya uwekezaji imeongezeka kutokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Kitanzania.

10.3. Mapato ya Serikali Kutoka Gawio, Mikopo na Sehemu Nyingine

Mapato yaliyokusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kutokana na gawio, urejeshaji wa mikopo na mapato mengine kutoka kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo hadi tarehe 30 Juni, 2011, yalipungua kwa Shilingi bilioni 11.86 sawa na asilimia 29.2 kutoka Shilingi bilioni 28.7 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 40.6 zilizokusanywa kwa mwaka 2009/2010. Hata hivyo, bajeti iliyopangwa kwa ajili ya mwaka huu ilikuwa Shilingi bilioni 51.5 ikiwa pungufu kwa asilimia 27. Upungufu huu ulisababishwa na sababu zifuatazo:-
(a) kupungua kwa "Mapato mengine" kwenye Hazina ya Serikali kwa Shilingi bilioni 7.4 sawa na asilimia 52.6, kutoka kiasi kilicholipwa cha Shilingi bilion 14.1 kwa mwaka 2009/2010 hadi kiasi cha Shilingi bilioni 6.7 kilicholipwa kwa mwaka 2010/2011. (b) kupungua kwa


mapato yatokanayo na mkopo na riba kwa Shilingi bilioni 9.1 sawa na asilimia 79.5, kutoka Shilingi bilioni 11.4 kwa mwaka 2009/2010 hadi Shilingi bilioni 2.3 kwa mwaka 2010/2011 (c). Hata hivyo, kiasi cha gawio kwa mwaka 2010/2011 kiliongezeka kwa shilingi bilioni 4.67 sawa na asilimia 30.9 kutoka Shilingi bilioni 15.1 zilizolipwa kwa mwaka 2008/2009 hadi Shilingi bilioni 19.8 zilizolipwa kwa mwaka 2010/2011. Kwa muhtasari, mapato yaliyokusanywa kutokana na gawio, ulipaji wa mkopo, na mapato mengine yaliyotokana na uuzaji wa hisa yalikuwa kama ifuatavyo:-

Jedwali Na.10: Mwenendo wa Mapato ya Serikali Kutokana na Gawio, Ulipaji Mikopo na Mapato Mengine.

	2007/08 Tarakimu ktk bilioni	2008/09 Tarakimu katika bilioni	2009/2010 Tarakimu katika bilioni	2010/2011 Tarakimu ktk bilioni
Gawio	57.1	31.3	15.1	19.8
Mkopo& Riba	11.5	6.7	11.4	2.3
Mapato mengine	8.3	46.1	14.1	6.7
Jumla	76.9	84.1	40.6	28.7

Mwenendo wa Mapato ya Serikali Kutokana na Gawio, Ulipaji Mikopo na Mapato Mengine unaweza kuonyeshwa kwenye histogram kama ifuatavyo:.

Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa Mapato ya Serikali kutokana na gawio, ulipaji Mikopo na Mapato mengine, kwa kipindi cha miaka ya (2007/08, 2008/09, 2009/10, 2010/11)



Kuna malimbikizo ya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 101.6 ambayo Shilingi bilioni 98.3 zilitokana na malimbikizo ya mkopo ambao ulitakiwa kuwa umeshakusanywa. Sababu za malimbikizo hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mashirika ambayo hayafanyi vizuri kiutendaji na sasa yako mufilisi kupitia CHC, na inatarajiwa kwamba, mapato yatakayotokana na kuyafilisi mashirika haya, ndiyo yatakayotumika kulipia mkopo husika.
- (ii) Mashirika ya Umma kama TANESCO na TRC (sasa Reli Assets Holding Corporation (RAHCO)) yana matatizo kifedha hivyo basi kuwa vigumu kurejesha mikopo yao.

10.4. Mchakato wa Ubinafsishaji, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mashirika Yaliyokwisha Binafsishwa

Serikali ilianzisha Sera ya Ubinafsishaji mwaka 1992 iliyolenga makampuni karibu 360 kwa lengo la kuiondoa serikali kwenye umiliki na shughuli za kuendesha biashara, kwa kuruhusu sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi. Chini ya sera hii, lengo la serikali lilikuwa ni kuhakikisha utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi, utawala bora na utunzaji wa sheria na uzingatiaji wa taratibu zilizowekwa. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2008, jumla ya Mashirika 336 yalikuwa yameshabinafsishwa. Aina ya ubinafsishaji ilikuwa ni pamoja na mauzo ya hisa zote za Serikali, mauzo ya sehemu ya hisa, ukodishaji, na mikataba ya usimamizi, na uuzaji wa shughuli zisizo za kibiashara/mali kwa wawekezaji binafsi. Kati ya mashirika 336 ambayo ubinafsishaji wake ulikamilika. Mashirika 180 yameuzwa kwa 100% kwa Watanzania, mashirika 27 yameuzwa kwa 100% kwa wawekezaji wa kigeni, wakati mashirika 129 yaliyobaki yanaendeshwa kwa ubia wa pamoja kati ya Serikali na wawekezaji binafsi wa ndani na nje.

Serikali ililipa mamlaka Shirika Hodhi la mali za Serikali kusimamia mchakato wa ubinafsishaji na baada ya ubinafsishaji, ufuatiliaji na tathmini ya makampuni yote yaliyobinafsishwa kuanzia Januari 1, 2008. Hii ni kwa mujibu wa Sheria Namba 16 ya 2007 ya Benki ya Taifa ya Biashara.

Sehemu inayofuata, inaeleza mambo muhimu yatokanayo na taarifa ya maendeleo ya mchakato wa ubinafsishaji wa mashirika yaliyosalia kwa ajili ya kubinafsishwa, na taarifa ya ufuatiliaji na Tathmini ya Mashirika yaliyobinafsishwa hadi tarehe 31 Disemba, 2011.

10.5. Taarifa ya Ubinafsishaji wa Mashirika Yaliyosalia kwa Ajili ya Kubinafsishwa, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mashirika Yaliyobinafsishwa

Katika mwaka 2011, Kurugenzi ya ubinafsishaji, pamoja na Wizara ya Fedha zilifanya ufuatiliaji na tathmini ya mashirika 69 yaliyobinafsishwa ili kujua utendaji wa kila chombo / kitengo dhidi ya viwango vilivyowekwa.

Kati ya mashirika 69 yaliyotathminiwa, 6 yalikuwa yanafanya vizuri na kuzalisha faida, 33 yalikuwa yanapata hasara kutokana na sababu mbalimbali kama vile gharama kubwa za uendeshaji, gharama za juu za ukarabati, mashine duni na ushindani mkubwa kutoka kwa makampuni mengine binafsi katika sekta husika. Mashirika 30 yamefungwa kutokana na usimamizi duni, uchakavu wa baadhi ya mashine za viwanda, mpango duni na ukosefu wa maelezo ya uwekezaji uliofanyika na kwa hiyo wanaendelea kupata hasara kila mwaka na hatimaye kufungwa. Sababu zingine zilikuwa ni madeni makubwa, kushindwa kupata masoko mazuri na kukosekana kwa umeme wa kutosha, kuchelewa kutimiza masharti kama yalivyo kwenye makubaliano ya kuuziana (kama vile kuchelewa kukabidhi hati za umiliki), na gharama kubwa za uendeshaji kama vile umeme na malighafi. Matatizo haya yanapelekea baadhi ya bidhaa zinazozalishwa kutoweza kushindana sokoni. Matatizo mengine ni migogoro kati ya wanahisa na idadi kubwa ya kesi zilizopo mahakamani.

10.6. Changamoto Zilizojitokeza Wakati wa Ufuatiliaji wa Kutathmini Mashirika Yaliyobinafsishwa

Shirika Hodhi la Mali za Serikali lilikabiliwa na changamoto mbalimbali, wakati wa kutekeleza zoezi hili, changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

- Kukosekana kwa taarifa muhimu na za msingi kwenye baadhi ya mashirika,

- Baadhi ya wawekezaji kusita kutoa habari na taarifa kama vile taarifa za kifedha,
- Ukosefu wa Mikataba kati ya Serikali/PSRC na wawekezaji,
- Baadhi ya Mikataba ya mauzo haikuwa na Mipango ya uwekezaji hivyo ilikuwa ni vigumu kutathmini utendaji wa mwekezaji.
- Baadhi ya mipango ya uwekezaji haiko wazi na haionyeshi muda kwa ajili ya shughuli mbalimbali,
- Kulikuwa na matatizo ya mawasiliano na wawekezaji kutokana na ukweli kwamba baadhi yao wamebadili biashara, majina ya maeneo, na anwani zao.

10.7. Mashirika Yaliyotengwa kwa Ajili ya Kubinafsishwa
 Kati ya malengo ambayo hayajatekelezwa hadi wakati wa kuandika ripoti hii Marchi 2012 ni kuhusu mashirika 34 ambayo bado yanasubiri kubinafsishwa. Hadi sasa idadi imebakia kuwa hiyo hiyo. Hata hivyo, shirika linapokuwa limetengwa kwa ajili ya kubinafsishwa, kwa kawaida huwa haliwezi kufanya upanuzi wowote wa kibiashara, kwa sababu huwa haliwezi kuandaa na kutekeleza mipango mikakati yeyote. Vile vile shirika husika huwa haliwezi kukopa kutoka benki, au kuwekeza n.k. Zaidi ya hayo, wafanyakazi wa mashirika yaliyo tengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji wanakuwa katika hali ya kukosa ari ya kutekeleza wajibu wao na kukata tamaa. Mali za mashirika yaliyo tengwa kwa ajili ya ubinafsishaji huwa zinakuwa chakavu kwa sababu hazifanyiwi ukarabati kutokana na uhaba wa fedha. Serikali inapaswa kufikiria ama kusimamia mchakato wa ubinafsishaji wa mashirika ya umma ili kuepusha kuchakaa zaidi kwa mali zinazomilikiwa na mashirika hayo, au maamuzi ya kutoyauza yafanywe ili serikali iendelee kuyapa fedha kwa ajili ya kuyafufua upya. Mashirika ambayo yameendelea kutengwa kwa ajili ya ubinafsishaji ni kama yalivyoorodheshwa kwenye kiambatanisho Na.IV.

SURA YA KUMI NA MOJA
MATOKEO YA KAGUZI MAALUM

11.0. Utangulizi

Kifungu cha 29 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum kufuatia maombi ya mtu, taasisi, wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa au mashirika ya umma.

Kwa msingi huo katika mwaka huu wa fedha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya jumla ya kaguzi maalum tisa (9) katika Mashirika ya Umma. Mashirika ya Umma ambayo kaguzi hizi maalum zilifanyika ni Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC), Chuo cha Ubaharia cha Dar es Salaam (DMI), Bohari Kuu ya Madawa (MSD), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE), Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA), Shirika la Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) na malipo yaliyofanywa kwa IPTL.

Ukaguzi Maalum wa Chuo Kikuu cha Dodoma ulihusu mifumo ya mishahara ya watumishi wa Chuo na matokeo ya ukaguzi huo yameainishwa katika sura ya nne (4) ya ripoti hii. Matokeo ya kaguzi maalum za Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) na malipo yaliyofanywa IPTL hayakuweza kuainishwa katika ripoti hii kwa sababu kaguzi hizo zilikuwa bado hazijakamilika, kwa hiyo matokeo hayo yataainishwa kwenye ripoti ijayo.

Matokeo ya kaguzi maalum yameainishwa kwenye ripoti hii kwa muhtasari tu, kwa hiyo matokeo ya kina yanapatikana katika ripoti husika. Yafuatayo ni

matokeo ya kaguzi maalum zilizofanyika na kukamilika katika kipindi cha taarifa hii:-

11.1. Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC)

Ukaguzi Maalum ulifanyika kufuatia maombi ya Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika Hodhi la Rasilimali za Umma (CHC) ili kujua kama kuna matumizi mabaya ya mali za Shirika au ubadhirifu unaofanywa na uongozi wa Shirika la CHC. Mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi wa Shirika Hodhi la mali za Serikali ni kama ifuatavyo:-

11.1.1. Mapungufu Katika Uuzwaji wa Kiwanja Na.10 Kando Kando ya Barabara ya Nyerere

Kulikuwa na mapungufu ya kutokuzingatia kanuni za utawala bora, ambapo maamuzi makubwa yahasuyo Shirika yalifanywa na Wizara ya Fedha badala ya Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la CHC. Maamuzi hayo hayakuzingatia vithibitisho na wala hayakufanyika kwa upembuzi yakinifu wa kuzingatia ushauri wa kisheria.

Mawasiliano yaliyokuwa yakifanyika kati ya Shirika la CHC, Kampuni ya Mohamed Enterprises Tanzania Ltd (METL), na Wizara ya Fedha yalionyesha majadiliano, maamuzi na miongozo ya kuuza kiwanja Na.10 kilichopo barabara ya Nyerere. Mawasiliano hayo yalionyesha wazi kuwa Wizara ya Fedha ilihusika katika uuzwaji wa kiwanja hicho kwa kutoa maagizo kwa uongozi wa Shirika kukiua bila kuishirikisha Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika hilo.

Kwa kuzingatia maagizo hayo, Kiwanja hicho kiliuzwa kwa Kampuni ya Mohamed Enterprises (T) Ltd kwa kiasi cha Shilingi bilioni 2.1 bila kuzingatia kanuni za utawala bora wala Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.

11.1.2. Kuwepo kwa Madai Yenye Utata ya Tozo la Matumizi ya Barabara na Gharama za Ulinzi kwa Ajili ya Kuingia Kwenye Kiwanja Na.192 Kilichopo Kando Kando ya Barabara ya Nyerere

Hati ya Madai ya Shilingi milioni 954.7 ikijumuisha kodi, ilitolewa na kampuni ya DRTC Trading Company (DRTC) ikiwa ni madai ya matumizi ya barabara na gharama za ulinzi za kuingia kwenye kiwanja Na.192 kilichopo kando kando ya barabara ya Nyerere. Licha ya kutolewa kwa hati hiyo ya malipo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezesaji aliandika barua kwa Mwenyekiti wa iliyokuwa “Presidential Parastatal Sector Reform (PSRC)” (Shirika lililokuwa linasimamia mali za Serikali kabla ya CHC), akimtaka kutekeleza ulipaji wa madai hayo ya DRTC. Baadaye Meneja Mkuu wa kampuni ya DRTC aliandika barua nyingine kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CHC akimtaka kulipa mara moja kiasi cha Shilingi bilioni 2.4 kwa DRTC; Barua hiyo pia iliainisha kuwa ni kutekeleza maagizo yaliyotoka Serikalini ya kulipa kiasi hicho cha fedha, kiasi ambacho kilikuwa kikubwa ikilinganishwa na hati ya madai iliyotolewa mwanzoni na DRTC ya Shilingi milioni 954.72.

11.1.3. Mapungufu Yaliyoonekana Katika Uuzwaji wa Jengo la Iliyokuwa Kampuni ya Kukarabati Magari Tanzania (Tanzania Motor Service Company TMC) Lilipo Kiwanja Na.24 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

Jengo la TMSK lililopo kiwanja Na.24 katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi liliuzwa kwa Saddiq Super Service Station (SSSS) kwa kiasi cha Shilingi Bilioni 1.3 na CHC. Malipo ya awali ya asilimia 10, sawa na Shilingi milioni 130 yalilipwa na kampuni ya SSSS kwa CHC.

Baadaye Wizara ya Fedha iliitaarifu CHC juu ya maamuzi ya Serikali ya kusitisha uuzwaji wa jengo hilo. Wizara ya Fedha pia ikatoa maagizo kwa CHC kuanza mazungumzo na kampuni ya SSSS ili kukubaliana kuhusu malipo ya fidia kwa usumbufu uliojitokeza kwa kampuni ya SSSS, sababu ikiwa kampuni ya SSSS ilishalipa asilimia 10 kama malipo ya awali. Kampuni ya SSSS iliwasilisha madai ya kiasi cha Shilingi bilioni 3.8 kama madai ya fidia, pamoja na Shilingi milioni 500 kama malipo ya usumbufu.

Baadaye iliamuliwa kuwa kampuni ya SSSS ilipwe kiasi cha Shilingi milioni 964.1 kiasi kilichojumuisha Shilingi milioni 130 kama fidia ya malipo ya awali yaliyofanywa na SSSS, malipo ya riba na malipo kwa ajili ya usumbufu. Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha alikuwa ndiye mwenyekiti wa kikao kilichopitisha malipo hayo ambayo aliyawasilisha kwa Waziri wa Fedha kwa ajili ya kupata kibali cha malipo ambayo yeye alishiriki kwenye maamuzi. Kiasi cha jumla ya Shilingi milioni 964.1 kililipwa moja kwa moja kwa kampuni ya SSSS kutoka Wizara ya Fedha bila kupitia CHC. Hali hii ya maamuzi inaleta shaka, uwalakini juu ya malipo hayo na malengo ya Wizara ya Fedha kulipa kiasi hicho cha fedha bila kushirikisha Shirika la CHC wala Bodi yake ya Wakurugenzi.

11.1.4. Kesi Baina ya Tantrack na TMSC

Kampuni ya Wakala Tantrack ilikodisha jengo la TMSC lililopo kiwanja Na.24 katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi kwa mkataba wa pango wa miaka miwili kuanzia tarehe 1 Julai 1993. Kampuni ya Tantrack iliingia gharama za ukarabati wa jengo hilo kwa kiasi cha Shilingi milioni 24 kinyume na makubaliano ya mkataba, na kampuni hiyo ikakataa kulipa kodi ya pango kwa madai kwamba gharama hizo zihesabike kama malipo ya kodi.

Kampuni ya Tantrack ilifungua kesi Na.257/1995 katika mahakama ya makazi ya Mkoa wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Regional Housing Tribunal - RHT) dhidi ya TMC kwa madai kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa mkataba wa pango baada ya kupewa notisi ya miezi sita ya kuvunja mkataba baada ya kukataa kulipa kodi ya pango. Kesi iliendelea kwa muda bila kuwepo kwa maamuzi yaliyokubalika na kutekelezwa.

Baadaye iliamuriwa na mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuwa jengo liuzwe kwa njia ya mnada kwa kampuni ya Africa Terminals Ltd (ATL) kwa kiasi cha Shilingi bilioni 3; CHC hawakuridhika kwa namna ambavyo mnada uliendeshwa kwa madai kuwa taratibu za sheria hazikufuatwa, hiyo kuwasilisha hati ya makubaliano na Tantrack (Deed of Settlement) ili mahakama iweze kutoa kibali cha makubaliano kati ya CHC na Tantrack; Kwa bahati mbaya kabla ya mahakama haijatoa kibali, Kampuni ya African Terminal Ltd (kampuni iliyonunua jengo la TMC kwa njia ya mnada) iliwasilisha pingamizi mahakamani kuzuia kupitishwa kwa hati ya makubaliano kati ya CHC na Tantrack. Kesi hii bado inaendelea hadi sasa ni miaka 15 ambapo inaonyesha wazi kwamba kumekuwepo na kutowajibika kwa pande zote zinazohusika ili kumaliza kesi hiyo.

11.1.5. Kutokuwepo Kwa Umakini wa Kutosha Kwenye Uuzaji wa Kiwanja Na. 33 Kilichopo Barabara ya Saza Eneo la Viwanda Chang'ombe kwa Kampuni ya Maungu Seed

PSRC iliingia mkataba wa mauzo ya Kiwanja Na.33 na Kampuni ya Maungu Seed tarehe 1/9/2004 kwa makubaliano ya Shilingi milioni 620 zitakazolipwa kwa awamu tatu. Kiwanja hiki kipo barabara ya Saza eneo la Viwanda Chang'ombe Dar es Salaam. Kiasi cha Shilingi milioni 200 kililipwa na Kampuni ya Maungu Seed pamoja na dhamana ya benki (Bank guarantee)

kutoka benki ya Rasilimali (TIB) ya Shilingi milioni 420. Ilikubalika pia kwamba PSRC itakabidhi mali hiyo kwa Maungu ndani ya miezi mitatu baada ya kusaini mkataba wa mauzo na hati zote kuwasilishwa kwa Maungu baada ya kulipa salio la mwisho. PSRC ilishindwa kukamilisha kukabidhi mali hiyo ndani ya muda wa makubaliano kwa sababu mali hiyo ilikuwa imewekwa rehani kwenye kampuni ya CDC London (UK) tangu mwaka 1959. Baadaye rehani (bond) ya mali hiyo iliachiliwa na kampuni hiyo ya Uingereza tarehe 26 Aprili 2006 na kwa wakati huo dhamana ya benki iliyokuwa imewekwa na Maungu ilishaisha muda wake, kwa hiyo kiasi cha malipo ya Shilingi milioni 420 yakawa bado hayajalipwa.

Mwaka 2010, Kampuni ya Maungu ilifungua kesi mahakamani na ikaamriwa PSRC iwasilishe kwa kampuni ya Maungu Seed hati miliki Na.6639 na PSRC iilipe kampuni ya Maungu kiasi cha Shilingi milioni 200 mara moja bila kuchelewa.

Kulipwa kwa Shilingi milioni 200 kwa kampuni ya Maungu yalikuwa ni sawa na malipo ya awali yaliyofanywa na kampuni ya Maungu. Hii ni wazi kwamba Kampuni ya Maungu Seed ilipata kiwanja hicho bure bila kulipa kiasi chochote cha fedha.

11.1.6. Kufutwa kwa Madeni

CHC ilirithi madeni mbali mbali kutoka kwa iliyokuwa kampuni ya SIMU 2000 na kutoka PSRC.

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa taratibu madhubuti za makabidhiano ya shughuli za iliyokuwa SIMU 2000 Limited na iliyokuwa PSRC na CHC. Mapungufu hayo yalipelekea kufutwa kwa madeni yaliyorithiwa na Shirika la CHC ambayo Shirika halikuweza kupata vithibitisho vya kuwepo kwa kiasi cha madeni hayo. Hata hivyo hakuna vithibitisho vilivyoonyesha kuwa

CHC ilifanya jitihada za kupata uhalisia na usahihi wa madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa walioshindwa kuonyesha ushirikiano.

Iliyokuwa SIMU 2000 Limited ilikuwa na jumla ya madeni ya Shilingi milioni 326 ikiwa ni salio chanya na kiasi cha Shilingi milioni 77.1 ya madeni yenye salio hasi ambayo yalifutwa na shirika Hodhi la Rasilimali za Umma.

11.2. Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI)

Ukaguzi maalum wa Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI) ulifanyika kufuatia barua iliyopokelewa tarehe 3 Juni 2011 iliyoomba kufanyike ukaguzi huo. Kufuatia kufanyika kwa ukaguzi huo Maalum wa DMI mapungufu yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo:-

11.2.1. Malipo ya Honoraria, na Posho Nyingine Bila Kibali cha Baraza la Ushauri la Chuo ya Jumla ya Shilingi Milioni 83.8

Ukaguzi maalum ulibaini kuwepo kwa malipo ya kiasi cha Shilingi milioni 12.1 zilizolipwa kwa maafisa wa Wizara ya Mawasiliano, Shilingi milioni 51.8 zililipwa kwa mwenyekiti wa baraza la Ushauri la Chuo zikiwa ni malipo ya posho za honoraria, posho za mafuta na malipo ya posho za kila mwezi. Pia Shilingi milioni 2.6 zililipwa kama posho za vikao kwa watumishi wa Idara ya uhasibu wa DMI bila kuhudhuria vikao husika. Shilingi milioni 10.4 zililipwa kwa watumishi wa DMI kama posho za zoezi maalum la kikosi kazi (Task force) kilichoundwa kwa ajili ya kuhuisha mtaala wa chuo, zoezi lililofanyika mwezi Juni, 2009 lakini watumishi hao walilipwa bila kuwepo katika kikosi kazi hicho na hawakushiriki kuifanya kazi hiyo. Iligundulika pia kuwepo malipo ya Shilingi milioni 6.9 yaliyolipwa kama posho kwa wajumbe mbalimbali na watumishi wa chuo kwa kutumia viwango ambavyo havijapata kibali cha

Baraza la Ushauri la Chuo na pia kulipwa kwa watumishi ambao hawakushiriki katika mkutano wa maandalizi ya mahafali ya 7 ya chuo hicho uliofanyika kati ya tarehe 9 Machi 2011 na tarehe 11 Machi 2011.

Malipo hayo yote ya posho yaliyotajwa yalikuwa kinyume na sheria za fedha za Chuo za mwaka 2008, na zililipwa bila kupata kibali cha baraza la Ushauri la Chuo.

11.2.2. Mapungufu Yaliyoonekana Katika Matumizi ya Shilingi Milioni 385.1 Zilizotolewa na Wizara kwa Ajili ya Kulipa Madeni ya Chuo

Chuo cha DMI kilipokea jumla ya Shilingi milioni 385.1 kutoka Wizara ya Mawasiliano kwa ajili ya malipo ya madeni ya Chuo. Ukaguzi maalum ulibaini kuwa kati ya fedha hizo ni kiasi cha Shilingi milioni 205.8 tu ndicho kilitumika kulipa madeni ya Chuo na kiasi kilichobaki cha Shilingi milioni 179.3 hakikutumika kulipa madeni bali fedha hizo zilitumika katika matumizi ya kawaida ya Chuo kinyume na maagizo ya matumizi ya fedha hizo.

11.2.3. Malipo ya Mishahara kwa Watumishi wa Chuo kwa Kutumia Viwango vya Mishahara Ambavyo Havijapitishwa na Baraza la Ushauri la Chuo

Chuo kinawalipa watumishi 12 mishahara kwa kutumia ngazi ya mshahara PGSS 5 au zaidi bila ya kupata kibali cha Baraza la Ushauri la Chuo. Hata hivyo, haikuweza kubainika ni lini watumishi hao walipandishwa kwenye ngazi hiyo ya mshahara ili kuweza kufanya tathmini ni kiasi gani cha mishahara kimeshalipwa kwa kila mtumishi kinyume na taratibu.

Ukaguzi maalum pia ulibaini kuwa, ngazi ya mshahara anaolipwa Mkurugenzi wa Fedha na Utawala ya PHTS si sahihi kwani ngazi hiyo ya mshahara inahusu wakufunzi wa Chuo (Lecturers). Ngazi ya mshahara anayostahili

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala ni PGSS. Sababu na namna mshahara wa Mkurugenzi wa Fedha ulivyobadilishwa kuwekwa kwenye ngazi hiyo kinyume cha sheria na bila kibali cha Baraza la Ushauri la Chuo hazikuweza kufahamika. Kwa mantiki hiyo, Mkurugenzi wa Fedha na Utawala ameshalipwa jumla ya Shilingi milioni 16.2 katika kipindi cha kuanzia Julai, 2009 hadi Januari, 2012 ikiwa ni kiasi kilichozidi mshahara wake stahiki.

11.2.4. Kuibiwa kwa Vifaa vya Kompyuta Katika Maabara ya Chuo na Kutokupokelewa kwa Kompyuta Zilizotolewa kwa Chuo kama Msaada

Ukaguzi Maalum ulibaini kuwa kuna Kompyuta 25 zilizotolewa kama msaada kwa Chuo kutoka Chuo Kikuu cha Leeds Metropolitan cha Uingereza kwa ajili ya maabara ya Chuo. Chuo kililipa kiasi cha Shilingi milioni 3.4 tarehe 7 Disemba 2007 kwa Kampuni ya M/s Meshade Ltd kama gharama za kuondoa mzigo bandarini, lakini Kompyuta hizo bado hazijapokelewa chuoni hapo hadi wakati tunamaliza ukaguzi huu Februari, 2012.

Ilibainika pia, kati ya Kompyuta 13 zilizopo katika maabara ya Chuo, ni Kompyuta nne (4) tu ndizo ambazo zingeweza kutengenezwa na kufanya kazi. Hivyo Kompyuta tisa (9) haziwezi kufanya kazi kutokana na kuibwa baadhi ya vifaa vyake ambavyo viliibiwa na mtumishi aliyeajiriwa kwa muda mfupi (temporary employee) na Chuo hicho. Vifaa vilivyoibwa ni pamoja na Ram, Processors, Hard Disks, Power supply na Mother Boards.

11.3. Bohari ya Madawa (MSD)

Ukaguzi Maalum wa Bohari ya Madawa (MSD) ulifanyika ili kubaini tatizo la upatikanaji wa madawa katika Bohari ya Madawa (MSD), katika kipindi cha miaka miwili kuanzia tarehe 1/7/2009 hadi tarehe

30/6/2011. Mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi huo maalum uliofanyika katika Bohari ya Madawa yalikuwa kama ifuatavyo:-

11.3.1. Bajeti ya Serikali kwa Ajili ya Madawa Katika Kipindi cha Miaka ya Fedha ya 2009/2010 na 2010/2011

Ukaguzi ulibaini kuwa bajeti ya Serikali kwa ajili ya manunuzi ya madawa ilipungua katika kipindi cha miaka miwili 2009/2010 na 2010/2011. Ilionekana kwamba, mchango wa Serikali katika ununuzi wa madawa ulipungua kwa kipindi chote cha miaka miwili ukilinganishwa na ule wa Mfuko wa fedha za Afya (Health Busket Fund). Mfuko wa fedha za afya ulipanga kutoa jumla ya Shilingi bilioni 83.5 katika kipindi cha miaka yote miwili wakati Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilipanga kiasi cha jumla ya Shilingi bilioni 64.7 kwa kipindi chote cha miaka miwili kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa vya matibabu.

Ukaguzi huu maalum ulibaini kuwa, fedha za afya zinazotengwa katika bajeti kwa ajili ya madawa na vifaa hazitolewi kwa Bohari ya Madawa (MSD) kama inavyokuwa kwenye bajeti. Kati ya fedha zilizotengwa katika bajeti, kiasi cha Shilingi bilioni 148.3 ni kiasi cha Shilingi bilioni 132.2 zilizotolewa kwenda MSD kwa ajili ya madawa na vifaa vya matibabu kwa kipindi chote cha miaka miwili.

Ilionekana pia, kiasi cha fedha kinachopolekwa MSD kwa ajili ya madawa na vifaa kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, siyo kiasi kinachoripotiwa na Wizara hiyo kwenda MSD. Kulionekana kuwepo na tofauti ya jumla ya Shilingi milioni 658.9 ikiwa ni pungufu ya kiasi ambacho kilipokelewa na kuripotiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwenda MSD lakini ushahidi wa kupokelewa haukutolewa. Pia kulikuwa na kiasi cha Shilingi milioni 100 kilichopokelewa na MSD kutoka

Wizara ya Afya na kikatumiwa na MSD bila kuwepo na unyambulisho/mchanganuo wa matumizi.

Ukaguzi maalum ulibaini pia kuwepo na kiasi cha Shilingi bilioni 4.5 zilizotoka Hazina kwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kununua madawa na vifaa vya hospitali, lakini kiasi cha Shilingi bilioni 4.344 tu ndicho kilichopokelewa na MSD ikiacha Shilingi milioni 196 bila kuwepo na ushahidi wa kupokelewa na MSD kutoka Wizara ya Afya.

11.3.2. Serikali Haijalipa Deni la Shilingi Bilioni 40 kwa MSD Hadi Kufikia Octoba, 2011

Serikali ilikuwa inadaiwa na MSD kiasi cha Shilingi bilioni 30.4 hadi kufikia tarehe 30/6/2011, deni ambalo limetokana na malimbikizo ya gharama za kuhifadhi na kutoa madawa na vifaa vya hospitali vinavyoingizwa nchini. Deni hilo limekuwa likiongezeka kuanzia mwaka 2006/2007. Serikali imekuwa hailipi madeni hayo hadi ilipoamua kupunguza kiasi cha deni mwaka 2010/11 kwa kulipa kiasi cha Shilingi bilioni sita (6). Kwa mujibu wa hesabu za MSD, hadi kufikia Oktoba, 2011 deni hilo limeongezeka na kufikia Shilingi bilioni 40.

11.3.3. Kutokupatikana kwa Madawa Muhimu na Kuwepo kwa Usambazaji Dawa na Vifaa vya Hospitali Visivyo na Kiwango Kutoka MSD

Madawa na vifaa vya matibabu ambavyo matumizi yake ni muhimu na huhitajika kila siku katika hospitali na vituo vya afya vilikuwa vimekwisha kwenye stoo za vituo vya hospitali zilizopo chini ya MSD. Vifaa na madawa yaliyokuwa yamekwisha ni pamoja na vifaa vya kukausha damu wakati wa operesheni na dawa za mseto za malaria (ALU).

Ilibainika pia kuwa, baadhi ya vifaa vinavyotolewa na MSD vimekuwa havina viwango vinavyostahili, kwa mfano vifaa vya kupima Shinikizo la damu na Machela za kubebea wagonjwa zilizotolewa kwa mganga mmoja wa Wilaya (DMO), viliharibika kabla ya muda uliokusudiwa. Kulikuwa na dawa aina ya Kwinini ambazo hazikuwa zimehifadhiwa vizuri hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu, pamba na vitambaa vya kuzuia utokwaji damu ambavyo vilikuwa ni vyepesi kiasi cha kutofaa kwa matumizi kama inavyotarajiwa.

Ilionekana kuwa, tarehe 30 Juni, 2011 MSD ilikuwa na salio la kiasi cha Shilingi bilioni 16 zilizokuwa zimewekwa kwenye akaunti za benki kwa ajili ya kununulia madawa na vifaa vya matibabu kwa ajili ya hospitali na vituo vya afya, na wakati huo huo, vituo hivyo vya Afya na hospitali nyingine zikikabiliwa na uhaba wa madawa na vifaa vya matibabu kama vile dawa za mseto za malaria (ALU) na vifaa vya kuzuia utokwaji damu wakati wa operesheni. Hali hii hupelekea vituo hivyo vya afya kulazimika kutafuta njia nyingine za kununua dawa na mahitaji mengine kwa kutumia vyanzo vingine vya mapato wakati fedha za mahitaji ya dawa na vifaa vya matibabu ya vituo hivyo zimeshikiliwa kwenye akaunti za benki na MSD.

11.3.4. Mapungufu Yaliyoonekana Katika Kuzingatia Sheria ya Manunuzi

MSD ilipitisha zabuni tisa (9) kati ya kumi na sita (16) zilizokaguliwa ambazo hazikuwa zimejumuishwa kwenye mpango wa mwaka wa manunuzi (APP). Zabuni hizo zilikuwa na jumla ya manunuzi yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.9, dola za Kimarekani milioni 9.4 na nyingine zenye thamani ya Euro elfu 99.60.

Bohari ya Madawa ilifanya manunuzi kwa kutumia njia ya chanzo kimoja bila kuwepo na sababu zilizopelekea kufanya hivyo kinyume na Kanuni ya 69(7) ya GN.97 ya

mwaka 2005. Manunuzi yaliyofanyika na kuonekana kuwa na mapungufu hayo ya sheria ya manunuzi yalikuwa ya Shilingi milioni 20, dola za Kimarekani milioni 4.6 na mengine ya Euro milioni 1.5.

Kulikuwa pia na manunuzi yaliyofanywa kwa mikataba yenye jumla ya Shilingi bilioni 3.9, dola za Kimarekani milioni 9.3 na mengine ya Euro milioni 1.5 ambayo hayakupitishwa na Bodi ya zabuni ya MSD kinyume na Kifungu cha 30 (C) cha Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni ya 40 ya (GN) 97 ya mwaka 2005.

Kwa upande mwingine, MSD ilipitisha zabuni nane (8) za manunuzi katika kipindi cha mwaka 2009/2010 na 2010/2011 ambazo zilifanyiwa tathmini na mjumbe mmoja tu wa Kamati ya Tathmini kinyume na kifungu namba 37 cha Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004. Kifungu hicho kinataka kuwa, tathmini ya zabuni ifanywe na wajumbe wasiopungua watatu wa Kamati ya Tathmini. Zabuni zilizofanyiwa tathmini na mjumbe mmoja kinyume cha sheria zilikuwa za Shilingi milioni 134.4, Dola za Kimarekani elfu 10 na nyingine zenye thamani ya Euro milioni 1.5 katika kipindi cha miaka miwili iliyokaguliwa yaani 2009/2010 na 2010/2011.

SURA YA KUMI NA MBILI

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

12.0 Mtazamo wa Jumla

Sura hii inazungumzia hitimisho na mapendekezo yaliyotolewa katika ukaguzi na ambayo kimsingi yanahitaji kufanyiwa maamuzi na Serikali, Bunge, Viongozi wa Mashirika na Bodi za Wakurugenzi zinazosimamia Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Mapendekezo niliyotoa yanatokana na mamlaka niliyopewa kisheria chini ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008. Kifungu hicho kinanipa uwezo wa kutoa mapendekezo kwa lengo la kuzuia matumizi yasiyo na tija ya fedha za umma, kuboresha makusanyo ya mapato ya serikali na kuondoa upotevu wa mapato ya fedha za serikali kwa uzembe, wizi, ukosefu wa uaminifu, ubadhirifu na kudhibiti vitendo vya rushwa katika mali za umma kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Baada ya kupitia na kuhitimisha kaguzi za hesabu za Mashirika ya Umma 125 na kuziwasilisha kwa wahusika ripoti hizi za kaguzi kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba, 2010, 31 Disemba, 2010 na 30 Juni, 2011 kwa kutumia mamlaka niliyopewa, ninapenda kutoa hitimisho na mapendekezo ya jumla kuhusiana na kaguzi zilizofanyika kwa vipindi husika kama ifuatavyo:-

12.1 Maoni ya Ukaguzi na Ripoti Zilizokamilika

Hadi kufikia tarehe 5 Machi, 2012 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 125 (71%) kati ya kaguzi 176 zinazotakiwa kukakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sababu kuu ya kuchelewa kusainiwa kwa ripoti hizi ni kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi katika baadhi ya mashirika na kuchelewa kuitisha vikao vya Bodi kwa wakati kama sheria

inavyoelekeza. Hali kadhalika, pamekuwepo na ucheleweshwaji wa majibu juu ya hoja za ukaguzi uliopelekea kuchelewesha zoezi la ukaguzi kumalizika kwa wakati.

Katika kaguzi zilizokamilika, kuna mashirika 107 ambayo ripoti zake zimeshasainiwa wakati mashirika 18 yanasubiri hesabu zake kupitishwa na kusainiwa na Bodi za Wakurugenzi. Hesabu 84 (78.5%) za Mashirika ya Umma zilizosainiwa kati ya Hesabu 125 zilipata hati inayoridhisha, Hesabu 12 (11.3%) zilipata hati inayoridhisha zenye masuala ya msisitizo, Hesabu 7 (6.5%) zilipata hati zenye kasoro, na kaguzi za mashirika manne (4) (3.7%) zilipata hati zenye kasoro na masuala ya msisitizo, hakuna shirika lililopata hati isiyoridhisha. Undani na mchanganuo wa maoni haya ya ukaguzi yameainishwa kwenye sura ya pili ya ripoti hii.

12.2 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti Zilizopita

Ripoti nne za miaka iliyopita zinajumuisha mapendekezo mengi, na hadi naandika taarifa hii, mapendikezo 31 hayakuwa yametokelezwa. Serikali haijachukua hatua madhubuti za kutekeleza baadhi ya mapendekezo ambayo yanahitaji uamuzi wa Serikali. Kwa upande mwingine ninakiri kupokea majibu ya Serikali ya ripoti yangu ya mwaka uliopita kupitia barua ya Mlipaji Mkuu wa Serikali ya tarehe 28 Juni 2011 yenye kumbukumbu Na.EB/AG/485/01/VOL.III/31 ambayo hata hivyo haikuonyesha msimamo wa Serikali katika kuhakikisha kwamba mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya Mashirika ya Umma ya mwaka 2009/2010 na za miaka ya nyuma ambayo bado hayajatekelezwa yanafanyiwa kazi.

Ili kuimarisha uwajibikaji na kujituma katika kufanya kazi ni muhimu kuwepo na mabadiliko katika utekelezaji wa mapendekezo yatolewayo katika ripoti

za kila mwaka. Nina imani kubwa na Serikali na Wadau wa Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kuwa watatambua umuhimu wa mapendekezo yaliyotolewa na kuyatafutia ufumbuzi mapema iwezekanavyo.

Ikumbukwe kwamba nia na lengo la kutoa mapendekezo katika ripoti za kila mwaka ni kurekebisha kasoro zilizoonekana ili kuleta ufanisi, njia bora na sahihi za kuendesha Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

12.3 Usimamizi wa Malipo ya Mishahara

Changamoto zinazokabili utaratibu wa malipo ya mishahara ya Vyuo Vikuu vya Umma kwa kiwango kikubwa, zinatokana na mfumo mzima wa usimamizi wa malipo hayo. Kukosekana kwa ushirikishwaji wa idara mbali mbali katika kutayarisha malipo ya mishahara ya Vyuo Vikuu na kutokuwepo mfumo thabiti wa mawasiliano kati ya idara zinazohusika katika mchakato mzima zimechangia kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa kutofautiana kwa taarifa zinazohusu jambo moja. Matatizo hayo yanakuzwa na Serikali kutopeleka fedha za kutosha kumudu kulipia gharama za mishahara ya watumishi wa Vyuo hivyo pamoja na kuchelewa kufanyia kazi taarifa mbalimbali zinazokuwa zikipokelewa miongoni mwa idara na Taasisi zinazohusika kukamilisha mchakato wa malipo. Matokeo kuhusu ukaguzi wa usimamizi wa malipo ya mishahara yapo katika sura ya nne ya ripoti hii.

Mapendekezo

Serikali inapaswa kuwa na mfumo wa kompyuta unaoweza kukusanya taarifa zote kutoka Hazina, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM) na vyuo vikuu vya umma, ili kuwezesha utoaji wa orodha ya mishahara ambayo ni sahihi na hivyo kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma. Serikali itengeneze mfumo wa mishahara ambao utatoa

uwiano sawa ili wahusika wote waweze kuutumia wakati huo huo wapate uwezo wa kubadilisha mabadiliko katika kumbukumbu za watumishi katika mfumo huu wa kompyuta.

Mawasiliano kati ya vyuo vikuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Hazina yanahitaji kuboreshwa. Hazina ijitahidi kujibu barua zinazoelekezwa kwake kutoka vyuoni na kutoa majibu stahiki na kwa wakati. Matumizi ya barua pepe yahamasishwe ili kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na Vyuo Vikuu. Kwa masuala yanayohitaji kutekelezwa haraka, Hazina iweke mfumo wa kuhakikisha kuwa mawasiliano yanafanyika mapema kwa vyuo vinavyohusika.

12.4 Usimamizi wa Sheria ya Manunuzi na Mikataba

Kutungwa kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 kulitoa mfumo wa kisheria unaosimamia na kuanzisha michakato ya manunuzi katika sekta ya Umma. Licha ya kuwepo kwa sheria hii, Mamlaka na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikutekeleza kikamilifu matakwa ya Sheria, ambapo ninaweza kuhitimisha kwamba kuna ufahamu mdogo kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi nyinginezo za Umma katika kutekeleza mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2004 na Kanuni zake za mwaka, 2005. Hii inathibitishwa na matokeo ya ukaguzi yaliyoainishwa katika sura ya sita ya taarifa hii. Zaidi ya hayo, ukaguzi wa Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ulibainisha kuwa, kulikuwa hakuna uzingatiaji kamili wa masharti ya Sheria ya Manunuzi ya Umma na kwamba mchakato wa manunuzi katika baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma haufanywi kwa uwazi, ufanisi na kwa kutilia maanani hali ya uchumi na thamani ya fedha katika shughuli zote za manunuzi. Katika ukaguzi huu, ilibainika kwamba

baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma hazikuwa na usimamizi mzuri wa mikataba ya manunuzi. Kwa upande mwingine, usimamizi wa mikataba ya manunuzi umeonekana kuwa moja ya maeneo hatarishi zaidi ambayo yanahitaji umakini na uboreshaji wa haraka.

Mapendekezo

Majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) pamoja na malengo yake ni kuhakikisha kwamba ukaguzi wa manunuzi unafanyika katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Kazi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imeonekana kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya Umma na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Ninapendekeza pia, kwamba huduma za ukaguzi wa manunuzi katika Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma ziendeele kufanyika bila kukoma na pia Taasisi zilizokwisha kaguliwa zinashauriwa zisibweteke kwa matokeo mazuri ya taarifa za kaguzi walizozipata, ila waendeele kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 zinazingatiwa ipasavyo.

12.5 Usimamizi wa Raslimali

Ukaguzi ulibaini mapungufu katika usimamizi wa rasilimali za baadhi ya Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Baadhi ya mapungufu yalikusishwa uwepo wa madai ya mapato ya muda mrefu yasiyokusanyika, madeni, uwekezaji na utoaji wa mikopo kwa mashirika yasiyo na tija na ambayo hayafanyi vizuri au mengine yakiwa yamefilisika bila kufanya marejesho. Matatizo mengine yalikuwa ni pamoja na usimamizi usiofaa wa fedha taslimu, kutokuwa na umiliki wa kisheria wa rasilimali zisizohamishika na uandaaji wa hesabu usiofuata taratibu za viwango vya kimataifa vya kijasibu.

Mapendekezo

Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Maafisa watendaji wa mashirika wahakikishe wanawekeza kwenye kampuni zinazofanya vizuri na zenye matokeo mazuri ya kibiashara ili kupata faida kwenye uwekezaji. Pia, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma zihakikishe kwamba kunakuwa na umiliki halali wa mali na mitambo. Vile vile, Msajili wa Hazina kwa kushirikia na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wakubaliane kuweka viwango vya uchakavu ambavyo vinaendana na hali halisi ya matumizi na muda wa maisha ya mitambo na mali zinazomilikiwa na Mashirika na Taasisi Nyinginezo za Umma. Pia hesabu ziandaliwe kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ukaguzi.

12.6 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Baadhi ya mashirika ya umma yaliyokaguliwa yalionekana kutofanya upimaji wa utendaji wa wafanyakazi, kuajiri wahasibu au wakaguzi wa ndani ambao hawajathibitishwa kuwa wakuu wa vitengo vya uhasibu na ukaguzi, kutojazwa kwa baadhi ya nafasi za kazi, ucheleweshaji wa uwasilishaji wa makato ya kisheria, kutohibitishwa kazini kwa wafanyakazi, kuondolewa kwa wafanyakazi kutoka orodha ya mishahara ya Hazina, mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za rasilimali watu, miongozo ya utumishi iliyopitwa na wakati, mapungufu mbalimbali katika mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu. Mapungufu yasipofanyiwa kazi kwa wakati yanaweza kupunguza motisha wa kazi na kuzorotesha utendaji wa Mashirika ya Umma.

Mapendekezo

Menejimenti za Mashirika ya Umma zihakikishe kwamba upimaji wa utendaji kazi wa wafanyakazi unafanyika kila mwaka na matumizi ya mfumo wa wazi wa upimaji unasisitizwa. Vitengo vya uhasibu na ukaguzi sharti viongozwe na wahasibu na wakaguzi wenye sifa stahili. Menejimenti za Mashirika ya Umma ziwasiliane na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM) kuhakikisha kwamba vibali vya ajira vinapatikana kwa ajili ya kujaza nafasi zilizo wazi na ambazo ni muhimu kwa ajili ya utendaji wa mashirika hayo. Menejimenti za Mashirika ya Umma zihakikishe kuwa makato yote ya kisheria yanawasilishwa kwa wakati katika taasisi husika, pia wafanyakazi wote wanaostahili kuthibishwa kazini, wathibitishwe kwa wakati kama njia ya kuamsha motisha wa kazi. Menejimenti zihakikishe pia kwamba miongozo ya utumishi inahuishwa. Kumbukumbu za kiutumishi lazima ziboreshwe kwa kutumia mifumo ya kisasa ya Usimamizi wa Rasilimali Watu (HRMS). Zaidi ya hayo, menejimenti za Mashirika ya Umma zihakikishe kwamba orodha za mishahara ya kila shirika inalingana na ile ya Hazina na inatumika kulipia mishahara.

Mwisho, mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu kama vile sera na taratibu, mikakati na mipango, uajiri, mafunzo na uendelezaji wa wafanyakazi, mifumo ya kupima utendaji, motisha kwa wafanyakazi na mazingira ya kazi lazima viundwe vizuri ili kufikia ubora katika usimamizi wa rasilimali watu.

12.6 Utawala Bora

12.7.1 Kuhusu Mapendekezo Yaliyopita

Kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miaka ya nyuma yanayohusu utawala bora inasisitizwa kwamba, ni vyema Serikali ikaweka mikakati ya utekelezaji wa

mapendekezo yaliyokwishatolewa. Mapendekezo yaliyotolewa kwa ajili ya utekelezaji ni pamoja na; kuboresha utendaji kazi wa Bodi za Wakurugenzi kwa kuacha kuteuwa mjumbe wa Bodi kuhudumia zaidi ya bodi moja. Utaratibu huu utawafanya wajumbe wa bodi kutekeleza majukumu yao kikamilifu katika vikao vya Bodi husika na kuhudhuria vikao kwa mujibu wa ratiba; kutenganisha uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi na ule wa Mtendaji Mkuu wa Shirika kutoka kwenye mamlaka moja ya uteuzi; Bodi za Wakurugenzi kuteuliwa kwa wakati baada ya muda kumalizika; kuhimiza na kukuza uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi; kutoa mwongozo wa jinsi ya kulipa posho na ada za Wakurugenzi wa Bodi katika Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo; kutatua tatizo la mgongano wa kimaslahi kwa Gavana wa Benki Kuu kuwa mwenyekiti wa Bodi, wakati Bodi ingetarajiwa kumshauri na kuzuia waheshimiwa Wabunge kutoteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

12.7.2 Mkaguzi kwa Mujibu wa Katiba na Hati ya Ukaguzi

Kama ilivyoielezwa katika sura ya nane, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kikatiba chini ya Ibara ya 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama ilivyofafanuliwa na vifungu vya 5,9,30 na 33 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008 kukagua hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo. Ukaguzi huu unayahusu mashirika yote ambayo serikali ina hisa zaidi ya asilimia hamsini (50%).

Mapendekezo

Serikali kupitia Msajili wa Hazina itoe maelekezo kwa mashirika ya umma yaelewe kwamba mashirika yote ya Umma ambayo serikali ina hisa zaidi ya asilimia hamsini (50%) yanatakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hivyo

mipangilio yeyote kinyume na hilo ni kwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

12.7.3 Bodi ya Wakurugenzi

Katika mwaka huu wa ukaguzi, imebainika kuwa idadi ya wajumbe wa bodi katika baadhi ya Bodi za Wakurugenzi haziendani na matakwa ya sheria zilizoanzisha mashirika hayo. Zaidi ya hayo, imebainika kuwa wajumbe wa bodi za baadhi ya mashirika ya umma wamekuwa wakishiriki katika shughuli za utendaji za mashirika ya umma wanayoyasimamia kinyume na kanuni za utawala bora ambazo zinataka utenganishi wa shughuli za menejimenti yaani shughuli za kiutendaji na shughuli za kiuangalizi za bodi.

Mapendekezo

Bodi za wakurugenzi za Mashirika ya Umma zihakikishe zinafuata sheria zilizoanzisha mashirika ya umma kuhusu suala la idadi inayotakiwa ya wajumbe wa bodi.

Zaidi ya hayo, kwa kuwa bodi ina jukumu la kutunga sera kuhusu masuala yanayoathiri taasisi kama vile kutengeneza mipango, kutengeneza muundo wa uongozi unaofaa, kuhakikisha kwamba shirika liko imara kifedha na kutoa uongozi kwa menejimenti. Inashauriwa kwamba shughuli za kiutendaji za shirika zitekelezwe na menejimenti na bodi iachwe kushughulikia upimaji wa utendaji kazi wa menejimenti kufikia mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati.

12.7.4 Haja ya kuwa na “Database” kwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma

Kwa kuzingatia ukweli kwamba Bodi za Wakurugenzi humaliza muda wake kwa nyakati tofauti, inakuwa vigumu kwa mamlaka za uteuzi kufuatilia kwa urahisi. Hivyo basi, ni maoni yangu kuwa Msajili wa Hazina

atengeneze kumbukumbu “database” ya bodi zote za wakurugenzi ambayo itakuwa imeandaliwa ili kutoa ishara ya kumalizika kwa muda wa bodi ya wakurugenzi na kuiwezesha mamlaka ya uteuzi kupata taarifa mapema kwa ajili ya uteuzi wa bodi mpya kwa wakati.

12.8 Ukaguzi wa Manejimenti

Katika ukaguzi huu ilibainika kwamba Chuo Kikuu cha Dodoma kina mipango mikubwa ya kupanua udahili bila kujali ubora wa huduma. Kwa upande mwingine, imebainika kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania haijawahi kufanya utafiti juu ya kiwango gani huduma zinazotolewa zinawaridhisha wateja.

Ukaguzi menejimenti ya Shirika la Madini (STAMICO) umebaini kuwa matatizo mengi katika sekta ya madini yanachangiwa na kukosekana na mamlaka ya udhibiti katika sekta hii ambayo imesababisha kutokuwepo kwa fursa sawa kwa washikadau.

Mapendekezo

Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dodoma iweke ulinganifu kati ya kupanua udahili wa wanufunzi na kupanua idadi ya shahada za uzamili dhidi ya ongezeko la idadi ya wakufunzi.

Inashauriwa pia kuwa menejimenti ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasilino ifanye utafiti kupima jinsi gani watumia huduma za mawasiliano wanaridhika na huduma hizo kwa kuhakikisha kwamba mamlaka ina taarifa zinazohitajika kupima ubora wa huduma kwa ufanisi na kwa wakati.

Serikali ifikirie uwezekano wa kuanzisha Mamlaka ya udhibiti wa madini ambayo itakuwa inasimamia shughuli zote za madini chini ya Sekta ya Madini

Tanzania na iweke usawa wa uendeshaji wa shughuli za madini kwa washikadau wote.

Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuliunda upya Shirika la Ndege, kulipatia fedha za kutosha kwa ajili ya kuliwezesha kufanya kazi zake vizuri. Hata hivyo, Shirika la Ndege la Tanzania lina wafanyakazi wengi ambao hawatumiki kutokana na kupungua kwa shughuli za shirika na hivyo kuwa ni gharama kwa Serikali. Ni maoni yangu kwamba, kama shirika litaweza kuundwa upya na likapewa mtaji wa kutosha na likawa na uongozi bora na madhubuti, na kusiwepo na muingiliano wa kiutendaji, shirika litafanya kazi vizuri na kurudisha imani ya watanzania.

12.9 Matokeo ya Ukaguzi Maalum

12.9.1 Shirika Hodhi la Mali za Serikali (CHC)

Msajili wa Hazina na Wizara ya Fedha kama wawakilishi wa Serikali katika kusimamia Mashika ya Umma na Taasisi Nyinginezo za Umma ambazo Serikali ina hisa, hawatakiwi kujihusisha kufanya maamuzi katika Mashirika na Taasisi hizo ili kuepuka mgongano wa kimaslahi.

Madai yanayopokelewa kwa ajili ya malipo yanatakiwa kuchunguzwa kwa umakini ili kuhakiki usahihi wake na vyanzo vya madai hayo ili kuiwezesha Serikali kupata tija na thamani halisi ya fedha katika malipo hayo.

Menejimenti ya CHC ihakikishe kwamba kunakuwa na njia bora za kuhakiki madeni ili kutambua uwepo wa madeni hayo kabla ya kufanya maamuzi ya kuyafuta, Menejimenti pia, inapaswa kuwa makini katika kusimamia mikataba ya Shirika hilo.

12.9.2 Chuo Cha Ubaharia Dar es Salaam (DMI)

Menejimenti ya Chuo cha Ubaharia Dar es Saalam (DMI) inapaswa kuhakisha kwamba, Sheria za fedha zinazingatiwa katika matumizi ya fedha za Umma. Kiasi chote cha fedha ambacho kililipwa kinyume na Sheria za Fedha na zilizotumika kwenye matumizi yanayotia shaka na fedha zilitumika kulipia matumizi mengine badala ya madeni ya Chuo zirejeshwe na kutumiwa katika matumizi halali kama ilivyokuwa imepangwa. Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watumishi wa Chuo waliohusika na matumizi hayo mabaya ya fedha za Umma.

Chuo cha DMI kinapaswa kifuatake taratibu za ajira zinazotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM) na stahili za Watumishi zifuatake Sheria za utumishi za chuo (Scheme of Service). Uongozi wa chuo unatakiwa kutafuta ufumbuzi wa kujua ziliko kompyuta zilizotolewa kama msaada chuoni hapo. Menejimenti ya Chuo ihakikishe pia hatua za kinidhamu zinachukuliwa kwa mtumishi aliyehusika na wizi wa vifaa vya kompyuta katika maabara ya chuo cha Ubaharia (DMI).

12.9.3 Bohari ya Madawa (MSD)

Wizara ya Afya ihakikishe kuwa kiasi cha fedha kinachopokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya manunuzi ya dawa na vifaa vingine vya matibabu kinawasilishwa MSD kama kilivyotolewa na Hazina na siyo kufanyiwa matumizi mengine na Wizara. Menejimenti ya MSD inapaswa kuhakikisha kwamba madawa muhimu na vifaa kwa ajili ya matibabu vinapatikana wakati wote bila kupungua, Menejimenti inapaswa pia kuhakikisha kuagiza madawa na vifaa vya matibabu ambavyo vinakiwango kinachotakiwa kuepuka madhara kwa binadamu na matumizi mabaya ya fedha. Menejimenti ya MSD inapaswa pia kuhakikisha kuwa inawasilisha dawa kwa wadau mapema kuepuka madawa kumaliza

muda wa matumizi na kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 pamoja na kanuni zake za mwaka 2005.

12.10 Maendeleo ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mashirika Yaliyobinafsishwa

Serikali inapaswa kuharakisha mchakato wa ubinafsishaji wa Mashirika ambayo bado ubinafsishaji wake haujakamilika ili fedha itakayotokana na mauzo hayo zitumike kulipa mikopo ili kuiondolea mzigo Serikali kutokana na mikopo ambayo imedhamini.

Inashauriwa tena kwamba, Serikali izingatie kuharakisha mchakato wa ubinafsishaji wa mashirika 34 ili kuepusha mali za mashirika haya kuendelea kuchakaa na kuharibika zaidi au serikali itengue maamuzi yake ya kubinafsisha mashirika haya na kuyaongezea mtaji wa kutosha ili yaanze kufanya kazi zake.

12.11 Vyanzo vya Uhakika vya Fedha kwa Ajili ya Uwekezaji

Maendeleo ya Taifa lolote lile hutegemea sana uchumi imara. Ili kufikia lengo hili upatikanaji wa vyanzo vya kuaminika vya fedha kwa ajili ya uwekezaji ni wa muhimu sana. Tanzania tuna fursa nyingi ambazo bado hazijatumika kikamilifu na ambazo zinaweza kuwa vyanzo vya fedha kwa ajili ya uwekezaji. Vyanzo hivi ni kama vile Soko la Mitaji, ubia kati ya watu binafsi na Serikali, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na fedha na mali ambazo zimetelekezwa na wamiliki wake.

Kwa sasa Soko la Hisa la Dar es Salaam lina idadi ndogo ya makampuni ambayo yamejisajili. Hii imesababishwa na kutokuwa na uelewa kwa baadhi ya makampuni na watanzania kwa ujumla. Kwa upande mwingine mifuko ya Hifadhi ya Jamii inaweza kutoa fedha za maendeleo katika sekta mbalimbali za kiuchumi kama ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo na vitu vingine kama

hivyo. Serikali inaweza kutafuta uwezekano wa kuwa na ubia na taasisi binafsi katika mipango ya kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Nimebaini kwamba, kuna fedha nyingi katika taasisi mbalimbali ambazo zimebaki bila kudaiwa na wenyewe kwa muda mrefu na ambazo kimsingi wenyewe hawapo. Fedha hizi ni pamoja na akiba za wateja zilizoko kwenye mabenki, hisa ambazo hazina wamiliki katika Soko la Hisa la Dar es Salaam, makato ya kisheria kwa wafanyakazi walioachishwa kazi au kufariki ambao makato yao yanaendelea kupelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii mifuko ya bima ya afya na gawio kwa makampuni yaliyosajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es salaam. Kimsingi rasilimali hizi si mali ya taasisi hizi ila ni mali ya wamiliki wasiojulikana. Kama rasilimali hizi zitaachwa bila uangalizi makini kuna hatari ya kutumiwa vibaya au zinaweza kubaki bila kutumiwa.

Serikali inapaswa kuwa na mpango mkakati wa kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ili iweze kutekeleza shughuli za kimaendeleo nchini. Tanzania ikiwekeza kwenye miradi ya maendeleo, ajira zaidi zitaundwa, wigo wa mapato utapanuka na hivyo kuwawezesha watu na kuondoa umaskini. Pasipokuwa na uwekezaji wigo wa kodi hautapanuka

Mapendekezo

Tanzania kama Taifa linaloendelea lazima libuni mkakati wa upatikanaji wa fedha za uwekezaji kwa gharama nafuu. Kuna haja ya Serikali kutunga sheria itakayoyataka makampuni makubwa hapa Tanzania kusajiliwa katika Soko la Hisa la Dar es salaam. Mfano wa makampuni haya ni kama makampuni ya uchimbaji madini, makampuni ya simu za mkononi, makampuni ya saruji, makampuni ya vinywaji baridi n.k .

Kuwepo kwa idadi kubwa ya washiriki katika Soko la Hisa inaweza kuwa ni chanzo kikuu cha fedha kwa ajili ya maendeleo ya Taifa kupitia mauzo ya hisa.

Makampuni makubwa na watu binafsi wanaweza kupata mitaji kwa ajili ya uwekezaji kutoka kwenye Soko la Hisa la Dar es salaam.

Fedha za mifuko ya jamii ni za wanachama, kwa hiyo umakini unatakiwa kuhakikisha kwamba uwekezaji unafanywa katika biashara zenye manufaa, na maandiko ya uwekezaji yanaandaliwa vizuri, yanachambuliwa kwa umakini, yanaidhinishwa bila muingiliano wa kisiasa katika maamuzi.

Umakini unatakiwa wakati wa kuingia katika mikataba ya aina hiyo kwani baadhi ya wawekezaji si waaminifu na wanaweza kukiuka makubaliano. Marejesho ya gharama za huduma hii yanaweza kupatikana kupitia ulipaji wa kodi za barabara.

Kuna haja ya Serikali kutunga sheria itakayozitaka taasisi za umma kurejesha Hazina mali ambazo hazijadaiwa na wenyewe ili ziwe mapato ya Serikali kama ilivyo kwa akiba ambazo zimekaa bila kutumika kwa zaidi ya miaka mitano (5) na hazitarajiwi kutumika. Fedha hizo ambazo hazina wamiliki zingeweza kuwekwa katika Mfuko Maalum wa Uwekezaji ili zitumike kama chanzo cha fedha za uwekezaji.

Fedha zinaweza zikatokana na gawio kutoka kwenye uwekezaji wa umma, mapato yatakayotokana na mauzo ya mali za Serikali yanaweza pia kuwa chanzo cha fedha katika Mfuko wa Uwekezaji wa Umma ili kuongeza ukwasi. Kwa upande mwingine Serikali inaweza ikawa na tengo katika bajeti zake za mwaka kwa ajili ya kutunisha mfuko huu. Kwa hali hiyo basi, Serikali inapaswa iweke msisitizo katika kuelekeza mapato yake kufadhili mfuko huu kwa kuwa haitatokea siku mapato ya Serikali yakatosheleza.

Orodha ya makampuni binafsi yanayokagua Mashirika ya Umma

S/N	Jina la Kampuni
1.	AA - Adolph Associates
2.	ABA Alliance
3.	AMAS Associates
4.	ATAM Consultancy
5.	ABS Consultants
6.	ATEKAY Accountants and Auditors
7.	Auditax International
8.	BK Associates & David Malishee
9.	BAAS Associates & EVK
10.	Citizen Certified Partners Consortium
11.	Co-operative Audit and Supervision Corp
12.	CT & Assocites & Chabegan & Associates
13.	BDO
14.	Deloitte & Touche
15.	Ernst & Young
16.	Elite Financial Managers
17.	Fincare & Company
18.	Global Finance and Business Solution
19.	Globe Accountancy Services
20.	Global Auditing and Management Solution
21.	ISM Consultants
22.	INNOVEX Auditors
23.	KPMG
24.	Martec & Company
25.	MATSAB & Company
26.	MEKONSULT Auditors
27.	MGK Certified Public Accountants
28.	MM Micro Business Consultants
29.	MURL-AATEC Associates
30.	PAN Associates
31.	Paul Clem Associates
32.	PIMA ASSOCIATES
33.	PKF Tanzania
34.	PricewaterhouseCoopers
35.	Philips & Company
36.	Quintex Financial Services
37.	R&S Associates
38.	RSM Ashvir
39.	Reliable Consultants,

S/N	Jina la Kampuni
40.	RS & Partners
41.	SBC Consultancy Services
42.	Shebrila & Co
43.	TAB Consultants
44.	Tanna Sree Kumar Co.
45.	TAG System Associates
46.	Tax Pro Associates
47.	TAC Associates
48.	TANSCOTT
49.	TMC Associates/TOP Consultants Consortium
50.	Trion & Company
51.	VA Business Assurance Services
52.	WISCON Associates

Aina ya Maoni ya Ukaguzi yaliyotolewa 2010/2011

	Hati Inayoridhisha
Na.	Shirika au Taasisi
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga
2.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha
3.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana
4.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)
5.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavuu na Majini (SUMATRA)
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Moshi
7.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania
8.	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama Shinyanga
10.	Bodi ya Sukari Tanzania
11.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama
12.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)
13.	Halmashauri ya Wafugaji Ngorongoro
14.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)
15.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)
16.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro
17.	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRPD)
18.	Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)
19.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)
20.	Bodi ya Korosho Tanzania
21.	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)
22.	Benki Kuu ya Tanzania
23.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)
24.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
25.	Bodi ya Chai Tanzania
26.	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi
27.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi
28.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba
29.	Baraza la Taifa la Uwezesaji wa Kiuchumi (NEEC)
30.	NHC/PPF IPS Building
31.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu Majenzi (AQRB)
32.	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha (AICC)
33.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza
34.	Baraza la Kiswahili Tanzania
35.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma
36.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)
37.	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)

38.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro
39.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya
40.	Bodi ya Pamba Tanzania
41.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati
42.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga
43.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma
44.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)
45.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa
46.	Shirika la Hifadhi Za Tanzania (TANAPA)
47.	Tume ya Ushindani (FCC)
48.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi
49.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania
50.	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro
51.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha
52.	Benki ya Twiga
53.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)
54.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF)
55.	Baraza la Taifa Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
56.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)
57.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida
58.	SNOTASHIP
59.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi (NLPC)
60.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Rukwa
61.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
62.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora.
63.	Chuo cha Ustawi wa Jamii
64.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu
65.	Chuo Kikuu Mzumbe
66.	Chuo Cha Elimu ya Biashara
67.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania
68.	Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMETRAC)
69.	Chuo cha Ardhi
70.	Chuo Cha Usafirishaji (NIT)
71.	Bodi ya Katani Tanzania
72.	Chuo cha Ufundi Arusha
73.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
74.	Bodi ya Manunuzi (PSPTB)
	Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo
Na.	Shirika/Taasisi
1.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)
2.	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)
3.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)

4.	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)
5.	TPRI
6.	Benki ya Raslimali Tanzania
7.	Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma
8.	Benki ya Posta Tanzania
9.	Bodi ya Tumbaku Tanzania
10.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)
11.	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko
	Hati Isiyoridhisha
Na.	Shirika/Taasisi
1.	Shirika la Magazeti Tanzania.
2.	Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka Musoma
3.	Shirika la Elimu Kibaha
4.	Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka Songea
5.	Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka Mtwara
6.	TAWIRI
7.	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO)
	Hati Isiyoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo
Na.	Shirika/Taasisi
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar-es-salaam(DAWASA)
2.	Shirika la Posta Tanzania
3.	Shirika la Maji Dar es salaam (DAWASCO)

Hali halisi ya Ukaguzi

A	Taasisi za Fedha, Mifuko ya Pensheni na Kampuni za Bima	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unae- ndelea	Kuhakiki Ubora wa Kazi	Hesabu Zinasubiri Kupiti- shwa na Bodi ya Wakuru- genzi	Ripoti Zilizoka milika	Maoni
1.	Benki Kuu ya Tanzania (BOT)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF).	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
3.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
4.	Local Authority Provident Fund	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
5.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
6.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma. (PPF)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
7.	Mfuko wa Mafao ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
8.	Benki ya Raslimali Tanzania (TIB)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

9.	Benki ya Posta Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Benki ya Twiga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
11.	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Shirika la bima la Taifa (NIC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
14.	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
15.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Hisa na Mitaji (CMSA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
16.	Mamlaka ya Usajili wa Bima Tanzania (TIRA)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	

B	Taasisi za uzalishaji	Hesabu zimepo kelewa	Ukaguzi unae-ndelea	Kuhaki-ki bora wa kazi	Hesabu zinasu-biri kupitishwa na bodi ya wakuru-genzi	Ripoti zilizoka milika	Maoni
1.	Taasisi ya Taifa ya Sukari	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
2.	Mamlakaa ya Hifadhi ya Ngorongoro	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
3.	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
4.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
5.	Kampuni ya Mbolea Tanzania.	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Hakuna Bodi
6.	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
7.	Shirika la Mafuta Tanzania (TPDC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
8.	Kampuni ya Ranch za Taifa (NARCO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
9.	Shirika la Magazeti Tanzania.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Shirika la Nyumba Tanzania	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
11.	Ubungo Plaza Co. Ltd	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	-

12.	NHC/PPF IPS Building	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Shirika la posta Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14.	Shirika la Tija la Taifa (NIP)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
15.	Shirika la Kutengeneza Magari (NYUMBU)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	Hakuna Bodi
16.	Taasisi ya Idara ya Madawa	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
17.	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
18.	Ngorongoro pastoralist Council	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

C	Bodi za Udhhibiti, Mabaraza, Kamisheni, na Mamlaka	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unaendelea	Kuhakiki Ubora wa Kazi	Hesabu Zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizokamilika	Maoni
1.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu majenzi (AQRB)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
3.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi (NLPC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
4.	Shirika la Nguvu za Atomic	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
5.	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
6.	Tume ya Ushindani (FCC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
7.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
8.	Baraza la Kiswahili Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
9.	Benjamin William Mkapa Foundation	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
10.	Bodi ya Biashara ya Nje (TANTRADE)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	

11.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Bodi ya Usajili ya Wakandarasi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Bodi ya Usajili ya Wahandisi	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
14.	Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na maji (Ewura)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
15.	Bodi ya michezo ya kubahatisha Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
16.	Baraza la sanaa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
17.	Bodi ya Taifa ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
18.	Bodi ya manunuzi (PSTB)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
19.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa elimu ya juu.	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
20.	Baraza la Ujenzi la Taifa. (NCC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
21.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Baraza la Taifa la uwezesaji wa kiuchumi (NEEC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
23.	Baraza la mitihani Tanzania (NECTA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

24.	Baraza la Michezo Tanzania	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
25.	Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
26.	Bodi ya Pareto Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
27.	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji. (RUBADA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
28.	Bodi ya sukari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
29.	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
30.	Bodi ya katani Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
31.	Shirika la Viwango Tanzania. (TBS)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Hakuna Bodi
32.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
33.	Bodi ya Korosho Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
34.	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
35.	Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na Majini (Sumatra)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
36.	Mamlaka ya anga Tanzania (TCAA)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
37.	Bodi ya kahawa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

38.	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania(TCU)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
39.	Mamlaka ya Kudhibiti manunuzi ya Umma (PPRA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
40.	Mamlaka ya udhibiti Mawasiliano Tanzania. (TCRA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo -	
41.	Bodi ya Pamba Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
42.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
43.	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
44.	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania(TFNC)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	Hakuna Bodi
45.	Tanzania Marine Parks	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
46.	Bodi ya Chai Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
47.	Bodi ya Utalii Tanzania	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Hakuna Bodi
48.	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
49.	Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania. (EPZA)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
50.	Shirika la Haki Miliki Tanzania. (COSOTA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
51.	Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma(CHC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	Hakuna Bodi

52.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
53.	Kampuni ya Kusimamia Rastimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Hakuna Bodi
54.	Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
55.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
56.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu. (SUMATRA CCC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
57.	Mamlaka ya Udhhibiti ya Mifuko ya Kijamii Tanzania (SSRA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
58.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA),	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
59..	Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
60.	Bodi ya Maziiwa Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
61.	Bodi ya Usajili wa Maghala Tanzania (TWLB)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	

D	Vyuo vya elimu ya juu, Tafiti, Mafunzo	Hesabu zimepo kelewa	Ukaguzi unaendelea	Kuhakiki ubora wa kazi	Hesabu zinasubiri kupitishwa na bodi ya wakurugenzi	Ripoti zilizoka milika	Maoni
1.	Chuo Kikuu cha Ardhi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Chuo Cha Elimu ya Biashara	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
3.	Chuo cha Technologia Dar es salaam	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
4.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
5.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
6.	Chuo cha Uhasibu Arusha	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Hakuna Bodi
7.	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
8.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	Hakuna Bodi
9.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
11.	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Shirika la Elimu Kibaha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

13.	Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14.	Chuo Kikuu Cha Mkwawa	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	
15.	CARMATEC	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
16.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
17.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUCHS)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
18.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
19.	Chuo Kikuu cha Mzumbe	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
20.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
21.	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
23.	Chuo Kikuu Cha Sokoine.	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
24.	Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
25.	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
26.	Arusha Technical College	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
27.	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	

28.	Chuo Kikuu cha Dodoma	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
29.	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
30.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
31.	Taasisi ya Utafiti na Uvuvi Tanzania (TAFIRI)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
32.	Taasisi ya Utafiti ya Wanyama Pori (TAWIRI)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
33.	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
34.	Centre for Foreign Relation	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
35.	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
36.	Shirika la Utangazaji Tanzania(TBC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

E	Mashirika ya Kutoa Huduma	Hesabu zimepo kelewa	Ukaguzi unaendelea	Kuhakiki ubora wa kazi	Hesabu zinasubiri kupitishwa na bodi ya wakurugenzi	Ripoti zilizoka milika	Maoni
1.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
2.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
7.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
9.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

11.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
12.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
14.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
15.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
16.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
17.	Marine Services Company	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	Hakuna Bodi
18.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
19.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbinga	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
20.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Rukwa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
21.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
22.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
23.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
24.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
25.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

26.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tukuyu	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
27.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kyela	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
28.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Ngara	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
29.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Korogwe	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
30.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mpanda	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
31.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
32.	Shirika la Masoko ya Kariakoo	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
33.	Maktaba Kuu ya Taifa	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-	
34.	Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
35.	Usafiri Dar-es-Salaam (UDA)	No	-	-	-	-	Umiliki wa serikali haelew eki.
36.	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-	Hakuna Bodi
37.	Shirika la Ndege Tanzania (ATC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	Hakuna Bodi
38.	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

39.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
40.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
41.	Makumbusho ya Taifa	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-	
42.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura CCC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
43.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
44.	Chinese -Tanzania Joint Shipping Company (SNOTASHIP)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	
45.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama shinyanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo	

Mashirika Yaliyotengwa kwa ajili ya Kubinafsishwa Lakini bado Ubinafsishaji wake Haujakamilika

N	Shirika
1.	Shirika la Reli Tanzania,
2.	Shirika la Bima Tanzania,
3.	Benki ya Biashara ya Taifa,
4.	Shirika la Posta Tanzania
5.	Shirika la Simu Tanzania
6.	Kampuni ya Kusaidia Maendeleo Tanzania
7.	Shirika la Ndege Tanzania,
8.	Mashamba ya Mahindi Namtumbo
9.	West Kilimanjaro -NAFCO (Harlington, Fosters, Kanamodo na Journeys End)
10.	Mashamba ya Kahawa Mbozi,
11.	Loji ya Mikumi,
12.	Hoteli ya New Africa
13.	PEHCOL
14.	Kampuni ya Mwananchi Engeering Conctruction Company
15.	Kampuni ya Usagishaji ya Taifa,
16.	Usafiri Dar es salaam,
17.	Aluminium Africa
18.	Kiwanda cha Matofali Kisarawe,
19.	Kampuni ya Huduma za Majini Tanzania,
20.	Kiwanda cha Mataili Tanzania,
21.	BP (T) LTD
22.	Kiwanda cha Sementi Mbeya
23.	Kiwanda cha Sukari Tanzania,
24.	Kiwanda cha Sukari Kilombero,
25.	TANSCAN LTD
26.	TANGOLD Korogwe
27.	Kiwanda cha Ngozi Morogoro,
28.	Kampuni ya Maji Songwe,
29.	Kampuni ya Madawa Keko,
30.	Maghala ya Kutunza Madawa ya Korosho,
31.	Viwanda cha Nyama i. Mbeya ii. Kitaraka Singida iii. Kawe DSM
32.	Benki ya Makabwela,
33.	Kampuni ya Kutunza Petiroli Tanzania.
34.	Shirika la Reli Tanzania,

Mshirika ya Umma Ambayo Hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi

Na	Jina Shirika
1.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
2.	Shirika la Viwango Tanzania
3.	Taasisi ya Taifa ya Uzalishaji
4.	Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania
5.	Shirika Hodhi la Reli
6.	Hospitali ya Taifa Muhimbili
7.	Chuo cha Uhasibu Arusha
8.	Kiwanda cha Mbolea Tanzania
9.	Kampuni ya Hudhuma za Majini
10.	Shirika Hodhi la Rasilimali za Serikali
11.	Bodi ya Utalii Tanzania
12.	Shirika la Ndege Tanzania